**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA PILI**

**KIKAO CHA NANE – TAREHE 16 FEBRUARI, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA HAIDI MKULO):**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Benki ya Posta Tanzania kwa Mwaka 2004 *(The Annual Report and Accounts of the Postal Bank of Tanzania for the year 2004)*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 83

**Kifuta Machozi kwa Waathirika wa Maandamano**

**MHE. ALI SAID SALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 2003 Serikali ilitamka Bungeni kuwa ina mpango wa kutoa kifuta machozi kwa wananchi walioathirika na matukio ya maandamano ya tarehe 26/1/2001 na 27/1/2001, lakini iko katika matayarisho na pindi itakapokamilika wahusika wataarifiwa na kwa kuwa hadi swali linapoulizwa hakuna taarifa yoyote iliyotolewa na Serikali kwa wahusika:-

Je, Serikali sasa inasema nini juu ya hatma ya waathirika hao wakiwemo yatima na vizuka?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa vile leo ni siku yangu ya mwisho kujibu maswali katika Mkutano huu wa pili kwenye vikao vyake, nichukue fursa hii kwanza kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika, kwa umahiri wenu na hekima katika kusimamia na kuendesha Bunge lako Tukufu. Pia napenda nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye ndiyo kiongozi wa shughuli za Bunge katika usimamiaji wake wa shughuli hizi kwenye mkutano huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani kama ifuatavyo:-

Ni kweli kumbukumbu zinaonyesha kuwa tarehe 4 Novemba, 2003, Bunge hili Tukufu liliarifiwa kuhusu matukio ya tarehe 26 na 27 Januari, 2001 na kwamba baada ya uchunguzi kufanyika na matokeo kuwasilishwa Serikalini, ilikubalika kimsingi kuwa matukio ya siku hizo mbili hayakuwa maandamano kama Mheshimiwa Mbunge anavyodai na kwamba kifuta machozi na siyo fidia. Naomba nirudie, "ilikubalika kimsingi kuwa matukio ya siku hizo mbili hayakuwa maandamano kama Mheshimiwa Mbunge, anavyodai na kwamba kifuta machozi na siyo fidia ndicho kitolewe kwa walioathirika au jamaa na za waathirika".

Mheshimiwa Spika, jitihada zimeendelea kufanywa tangu kipindi hicho kwa kushirikiana na Jumuiya ya Madola ili kupitia Mfuko wake wa Ujenzi mpya wa Maridhiano *(Fund for Reconstruction and Reconciliation)* uweze kusaidia kutoa fedha za malipo kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kifuta macho hicho kama anavyoeleza Mheshimiwa Mbunge hakijalipwa hadi sasa, Serikali ya Awamu ya Nne itaendeleza jitihada hizi za kufuatilia na kuhakikisha wananchi wanaarifiwa kila hatua itakayokuwa imefikiwa.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa ni kipindi kirefu tokeo Serikali itoe tamko kwamba mipango iko karibu kukamilika na wahusika kulipwa hicho kifuta machozi na tokea muda huo mpaka leo ni zaidi ya miaka mitatu. Je, Serikali haioni kwamba imechukua muda mrefu kuweza kulipa hicho kifuta machozi kwa waathirika na kama hivyo ndivyo kama Serikali imeshindwa si ingekuwa vema Serikali kutoa tamko kwamba imeshindwa kulipa hicho kifuta machozi ili wananchi hao wakate tamaa kabisa kabisa? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuongezea pale ambapo Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu vizuri sana swali hili. Kimsingi si kweli kwamba Serikali imeshindwa kulipa

kifuta machozi. Katika swali la msingi tumeeleza kwamba Serikali inafanya mazungumzo na huu mfuko wa *Fund for Reconstruction na Reconciliation*, mazungumzo haya yanaendelea na hizi fedha zikipatikana wataarifiwa na watalipwa. Suala la muda halipo kwa sababu sisi tumeomba kwenye mfuko huu wao ni maamuzi yao kutupatia lakini tunawahakikishia fedha hizi zikipatikana wataarifiwa rasmi na wote hawa watapewa kifuta machozi. Hatusemi lini maana ni mazungumzo yanaendelea. Ahsante. (*Makofi*)

Na. 84

**Kituo cha Afya cha Makorongo**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa majengo mengi ya kituo kipya cha afya cha Makorongo Wilayani Kondoa yamekamilika:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufungua kituo hicho ili wananchi wapate huduma ya tiba iliyokusudiwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Degera Mbunge wa Kondoa Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Kituo cha Afya cha Makorongo ni matokeo ya kutatua tatizo lililoibuliwa na wananchi chini ya uchambuzi shirikishi jamii mwaka 1999. Ujenzi wa kituo ulianza mwaka 2001 chini ya wafadhili wa *World Vision Tanzania*. Serikali imechangia Shilingi 7,000,000/= na michango ya wananchi ni Shilingi 2,000,000/=. Kituo kikikamilika kinategemewa kuhudumia wananchi wapatao 12,763. Mpaka sasa kituo hicho kimekamilisha majengo yafuatayo; majengo ya *OPD* ambayo ni ya wagonjwa wa nje, nyumba tatu za Watumishi na jengo la kliniki. Aidha kazi ambazo zimebakia ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa wodi ya wanaume na wanawake, ujenzi wa mfumo wa maji taka, ujenzi wa jiko la kupikia chakula cha wagonjwa, kujenga chumba cha kuhifadhi maiti, ununuzi wa vifaa vya kitaalam pamoja na kujaza ikama inayostahili kwa kituo cha afya. Kituo hicho kinategemea kukamilika Septemba, 2006.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha shughuli zilizotajwa hapo juu, Kituo cha Afya cha Makorongo kitakuwa tayari kimefikia hadhi ya kuitwa kituo cha afya. Hivyo Serikali itakuwa tayari kukifungua kituo hicho ili kitoe huduma inayostahili kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali, napenda kutoa pongezi za dhati kwa wananchi wa Kondoa Kusini, wakiongozwa na Mheshimiwa Mbunge kwa juhudi kubwa za kuboresha huduma za Afya katika Jimbo hilo.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa majibu yake mazuri. Nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa imechukua muda mrefu sana kukamilika kwa kituo hiki na kwa kuwa kama alivyosema yeye katika jibu lake sehemu ya *OPD* imekwisha kamilishwa, je, isingekuwa busara kwa Serikali kufungua angalau huduma hata ya zahanati ili wananchi waweze kuanza kunufaika na huduma ya afya?

(b) Kwa kuwa kuna zahanati nyingi ambazo zimekwishakamilika katika Jimbo la Kondoa Kusini moja ikiwa Jogolo na nyingine Mwaikisabe na kwa kuwa zahanati hizo pia bado hazijafunguliwa. Je, Naibu Waziri anasema nini kuhusu zahanati hizo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ili kituo cha afya kiitwe kituo cha afya kuna masharti yake lazima yatimizwe na Kituo cha afya cha Makorongo hakijatimiza masharti ya kituo cha afya. Iwapo yatakamilika hayo majengo yaliyobakia ndipo kitaitwa kituo cha afya na kitaanza kutoa huduma. Siyo vizuri kama mpango wa awali ulikuwa ni kujenga kituo cha afya tukakibadilisha ghafla kuwa zahanati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu zahanati ya Jogolo kama nilivyosema kwamba ili iwe zahanati ina masharti yake ambayo yamewekwa na Wizara ya Afya. Kwa hiyo, haiwezi ikafunguliwa bila kutimiza masharti ya kuwa zahanati. (*Makofi*)

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja zito la nyongeza.

Kwa kuwa katika nchi nzima kuna viporo vingi vya kumalizia vituo vya afya na zahanati na imekuwa kero na kwa kuwa kuna miradi mikubwa mizito ya MMES pamoja na MMEM, haingekuwa jambo la busara sasa katika Awamu ya Nne hii kuingiza masuala ya afya na kupata mradi mkubwa wa kuweza kuhudumia mambo ya afya kama zahanati na kadhalika na kuomba mkopo mkubwa kwa sababu imekuwa ni kero kubwa sasa hivi katika nchi hii kumalizia vituo vya afya na zahanati? (*Makofi*)

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, sera ya afya tunayoitumia mpaka sasa ni mwaka 1990 imeonekana ina mapungufu na tunafanya mapitio. Kwa mfano kila kituo cha afya, kinahitajika kuhudumia watu 50,000 na kila *dispensary* watu 10,000 bila kuangalia hao watu wako wapi. Unaweza ukakuta katika maeneo mengine watu 10,000 wamesambaa katika eneo kubwa. Kwa hiyo, sasa hivi tunafanya tathmini na kupitia ili tuangalia *distance* pamoja na uwingi na tutaleta mawazo hapa Bungeni ili yapitishwe kwa sababu tumekuwa na vituo vichache watu wamekuwa wengi na kama alivyosema tuna wazo hilo kwamba tuwe na mradi kama wa MMEM ambao ulifanikiwa ili tujaribu kuboresha huduma za afya kwa wananchi, ahsante. (*Makofi*)

Na. 85

**Televisheni ya Taifa**

**MHE. DIANO M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliahidi kufunga Televisheni ya Taifa katika mwaka wa fedha 2005/2006:-

(a) Je, Serikali inakumbuka ahadi hiyo?

(b) Kama inakumbuka ni lini sasa itafunga *TV* hiyo ili wananchi wa Singida wanufaike na huduma hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MICHEZO NA UTAMADUNI (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inakumbuka ahadi yake ya kujenga mtambo wa Televisheni ya Taifa katika Mkoa wa Singida na inampongeza Mheshimiwa Chilolo kwa kufuatilia kwa karibu. (*Makofi*)

(b) Ujenzi wa kituo cha kupokea na kurushia matangazo cha Singida umo katika Awamu ya Nne ya ujenzi wa Televisheni ya Taifa wenye lengo la kufanya Televisheni ya Taifa ionekane nchi nzima kwa ukamilifu. Mpango huu unahusisha pia Mikoa ya Ruvuma, Rukwa, Shinyanga, Iringa, Morogoro, Kilimanjaro na Manyara. Kukamilika kwa mpango huu kutawezesha watu wa Singida na Mikoa niliyoitaja kunufaika na matangazo ya Televisheni ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Wizara yangu katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007 itatenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. (*Makofi*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali iliahidi kutoa huduma hii mwaka 2005/2006.

(a) Je, Serikali haioni kwamba kupeleka mwaka 2006/2007 ni kujichanganya? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa *Channel Ten* nayo inatoa huduma kwa Mikoa mingi hapa nchini. Je, huduma hiyo pia itatolewa lini Mkoa wa Singida? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MICHEZO NA UTAMADUNI (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali haijichanganyi kwa utaratibu huu kwa kuwa imeshaanza kulishughulikia kwa ukamilifu suala hili. Mwaka wa fedha 2005/2006 Serikali ilitenga jumla ya Shilingi 2,900,125,900/= kwa ajili ya mradi huo kwa ajili ya ukamilishaji wa miundombinu na mwaka huu wa fedha itakazotenga ni kwa ajili ya mitambo na uwekezaji wa mitambo hiyo ya televisheni. (*Makofi*)

Ni kweli kwamba *Channel Ten* inapaswa ionekane vizuri nchi nzima lakini kwa kuwa ni mradi wa Kampuni binafsi tutashauriana nao na kuona cha kufanya, ahsante. (*Makofi*)

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo la Singida ni sawa tatizo la Tabora kutokuonekana kwa *TVT* na kutokupatikana kwa *Radio Tanzania.* Walikuja Tabora tukawapa nafasi ya kuweza kufunga mitambo yao. Je, Mheshimiwa Waziri atatuthibitishia vipi nafasi ile ambayo tumewapa mpaka leo hakuna chochote ambacho kinaendelea? (*Makofi*)

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu fedha tuna mpango wa kujenga vituo 7 na tunatarajia mwezi Machi vituo vyote vitakuwa vimemalizika navyo ni Tanga, Lindi, Mbeya, Tabora, Kigoma, Musoma na Kagera.

Mheshimiwa Spika, suala la *Radio Tanzania* pia linashughulikiwa katika mpango wa fedha wa mwaka huu. (*Makofi*)

Na. 86

**Uchumi Ghali**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika vipindi vya bajeti ya 2003/2004 na 2004/2005 iliahidi kulifanyia kazi tatizo la ughali wa uchumi wetu.

(a) Je, nini matokeo ya utafiti huo?

(b) Je, ni hatua gani zilizochukuliwa kupunguza ughali huo wa uchumi?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, swali lake lenye sehemu (a) na(b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haijawahi kuahidi kufanya utafiti kuhusiana na ughali wa uchumi wetu kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge. Aidha, Serikali haioni umuhimu wa kufanya utafiti huo kwa vile hali halisi ya ughali huo ilishajionyesha dhahiri kutokana na malalamiko ya wananchi wa kawaida na wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, suala la ughali wa uchumi lina pande mbili. Kwanza kwa upande wa wawekezaji na pili kwa wananchi wa kawaida. Wawekezaji wamekuwa wakidai kwamba gharama za kufanya biashara nchini ni kubwa hususan kwa upande wa kodi, umeme, maji, mfumo wa sheria na urasimu. Kwa upande mwingine, baadhi ya wananchi wa kawaida wanadai kuwa hawaoni faida zinazotangazwa za kukua uchumi na kutengemaa kwa uchumi jumla kwani hali zao za maisha zinadaiwa kuwa duni kila kukicha.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo matatizo ambayo Serikali iliahidi kufanyia kazi na wala siyo kuyafanyia utafiti katika vipindi vya bajeti vya 2003/2004/2005. Katika jitihada za kuyatatua matatizo hayo, Serikali ilichukua hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kero kwa wawekezaji, Serikali ilichukua hatua zifuatazo:-

1. Kukifanya kituo cha uwekezaji (*TIC*) kuendelea kutoa huduma zake za *one stop centre* na kuziboresha huduma hizo ili kuweza kukidhi matakwa ya wawekezaji wa ndani na nje.

2. Serikali imeboresha mazingira ya kufanya biashara nchini kwa kutekeleza programu ya kuimarisha mazingira bora ya biashara Tanzania *(Business Environment Srengthening for Tanzania BEST programme)* programu hii ilipitishwa tarehe 2002 na ambayo inatekelezwa na kitengo cha taratibu Bora za Biashara kilichopo chini ya Wizara yangu.

3. Serikali imeanzisha Baraza la Mashauriano la Taifa baina ya Serikali na Sekta Binafsi *(Tanzania National Business Council)* mbapo Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi chini ya mwamvuli wa *TNBC* imeshughulikia yafuatayo:-

    - Imefanya mapitio na marekebisho ya mfumo wa kodi yaliyowezesha kupitishwa kwa sheria ya kodi ya mwaka 2004 ambayo inampa unafuu mwekezaji;

    - Imeondoa adha ya utozaji wa kodi nyingi; na

    - Kupunguza urasimu katika kutoa leseni.

Mheshimiwa Spika, ni vigumu sana kumwelewesha mwananchi wa kawaida kwamba uchumi wetu umekua na akakuelewa japo pengine yeye mwenyewe mwananchi amechangia kwa njia moja ama nyingine katika ukuaji wa

uchumi huo. Hata hivyo, Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kuwashirikisha wananchi katika kukuza uchumi na kufaidi matunda yake. Miongoni mwa jitihada hizo ni:-

- Kuanzia Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA) programu hii ilizinduliwa Oktoba 2004 ikiwa na lengo la kurasimisha biashara na rasilimali mfu ili ziweze kutumika kisheria katika mfumo rasmi kama dhamana ya kujipatia mkopo kutoka katika Taasisi za fedha.

- Kudhibiti mfumko wa bei; ughali wa uchumi kwa mwananchi wa kawaida pia unaweza kupimika kwa kutumia kiashiria cha fahirisi ya bei za walaji *(Consumer Price Index)*. Hali ya maisha inakuwa ghali zaidi pale ambapo wastani wa bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinapopanda kwa kiwango kikubwa. Hali hii ilikuwepo katika miaka ya 1990 ambapo wastani wa kasi ya upandaji bei ilikuwa kati ya asilimia 13 na 35 kwa mwaka. Kwa kutambua adha waliyokuwa wanapata wananchi, Serikali ilichukua na itaendelea kuchukua hatua za makusudi za kudhibiti matumizi ya Serikali na ujazi wa fedha. Zaidi ya hayo, Serikali kupitia *TRA* ilipanua wigo wa mapato na kuongeza makusanyo. Aidha Benki Kuu ya Tanzania, nayo ilitekeleza sera za fedha zinazozingatia hoja ya uchumi tulivu. Kufuatia jitihada hizo wastani wa kasi ya upandaji bei ulipungua kutoka 35.5% mwaka 1994 hadi 7.8 mwaka 1999 na kuwa chini ya asilimia 5 kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita. Jambo la kujivunia kuhusu usimamizi wa uchumi wetu ni kuwa pamoja na kuwa na mfumuko wa bei, mfumko huo hauzidi asilimia tano na uko tulivu (*stable*). Jawabu la kudumu la kupunguza ughali wa uchumi linajumuisha yafuatayo:-

  (i) Ongezeko la haraka katika uzalishaji wa bidhaa na utoaji wa huduma mbalimbali ndani na nje ya nchi; (*Makofi*)

  (ii) Ongezeko la haraka katika tija ufanisi na kufanya kazi kwa bidii na maarifa;

  (iii) Uendeshaji kwa ufanisi zaidi shughuli za usambazaji; na
  (iv) Kuendelea kuondoa vikwazo kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara na kupunguza gharama za kufanya biashara nchini. (*Makofi*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ikiwa itathibitika kwamba Serikali iliahidi kufanyia utafiti suala la ughali wa uchumi, je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kujiuzulu kwa kauli yake? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ukipenda unaweza kulijibu.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kumbukumbu zetu zinaonyesha kwamba hatukuahidi namna hii. Basi kama atatuletea uthibitisho basi tutajadiliana. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 87

**Uimarishaji wa Ofisi za Idara ya Kazi**

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Ofisi za Idara ya Kazi zina ukosefu wa vitendea kazi na majengo yaliyochakaa na pia hakuna miundombinu ya kutosha:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kulitatua hilo?

(b) Je, Serikali ina mipango gani ya kuwaendeleza watumishi wa Wizara husika ili wamudu changamoto za leo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Wizara yangu ipo katika marekebisho makubwa ya Sheria za Kazi ambazo zimepitwa na wakati na zimekuwa ni kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya uwekezaji hapa nchini.

Mnamo mwaka 1996, Serikali kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria *(Law Reform Commission)* chini ya Jaji Anthony Bahati wa Mahakama Kuu ilipitia Sheria zote ambazo ni kikwazo kwa uwekezaji. Aidha, Sheria za Kazi zilionekana ni kikwazo kikubwa kwa ushindani na uwekezaji hapa nchini. Hivyo mwaka 2001, Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa wakati huo, ilimteua Jaji John Mrosso wa Mahakama Kuu pamoja na Kamati yake iliyoshikirisha Chama cha Waajiri *(ATE),* Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi *(TUCTA),* Serikali pamoja na Wadau wengine ili kupitia, kuchambua na kuzitayarisha upya Sheria za Kazi. Kazi hii bado inaendelea kukamilishwa kwa msaada wa Serikali ya Denmark kupitia Shirika lake la Maendeleo *DANIDA*.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi ,sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kupitia mradi huu wa Kurekebisha Sheria Mpya za Kazi, ofisi zote za Idara ya Kazi kuanzia Makao Makuu, zitafanyiwa ukarabati mkubwa na kuimarishwa kwa kuzipatia vitendea kazi kama vile samani, kompyuta, simu, fax na kuunganishwa na mtandao wa *internet.* Katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi huu Taasisi za Kazi ambazo

zimeanzishwa kwa Sheria Na. 7 ya 2004 zitapata vitendea kazi vitakavyorahisisha utendaji wa kazi na kuleta ufanisi, mahala pa kazi.

Taasisi hizo ni pamoja na Tume ya Utatuzi na Usuluhishi wa Migogoro *(CMA),* Mahakama ya Kazi *(Labour Court)* na Baraza la Kazi na Uchumi na Masuala ya Jamii (*LESCO*).

Mheshimiwa Spika, sambamba na Urekebishaji wa Sheria Mpya za Kazi, suala la kuwaendeleza watumishi watakaosimamia Sheria hizo, limepewa kipaumbele katika mradi huo. Tayari Maafisa wa Kazi wa Mikoa yote na wale kutoka Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri wapatao 90 wamekwishapata mafunzo ya stashahada ya uzamili. Mafunzo hayo yaliendeshwa na wataalamu kutoka Afrika ya Kusini. Mafunzo hayo yalifanyika katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Kijitonyama, Dar es Salaam. Chuo hiki kimeandaa mtaala kwa ajili ya kuendeleza mafunzo hayo.

Na. 88

**Uundwaji wa Baraza la Vijana**

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katka zoezi la kurejeshwa Sera ya Vijana na Uundwaji wa Baraza la Vijana?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Halima Mdee, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Sera ya Maendeleo ya Vijana ya Taifa ilitolewa mwaka 1996. Kuanzia mwaka 1996 hadi sasa kumekuwa na maendeleo na mabadiliko makubwa katika sayansi na teknolojia, uchumi na mifumo ya siasa na masoko duniani. Mabadiliko hayo yameleta changamoto kubwa sana za kiuchumi, kijamii, kisiasa na utamaduni katika nchi yetu.

Kutokana na changamoto hizi, Serikali iliamua kufanya mapitio ya sera ya Maendeleo ya Vijana ya Taifa ili iendane na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2005. Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini (MKUKUTA), Soko Huria pamoja na Utandawazi *(Globalization).*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima Mdee kama ifuatavyo:-

Nia ya mapitio haya ni kuweka mazingira mazuri ya kulea vijana wazalendo wenye ujuzi na uwezo wa kukabiliana na changamoto za maisha ya kisasa na wenye ari ya kujiendeleza na kushiriki katika maendeleo ya Taifa letu.

Mapitio ya sera hii sasa yamekamilika na rasimu ya kwanza ya Sera hii kwa lugha za Kiswahili na Kiingereza ziko tayari kujadiliwa katika vikao vya juu vya Serikali kabla ya kutolewa upya.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kuunda Baraza la Vijana Tanzania (BAVITA) ulianza rasmi kwa kuitisha mkutano wa wawakilishi wa vijana kutoka Mikoa mbalimbali ya nchi yetu, Vyama vya Siasa, Vikundi vya vijana vya uzalishaji, Mashirika yasiyo ya Kiserikali *(NGOs)* na Mashirika ya Dini. Mkutano ulifanyika mwezi Desemba 1998 na kukubaliana juu ya muundo wa Baraza lenyewe na kuteua Kamati ya kutengeneza rasimu ya Katiba ya Baraza hilo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijadili na kukamilisha rasimu ya Katiba hiyo katika kikao kilichofanyika Januari 1999. Baadaye mwezi Mei 1999, mkutano wa wawakilishi wa vijana wawili kutoka kila Mkoa, wawakilishi wa vijana kutoka vyama vya siasa (CCM, *CUF, CHADEMA, NCCR-MAGEUZI, NLD, TADEA, TLP, TTP, UPDP* na *UDP), NGOs,* Vikundi vya uzalishaji mali na Mashirika ya Dini, walikutana Iringa na kupitisha Katiba ya Baraza hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana na Uundaji wa Baraza la Vijana Tanzania (BAVITA), Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana imeanda nyaraka za Baraza la Mawaziri na zimekwishajadiliwa katika ngazi mbalimbali za Kiserikali na hatua inayofuata sasa ni kujadiliwa katika ngazi ya Baraza la Mawaziri.
Aidha, baada ya hatua hiyo, hatua zitakazofuata ni pamoja na kuandaa Muswada wa Sheria ya Baraza la Vijana Tanzania (BAVITA) ambao utawasilishwa katika Bunge hili Tukufu mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Nina maswali mawili ya nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri tunafahamu kwamba uundwaji wa Baraza la Vijana ilikuwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Vijana ambayo iko tayari. Je, ni kwa nini Serikali inapiga danadana uundwaji wa Baraza husika? Hilo ni swali namba moja.

Pili, anasema kwamba mwaka 1998 iliundwa Kamati Maalum kuhusiana na suala hilo. Miaka imepita na wengi waliokuwa kwenye Kamati hiyo wamepita umri wa vijana na vile vile wana majukumu mengine ya Kitaifa. Je, Serikali ina mkakati gani ku-*review* hiyo Kamati ili iweze ku-*suit* umri wa vijana?

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO):** Mheshimiwa Spika, kwanza rasimu ya Baraza la Vijana la Tanzania iko tayari na imeshajadiliwa katika ngazi za juu Serikalini, inangojea kupelekwa kwenye Baraza la Mawaziri. Kwa hiyo, si kweli kwamba Serikali inapiga danadana Baraza hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi ya Kamati ilikuwa ni kupitia na kukamilisha rasimu ya Katiba ya Baraza. Kazi hiyo imekwisha na nawapongeza sana wale ambao walishiriki katika Kamati hiyo, akiwemo Mheshimiwa Dr. Emmanuel J. Nchimbi ambaye sasa ni Naibu Waziri wa Habari na Michezo. Ahsante Mheshimiwa Spika. (*Makofi)*

Na. 89

**Watoto Wazururaji Jijini Dar es Salaam**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR (k.n.y. MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA)** aliuliza:-

Kwa kuwa idadi kubwa ya watoto wazururaji inaongezeka kwa kasi Jijini Dar es Salaam na kuwa tishio katika jamii kadri siku zinavyoongezeka, je, Serikali ina utaratibu gani kuliangalia kwa haraka na kulidhibiti tatizo hilo kabla halijaleta athari kubwa siku zijazo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba idadi kubwa ya watoto wazururaji inaongezeka kwa kasi Jijini Dar es Salaam na vile vile inakuwa ni tishio katika jamii kadri siku zinavyoendelea. Baadhi ya watoto hao inaaminika hujihusisha na maovu mbalimbali yakiwemo uporaji, ubakaji, biashara zingine za ngono na mambo mengine. Hata hivyo, napenda kukiri kwamba utafiti wa kina haujafanyika kujua idadi kamili ya watoto hao tunaowazungumzia ikiwa ni pamoja na wale watoto yatima na wale wanaoishi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na tatizo hilo, Wizara yangu imeanza kufanya utafiti ili kuona ukubwa wa tatizo hili kwa nchi nzima. Aidha, Wizara inatekeleza Sera ya Maendeleo ya Mtoto ambayo inatoa mwelekeo wa kuwalinda watoto wanaoishi katika mazingira magumu wakiwemo wale wanaozurura katika mitaa ya Dar es Salaam. Sera hiyo inaelekeza kudhibiti ongezeko la watoto walio katika mazingira magumu na athari zinazotokana na hali hiyo. Aidha, Sera inatoa dira ya kuweka mazingira mazuri ya kuwahudumia watoto wanaozurura mitaani. Sambamba na jitihada hizi, Wizara yangu inaandaa Sera ya Maendeleo ya Familia ambayo inatoa mwelekeo na imeweka msisitizo mkubwa katika utoaji wa elimu kwa familia, jamii na taasisi mbalimbali juu ya kupambana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, napenda kutoa wito kwa wazazi, familia na jamii yote kwamba tuna wajibu mkubwa wa kuwalea watoto wetu ipasavyo. Aidha, kuhusu watoto yatima, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Ajira

na Maendeleo ya Vijana; Afya na Ustawi wa Jamii; Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Asasi zingine za Kiserikali zitazoshughulikia masuala haya tunaratibu mpango wa utekelezaji kupitia MKUKUTA ili kukabiliana na tatizo hili. *(Makofi)*

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipatia nafasi kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kwa vile Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri kuwa tatizo hili lipo na linaathiri Serikali, kwa nini Serikali isifanye mkakati maalum wa kuviziba vile vyanzo ambavyo vinasababisha watoto wa mitaani na yatima?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya jitihada kubwa kupitia Wizara zote, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ni Wizara ambayo inashughulikia masuala mtambuka. Kwa hivyo, kwa kupitia Wizara ya Elimu kuna mikakati ya kuweza kuhakikisha kwamba vijana wale wanaokosa masomo ya msingi wanapata kuendelea.

Kuna programu ambayo wale ambao hawakuweza kuendelea wanaweza kupata elimu. Wale vijana ambao wamemaliza shule ya msingi ambao bado hawajatimiza miaka 18 wataweza kupata mafunzo kupitia vyuo vya ufundi na stadi za maendeleo. Lakini vile vile kwa kushirikiana na Wizara inayoshughulikia Tawala za Mikoa kuna uboreshaji wa shughuli zote za vijijini na sisi tutatoa mchango wetu kupitia Vyuo vyetu vya Maendeleo ya Jamii kuhakikisha kwamba kunakuwa na maendeleo vijijini na kusababisha kwamba vijana hawatoki tena vijijini kwenda mijini. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa katika swali la msingi Waziri amekiri kabisa kwamba kuna uzembe wa wazazi kutokujali watoto wao ndio maana wingi wa watoto wanaokuwa mitaani wanakuwa ni wengi. Je, Serikali inaaandaa mkakati gani kwa wazazi ambao uwezo wanao na wanawaachia watoto wanakuwa ombaomba?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, suala la wazazi ambao wana uwezo kuwatunza watoto wao lakini hawafanyi hivyo ni suala ambalo kwa kweli Wizara yetu inakemea na tunatoa wito kupitia Bunge hili kwamba ni jukumu la kila mzazi mwenye uwezo kuhakikisha kwamba anamlea mtoto wake. Serikali itasaidia pale ambako kuna watoto yatima kupitia asasi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge hili Tukufu, Wizara inapenda kutoa tamko kwamba zile taasisi zote zisizo za Kiserikali ambalo zinashughulikia masuala ya watoto zitoe taarifa Wizarani kwetu ifikapo mwezi wa nne ili tuweze kujua shughuli gani wanazozifanya kwa watoto tuweze kuzifuatilia na kusaidiana nao. Ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 90

## Tatizo la Maji Nchini

**MHE. GRACE S. KIWELU** aliuliza:-

Kwa kuwa tatizo la maji nchini limekuwa sugu kwa muda mrefu sasa:-

Je, ni nini Sera ya Serikali ya Awamu ya Nne kuhusu maji, hasa ikizingatiwa kuwa tangu sera ya maji ilipotangazwa mwaka 1972 hadi leo hakuna utekelezaji wa maana juu ya yale yaliyoahidiwa katika sera hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu, Mbunge Viti Maalum, naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 1971, Serikali kwa kushirikiana na Wahisani mbalimbali iliwekeza kwa kiwango kikubwa kwenye miradi ya maji mijini na vijijini chini ya Programu ya miaka 20 ya maji kwa wote. Programu hii ililenga kuwapatia maji safi na salama wananchi katika umbali usiozidi mita 400 kutoka makazi yao ifikapo mwaka 1991. Hata hivyo, malengo ya Programu hiyo hayakuweza kufikiwa kutokana na upungufu uliojitokeza ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa ushiriki wa wadau katika usimamizi na uendeshaji wa miradi na uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, upungufu huo ndio ulioilazimu Serikali kuandaa Sera ya Kwanza ya Taifa ya Maji ya mwaka 1991 ambayo ilitoa dira ya namna ya kuwapatia wananchi maji safi na salama. Mikakati ya Sera hiyo ilikuwa ni pamoja na kuhimiza ushirikishwaji wa jamii kupitia Kamati za Maji na Mifuko ya Maji katika uendeshaji wa miradi ya maji. Aidha, utekelezaji wa sera hiyo ulifanyiwa mapitio mwaka 1995 ambayo yalizaa Sera ya Taifa ya Maji ya 2002 ambayo ndiyo inayotumika sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba tangu Sera ya Maji ilipotangazwa hakuna utekelezaji wa maana uliofanyika. Hivyo napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge baadhi ya mafanikio ya utekelezaji wa Sera hiyo hadi mwaka 2002 kama ifuatavyo:-

(i) Ofisi tano za mabonde ya maji ikiwemo (Pangani, Wami/Ruvu, Ziwa Nyasa, Rufiji na Ziwa Victoria) zilikuwa zimeanzishwa ili kusimamia utunzaji na uendelezaji endelevu wa rasilimali za maji nchini.

(ii) Kulikuwa na ongezeko la asilimia ya wakazi wa vijiji wanaopata huduma ya maji safi na salama kutoka asilimia 32 mwaka 1990 hadi asilimia 50 mwaka 2002.

(iii) Kamati za Maji za Vijiji zenye mifuko ya maji 5,384 zilianzishwa na jumla ya shilingi milioni 776,213,314/= zilikuwa kwenye akaunti katika matawi ya benki mbalimbali kwa lengo la kuboresha huduma ya maji vijijini.

(iv) Kulikuwa na ongezeko la asilimia ya wakazi wanaopata huduma ya maji mijini kutoka asilimia 45 mwaka 1990 hadi asilimia 73 mwaka 2002.

(v) Mamlaka za Maji Safi na Majitaka katika miji mikuu 18 ya Mikoa na mamlaka 9 katika miji mikuu ya Wilaya Tanzania Bara zilianzisha zikiwemo chini ya Bodi Huru za Uongozi wa Maji. *(Makofi)*

(vi) Pamoja na mafanikio hayo ili kuongeza kasi ya utekelezaji, Serikali ilifanya mapitio ya Sera ambayo ilizaa Sera ya Taifa ya Maji mwaka 2002 inayotoa mwongozo unaohakikisha kuwa rasilimali za maji nchini zinalindwa, kuhifadhiwa na kutumiwa kwa kuzingatia uwiano wa mahitaji ya sekta mbalimbali ikiwa pamoja na mahitaji ya maji majumbani, viwandani katika uzalishaji wa umeme, umwagiliaji mashambani na utunzaji wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge, Serikali ya Awamu ya Nne kwa sasa inakamilisha programu za uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za maji na programu za uendelezaji na utoa huduma za maji mijini na vijijini. Utekelezaji wa programu hizo utaanza mwezi Julai mwaka huu 2006 na utafanyika kwenye ngazi zote ikiwa pamoja na mabonde ya maji, Mikoa, Wilaya, Miji Mikuu ya Mikoa na Vijijini. *(Makofi)*

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

Kwa kuwa nchi yetu imejaliwa katika baadhi ya maeneo kuwa na vyanzo vya maji vya uhakika, mfano maji yanayotoka katika Mito ama Maziwa, lakini bado vyanzo hivyo havijatumika sawasawa katika kupata maji safi na salama katika maeneo ya vijijini, ukiachilia mbali mradi wa Ziwa Victoria ambao unatoa maji katika Mkoa wa Shinyanga. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha maji safi na salama yanapatikana vijijini katika sehemu ambazo zimezungukwa na Maziwa na Mito mfano Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na Maziwa mengine? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba Wizara ya Maji kwa kufuatana na Sera ya Maji ya mwaka 2002 imeona jambo hili lina umuhimu na kwa hivi sasa imeanzisha mabonde 9 ya maji. Mabonde yakiwemo maziwa makuu, pia hali kadhalika ikiwepo mito mikuu ambapo ndiyo hiyo itasimamia kikamilifu ili kuweza kutumia maji salama na yawe safi katika vijiji, miji na kila sehemu. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Sera ya Maji ni kuwapatia wananchi wote maji safi na salama na kwa kuwa kuna viwanda ambavyo vinamwaga maji machafu kwenye mito ambayo wananchi wanayatumia. Je, Wizara inachukua hatua gani kuweza kushughulikia tatizo hilo ambalo limekuwa sugu kwa maeneo mengi? Ahsante Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Wizara ina sababu kubwa ya kuanzisha programu hii inayoitwa Programu ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira na hii programu itakuwepo nchi nzima na kwa hivi sasa Halmashauri zote za Wilaya zinafahamu hiyo programu na wanatayarisha mapendekezo yao aina mbalimbali. Katika programu hii pia humo humo kutakuwa na mafunzo maalum na ushirikishwaji wa wananchi wote vijijini na kila mahali kuhusu matumizi ya maji na kuhifadhi mazingira na pia kuweka maji yote yanayotumiwa kwa binadamu yawe safi. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika,ahsante. Naomba kuuliza swali dogo la nyongeza kwa sababu Naibu Waziri amekubali kwamba wataanzia kwenye maeneo yenye maji. Haoni ya kwamba ni vizuri kuvitembelea Visiwa vya Ukerewe ambavyo Mungu amevijalia kukaa juu ya maji ili aharakishe kuondoa aibu ya kubeba maji kichwani wakati tumekaa juu ya maji? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nakubali mwaliko na tutakwenda kutembelea Ukerewe ili tuone hali na tuweze kujua jinsi ya kufanya, ahsante. *(Makofi)*

Na. 91

**Mradi wa Uboreshaji Huduma za Maji**

**MHE. JOB Y. NDUGAI (K.n.y. MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilipendekeza na kuchagua miji midogo tisa (9) kati ya kumi na tisa (19) iweze kutekeleza miradi ya uboreshaji wa huduma ya maji katika miji hiyo kwa kutumia vigezo vilivyoainishwa:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kasi ya utekelezaji wa mradi huu inakwamishwa na uteuzi ama uchaguzi wa mkandarasi mmoja tu wa uchimbaji wa visima katika miji yote tisa?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba, upo umuhimu wa kazi kama hizo kugawanywa kwa makandarasi wengine wenye uwezo na vifaa bora ambao Halmashauri imekuwa ikiwatumia kwa shughuli kama hizo?

(c) Je, ni lini mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira kwa mji wa Mpwapwa na Ving'hawe utaanza kutekelezwa na kukamilika ili kuondoa kero na adha ya upungufu/uhaba wa maji katika mji wa

Mpwapwa na Ving'hawe kwani maji ni kichocheo kikubwa cha maendeleo ya wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a), (b) na (c), naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, naomba kuanza kwa kutoa maelezo. Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa kupitia Shirika lake la Kifedha la *AFD*, ilibuni Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira katika miji midogo. Lengo la Programu hiyo ni kutoa huduma endelevu ya maji safi, salama na ya kutosha na pia kutoa elimu ya afya na usafi wa mazingira kwa wakazi wa miji midogo. Uchunguzi wa awali wa Programu hiyo ulihusisha miji 19 katika Mikoa ya Pwani, Morogoro na Dodoma. Miji hiyo ilichujwa kwa kutumia vigezo mbalimbali na kubaki miji 9, ambayo hiyo 9 ikiwemo Utete, Ikwiriri na Kibiti, Turiani na Mvomero, Kilosa na Gairo, Kibaigwa na Mpwapwa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa programu hii upo katika hatua za mwisho za uchunguzi wa kina wa vyanzo vya maji. Hivi sasa, uchimbaji wa visima vya utafiti kwenye maeneo yaliyoainishwa na Mtaalam Mshauri wa Programu unaendelea. Uchimbaji wa visima hivyo unalenga kujua upatikanaji, ubora na uwingi wa maji kutoka kwenye maeneo hayo. Matokeo ya uchunguzi huo yatawezesha kufanyika kwa usanifu wa kina na hatimaye ujenzi wa mifumo ya maji na usafi wa mazingira kufanyika katika miji hiyo 9 kwenye programu imepangwa kukamilika ifikapo mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

(a) Mchakato wa kupata wakandarasi wa uchimbaji wa visima vya utafiti katika miji hiyo 9 ulizingatia kanuni na taratibu za Sheria Na. 21 ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004. Wizara iliandaa zabuni ya uchimbaji wa visima vya utafiti na kuigawa katika makundi 3. Kundi la kwanza lilihusisha miji ya Utete, Ikwiriri na Kibiti. Kundi la pili ilihusisha miji ya Turini na Mvomero na kundi la tatu lilihusisha mijiji ya Gairo, Kibaigwa na Mpwapwa. Zabuni hii ilitangazwa na Bodi ya Zabuni ya Wizara kwa muda wa zaidi ya mwezi mmoja kupitia magazeti mbalimbali hapa nchini. Hadi kufikia tarehe ya mwisho wa kuwasilisha maombi, jumla ya makampuni 4 yalikuwa yamenunua makabrasha ya zabuni. Hata hivyo, kati ya makampuni hayo 4, ni makampuni 2 tu ndiyo yaliyowasilisha maombi ya kazi. Baada ya tathmini kufanyika kwa kuzingatia uwezo wa makampuni hayo, kampuni moja ndiyo iliyoshinda kandarasi ya kuchimba visima kwenye makundi yote matatu niliyoyataja hapo juu niliyoyataja hapo.

Mheshimiwa Spika, kuchelewa kuanza kwa kazi ya uchimbaji wa visima kama Mheshimiwa Mbunge alivyouliza katika miji midogo iliyopo katika kundi hayo matatu na kundi la tatu ikiwa Gairo,Kibaigwa na Mpwapwa, ambapo ndiyo kwake kulisababishwa na mkandarasi kushindwa kuwasilisha Wizarani hati ya udhamini wa kibenki *(Bank Guarantee)* ya kumwezesha kulipwa malipo ya awali ili aanze kazi. Hata hivyo, Wizara kwa kushirikiana na Mhisani wa Programu hiyo *(AFD)* imefanya jitihada za kutatua tatizo hilo na tarehe 24 Januari 2006 mkandarasi alipata fedha, ambazo pamoja na mambo mengine zimemwezesha kufanya maandalizi ili kazi ya uchimbaji kwenye mji wa Mpwapwa ianze tarehe 30 Januari 2006.

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri wa Maji alitembelea mradi huu na alimkuta mkandarasi tayari ameanza kazi na sasa hivi anashughulika na usanifu. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mtindo wa kugawanya kazi ili ifanywe na makandarasi zaidi ya mmoja wenye uwezo na vifaa bora unaharakisha utekelezaji na ukamilishaji wa kazi kwa wakati uliopangwa. Ni kwa kuzingatia mbinu hii, Wizara iligawanya kazi ya uchimbaji wa visima katika makundi matatu kwa matarajio kwamba kundi lingepata mkandarasi mmoja kazi ingeharakishwa zaidi. Aidha, Wizara iliwajibika kwa kutangaza katika magazeti ili makampuni mbalimbali ikiwemo na makampuni ya ukandarasi ya Mpwapwa ili na wenyewe waweze kuomba. Hata hivyo hakuna wakandarasi wa Mpwapwa waliomba. Sisi Wizara tungefurahi sana kuomba kwamba kila Halmashauri ya Wilaya inayohusika inahamasisha makampuni ya makandarasi wenye uwezo kutoka kwenye Wilaya zao wanaowafahamu ili waweze kufanya kazi hizo.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua adha ya maji inayowapata wakazi wa mji wa Mpwapwa na vitongoji vyake, ikiwa ni pamoja na kitongoji cha Ving'hawe. Aidha, Wizara inatambua kwamba maji ni kichocheo muhimu cha maendeleo ya wananchi. Kwa hali hiyo, Mji wa Mpwapwa utakapopata maji pia na Kitongoji cha Ving'hawe ni kimojawapo ambacho kimo kwenye programu hiyo na wakifanikiwa kupata hiyo na mji huo wa Ving'hawe utapata maji.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Wizara ina miradi mikubwa miwili ya maji na usafi wa mazingiza, mradi wa kwanza ukiwa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini na upo huu wa Maji na Usafi wa Mazingira kwenye miji midogo ikiwemo miji ya Gairo, Mji Mdogo wa Kibaigwa na Mji wa Mpwapwa. Uzoefu umeonyesha pamekuwa na ucheleweshaji mkubwa sana wa utekelezaji wa mradi huu kutokana na makandarasi na makonsaltansi wote waliochaguliwa kuwa wanatoka Dar es Salaam mbali toka kwenye utekelezaji wa mradi husika upo. Lakini je, leo makampuni hayo yamechukua miradi

mingi na kwa hiyo yanakosa kuweka ile *Bank Guarantee* ili waweze kutekeleza miradi hii. Je, Wizara inasema nini kuhusu ucheleweshaji huu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kabisa kwamba kweli mkandarasi akiwa ni mmoja anachelewesha hizi kazi. Mimi mwenyewe nikiwa kama Naibu Waziri nimetembelea miradi ya kwa Mheshimiwa Ndugai ambako kuna miradi 11 ya maji na yenyewe ilikuwa na tatizo hilo hilo. Tulikaa kikao pamoja na Halmashauri ya Wilaya na tukajadili jambo hilo na tatizo likaonekana ni kuhusu Wakandarasi na sisi tukawaambia kwamba ni jukumu lao wenyewe kuwahamasisha wakandarasi wengi iwezekanavyo ili waweze kufanya kazi hizo. (*Makofi*)

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa Waziri ili aweze kuwapatia wananchi wa Tarime maelezo ni kwa nini ahadi ya Rais wa Awamu ya Tatu mwaka 1995 ambapo aliwaahidi wananchi wa Tarime kwamba atawapa maji haikutekelezwa wakati miji mingine 9 na 19 ilikuwa inapangiwa hiyo miradi. Sijui mnasemaje kuhusu hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, swali hili lina sura ya swali jipya lakini kama uko tayari kujibu kuhusu Tarime ...

Ni swali jipya nadhani tuliache, ahsante. *(Makofi)*

Na. 92

**Upungufu wa Vitendea Kazi - Vituo vya Uhamiaji - Zanzibar**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa Vituo vya Uhamiaji Zanzibar ni vizuri na ni vya kisasa lakini vina upungufu wa vitendea kazi kama magari, Pikipiki na Kompyuta kama ilivyo kwa kituo cha Kivunge Mkoa wa Kaskazini Unguja:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukipatia kituo hicho gari?

(b) Kama mpango huo upo, je ni lini utatekelezwa hasa katika kipindi hiki ambacho hawana gari?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Mkwajuni, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inao mpango wa kuzipatia kwa awamu Ofisi zote za Uhamiaji nchini kikiwemo kituo cha Kivunge, vitendea kazi muhimu hasa magari, pikipiki, vifaa vya mawasiliano na kompyuta. Lengo ni kuwawezesha Maafisa wa Uhamiaji wa Mikoa, Wilaya na vituo vingine kote nchini, kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tanzania Zanzibar, Wizara yangu imejitahidi kupata gari moja kwa kila Mkoa. Kituo cha Kivunge ambayo ndio ofisi ya Mkoa wa Kaskazini Unguja, kina gari moja aina ya *Toyota Prado Na. SMZ 5122*, pikipiki moja na kompyuta moja.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wa karibu kuhusu Idara ya Uhamiaji kupatiwa vitendea kazi Zanzibar. *(Makofi)*

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Hata hivyo Mheshimiwa Naibu Waziri gari alilolitamka lililopo pale kwa kweli ni bovu na haliwezi kufanya kazi kama inavyohijika kufanya kazi katika Mkoa wetu na yeye anajua kuwa lile gari halifanyi kazi, ni bovu. Pili, matatizo mengi ambayo nimeyataja yatapatiwa ufumbuzi tu kipindi kifupi ambacho kakitaja Mheshimiwa Naibu Waziri lakini kuna uchache wa watumishi na nyumba za watumishi pale, je, tatizo hili atalishughulikiaje?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nilikwenda Kivunge mwezi uliopita nimeona, ni kweli kuna gari bovu ndio maana Wizara yangu inakusudia kupeleka gari moja jipya katika mwaka wa fedha unaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikagua pia nyumba za wafanyakazi ni kweli ni nyumba chakavu na Wizara yangu inakusudia kutenga fedha kwa awamu ili kusudi kujenga nyumba za wafanyakazi wa Idara ya Uhamiaji. *(Makofi)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri yeye na Mheshimiwa Waziri siku tatu tu baada ya kuapishwa kuchukua dhamana hii walihudhuria ufunguzi wa jengo zuri la kisasa katika Jimbo langu la Koani kwa ajili ya Mkoa wa Kusini Unguja ambalo limekamilika ambalo linapendeza na ninawapongeza sana. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba wafanyakazi wengi wa Idara ya Uhamiaji Zanzibar hawajapelekwa masomoni ili angalau nao watie nuru macho yao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hilo ni swali jipya kabisa kwa sababu linahusu mafunzo na swali lilikuwa linahusu gari.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, Serikali inaweza kutamka imetenga kiasi gani kwa ajili ya kununu vifaa vya uhamiaji nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga fedha za kutosha kwa ajili ya kununua magari 30, pikipiki 30 na boti mbili za doria. *(Makofi)*

Na. 93

**Hospitali ya Haydom Kufanywa ya Rufaa**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa Hospitali ya Haydom ni Hospitali kubwa ya KKKT Dayosisi ya Mbulu inayohudumia wagonjwa toka Wilaya za Mbulu, Hanang, Iramba, Karatu, Singida, Shinyanga na kadhalika inavyo vifaa vya kisasa, waganga wa ndani na nje, inapata msaada mkubwa sana toka Serikali ya Norway kupitia Ubalozi wake hapa nchini, pia mashirika mengine makubwa ya nje na Serikali yetu imekuwa inatoa mchango mkubwa kupitia *Basket Fund;* na kwa kuwa, kama hospitali hiyo itasajiliwa kuwa hospitali ya Rufaa kwa mkataba na Hospitali ya *KCMC* kutoa Madaktari Bingwa wake wenyewe; na kwa kuwa, tayari Uongozi wa KKKT Dayosisi ya Mbulu kupitia Hospitali ya Haydom ilishaleta ombi Serikali, kuomba iwe Hospitali ya Rufaa:-

(a) Je, ni lini Serikali itatoa kibali kwa Hospitali hiyo iwe ya Rufaa kwa faida ya wananchi wa Mikoa ya Manyara, Singida, Shinyanga, Dodoma na kadhalika ambao wanakaa mbali na Hospitali za Rufaa za Bugando, *KCMC* na Muhimbili?

(b) Kwa kuwa, hospitali ya Haydom ilishaingia mikataba na hospitali ya *KCMC* kuwapatia Madaktari Bingwa; je, Serikali haioni kwamba, ni jukumu lake sasa kuharakisha kibali hicho mapema?

(c) Kwa kuwa Ubalozi wa Norway upo tayari kuongeza misaada ya fedha kwa ajili ya kutoa elimu kwa Madaktari Bingwa, Waganga wa fani mbalimbali na pia misaada mingine; Je, huu si wakati muafaka kwa Serikali yetu ambayo ina mahusiano mazuri na Serikali ya Norway kupata misaada hiyo kupitia Hospitali ya Haydom?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu maswali yaliyoulizwa na Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Singida Mashariki, naomba kutoa maelezo mafupi kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuna ushirikiano mkubwa kati ya Serikali na Uongozi wa Hospitali ya Haydom inayomilikiwa na KKKT Dayosisi ya Mbulu. Jumla ya fedha zilizotolewa na Serikali kwa Hospitali ya Haydom mwaka 2004/2005 ni Shs.275,324,086/25 kama ruzuku ya vitanda *(bed grants),* kutoka mfuko wa pamoja

*(basket fund)* na mishahara ya watumishi. Fedha hizi zinatolewa na Serikali ili wananchi wanaotumia huduma za hospitali hiyo na waweze kuzipata kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu a, b na c, kama ifuatavyo:-

(a) Ili hospitali iwe ya rufaa, kuna vigezo vilivyowekwa ambavyoinatakiwa kutimiza kabla ya kupewa hadhi hiyo. Vigezo hivyo ni pamoja na idadi ya Madaktari na Wataalamu Bingwa katika maeneo mbalimbali ya kutolea huduma *(departments),* vifaa na majengo. Rasilimali hizi ni zile ambazozipo kila wakati katika hospitali. Baada ya kupokea ombi la Uongozi wa Hospitali ya Haydom ambayo kwa sasa ni Hospitali ya Rufaa ngazi ya kwanza, Wizara yangu iliutaka uongozi ueleze idadi ya wataalamu iliyonao na kulinganisha na mwongozo uliopo (nakala walipelekewa). Uongozi pia ulitakiwa kuwasilisha ramani ya Hospitali. Baada ya kudhihirisha kuwa rasilimali za hospitali hiyo hasa wataalamu, hazikidhi matakwa ya mwongozo, Uongozi wa Hospitali hiyo ulibadili mawazo na kuomba Haydom itambuliwe kama Hospitali ya Rufaa Ngazi ya Pili *(Second Level)* sawa na Hospitali ya Mkoa. Hata hivyo, ilidhihirisha kuwa bado wataalamu waliopo *(full time technical staff, doctors and specialists)* hawatoshi kuifananisha na Hospitali ya Mkoa. Hospitali ina Daktari Bingwa mmoja (1) tu kati ya walau wanne (4) wanaohitajika kuwepo. Haina Daktari wa Kawaida *(Medical officer)* hata mmoja kati ya saba (7) wanaohitajika. Ina Madaktari Wasaidizi *(Assistant Medical Officer)* saba (7), kati ya 17 wanaohitajika.

(b) Mheshimiwa Spika, katika barua yao ya maombi, Uongozi wa Hospitali ya Haydom ulionyesha kuwa na makubaliano kati yake na Hospitali ya *KCMC* yaliyokuwa bado hayajahitimishwa. Barua hiyo ilionyesha kuwa Madaktari hao hawatahamishiwa katika Hosptiali ya Haydom, bali watakuwa wakifika kutoa huduma na kisha kurudi *KCMC Moshi (Outreach).*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa kuna hospitali kadhaa zinazofaidika na mpango kama huu wa Madaktari Bingwa kutembelea hospitali na kutoa huduma katika tarehe zilizopangwa na kisha kurudi kama *Flying Doctors.* Katika mpangohuu, Hospitali ya Mkoa ya Bukoba pia unafaidika kutoka Hospitali ya Rufaa Ngazi ya Tatu (Level III). Wizara yangu ina mpango wa kuzishawishi hospitali zote za rufaa Ngazi ya Tatu zizidishe huduma hii kwani ni moja ya majukumu yao. Kwa utaratibu huu Wizara inatagemea kujenga uwezo mkubwa zaidi kwa hospitali za ngazi za chini katika kutoa huduma bora. Hivyo, kwa kuzingatia upungufu wa wataalamu uliopo sasa pamoja na kuonyesha kwamba bajeti za kuiendesha ni tegemezi, Wizara inasita kutoa kibali hicho.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara inatoa shukrani kwa misaada inayotolewa na Serikali ya Norway kwa Tanzania kupitia Hospitali ya Haydom. Wananchi wengi wamefaidika na wanaendelea kufaidika nayo. Wizara inaomba kuushauri Uongozi wa Hospitali ya Haydom uendelee kuzungumza na Ubalozi wa Norway ili Hospitali hiyo

isaidiwe kuongeza idadi ya Madaktari Bingwa na vile vile iongezewe misaada ya kuboresha miundombinu na kuongeza vifaa vya kisasa vya tiba.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa juhudi za Serikali zinaelekezwa zaidi Mikoa iliyopo katika Kanda ya Kati na ile ya Kusini ili nayo ipate Hospitali za Rufaa Ngazi ya Tatu *(Level III). (Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa, Ubalozi wa Norway uko tayari kusaidia kutoa Madaktari Bingwa kwa wingi na kwa kuwa Hospitali ya Haydom inatibu Watanzania wa maeneo yote niliyoyataja je, Serikali nayo itachangia kupata Madaktari Bingwa ili hospitali hii iwaokoe watu wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, iwapo kama Ubalozi wa Norway utaweza kutupatia msaada kwa kuwasomesha Madaktari Bingwa na wengineo, nina hakika Serikali nayo itaongezea ili kuweza kui-*support* hiyo Hospitali ya Haydom iweze kupata hiyo hadhi. *(Makofi)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa katika jibu la msingi alisema Serikali inasisitiza suala zima la *Outreach Program Flying Doctor Service* nchi nzima, je, Serikali au Wizara itaona umuhimu sasa hivi kitengo au idara au Hospitali ya *MOI (Muhimbili Orthopedic Institute)* iwe inafanya *Outreach Program* katika Hospitali ya Tumbi Kibaha ambayo inapokea karibu asilimia 30 ya *accident* ya nchi nzima?

**SPIKA:** Naona ni swali jipya. Maswali yamekwisha. Kuna matangazo Waheshimiwa Wabunge.

Kwanza, haitawezekana kwa sasa hivi mara baada ya maswali kuingia katika zoezi la uchaguzi kama ilivyopangwa kwenye *Order Paper* kwa sababu za kiufundi. Karatasi za kura zilikuwa hazijakamilika, mtaona chaguzi zinahusu nafasi nyingi sana. Kwa hiyo, karatasi bado zinashughulikiwa. Kwa hiyo, baada ya matangazo haya, nitamwita tu mtoa hoja.

La pili, wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, wanaombwa wakutane saa saba mchana, chumba Na.231.

Tatu, wanachama wa Bunge wa Chama cha *Population and Development* wanaombwa wakutane ndani ya Ukumbi huu wa Bunge saa saba mchana. Mwenyekiti ameomba kwamba hata wale Waheshimiwa Wabunge si wanachama wanakaribishwa ili wajifunze na kuelewa masula haya ya Idadi ya Watu na Maendeleo *(Population and Developmet)* na pengine kwa kusikiliza wenzao wanaweza wakajiunga katika chama hiki muhimu.

Nne, Kamati ya uongozi ikutane saa 7.30 mchana kuzingatia zile kazi tulizokabidhiana.

Tano, leo kutakuwa na tafrija ya shukrani *Dodoma Hotel* kwa Waheshimiwa Wabunge waliopita katika chaguzi za juzi. Wale waalikwa wote wanakumbushwa kwamba ni *Dodom Hotel* mara baada ya kuahirishwa Bunge hapo saa 1.45.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada Wa Sheria ya Kusimamia Maeneo Maalum ya Uwekezaji Rasilimali *(The Special Economic Zones Bill, 2006)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi nianze kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kunichagua kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Nami naomba niahidi kwamba kwa heshima na kwa kushirikiana na Waziri wangu na wafanyakazi wote wa Wizara, tutafanya kazi kwa uaminifu mkubwa kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikupongeze wewe na Mheshimiwa Naibu Spika kwa namna ambavyo mlichaguliwa kwa kura nyingi sana na Bunge hili. Pia nimpongeze Waziri Mkuu kwa kupata kura nyingi katika Jimbo lake lakini pia kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na kupitishwa kwa kura nyingi na Bunge hili. Mwisho niwashukuru sana akina mama wa Kilimanjaro kwa namna ambavyo walivyonipitisha kwa kura nyingi na kunirudisha katika Bunge hili. Ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Naomba nianze na hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Fedha pamoja na hoja ya Mheshimiwa Esther Nyawazwa ambao walipendekeza kuongeza idadi ya wajumbe katika mamlaka kutoka nafasi mbili kuwa nafasi nne. Hoja hii tumeikubali na imeshatoka katika *Schedules of Amendment. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inayofuata ni kutoa kipaumbele cha ajira kupewa Watanzania. Hoja hii ilitolewa na Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda; Msemaji Mkuu wa Upinzani pamoja na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi.

Mheshimiwa Spika, Muswada unapendekeza wawekezaji kuleta wataalamu kutoka nje wasiozidi watano na zaidi ya hapo itazingatia ukosefu wa wataalam wa Kitanzania kwenye *cadre* husika. Hata hivyo, katika utekelezaji Serikali itazingatia maoni ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa inahusu mitambo ambayo tayari imo nchini itambulike kama sehemu ya mitaji ya uwekezaji ndani ya *SEZ*. Hoja hii ilitolewa na Msemaji Mkuu wa Upinzani. Sisi tunasema maudhui ya Muswada huu ni kuleta

uwekezaji mpya ambao utaongeza tija, teknolojia mpya, ajira na mauzo nje, yaani utaleta *impact* katika uchumi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni *Tanzania Investment Centre* na *EPZ* kuwa Idara za *SEZ.* Hoja hii ilitolewa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani. *TIC* ilianzishwa kwa Sheria Na.26 ya mwaka 1997 na *EPZ* ilianzishwa kwa Sheria Na.11 ya mwaka 2002. Sisi tunaona ni muhimu kuendelea kuheshimu sheria hizi mbili tofauti.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kuboresha elimu inayotolewa. Hoja hii ilitolewa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani na sisi tunasema kwamba mpango wa MMEM na MMES unalenga kufikia malengo haya na Serikali itazingatia ushauri huu na aidha Serikali vile vile imedhamiria kuanzisha Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja kwamba kila kiwanda kiwe ni sehemu ya *SEZ*. Hoja hii ilitolewa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani na sisi tunasema kwamba *SEZ* ni *Custom Controlled Area* yaani eneo linalodhibitiwa na Ushuru wa Forodha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatambua matatizo yanayoathiri sekta ya kilimo na yatatatuliwa kwa sera na mikakati mingine. Mazao mapya yataanzishwa chini ya *Tanzania Mini-tiger Plan* ya *2020.*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kwamba hoja hazifanyiwi kazi zinawekwa tu kwenye ma-*shelf* na mfano uliotolewa ni *AGOA*. Hoja hii iliietwa na Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah. Tunasema kwamba kwa kuanzisha *SEZ* tunaweza kufaidika na fursa za soko la *AGOA* na *EBA* na waliowahi kufaidika na sera hizi ni Kiwanda cha *Sun Flag*. Kwa hiyo, tuna mfano hai kabisa Kiwanda cha *Sun Flag Arusha*. *SEZ* itaongeza fursa za kufaidika na biashara ya ndani na biashara ya nje.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine miundombinu ya *SEZ* ijengwe na sekta binafsi. Hoja hii vile vile ilitolewa na Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah. Tunasema Muswada wa *SEZ* unatambua majukumu ya Serikali na sekta binafsi kwenye ujenzi wa miundombinu ya *SEZ*.

Mheshimiwa Spika, malighafi za *SEZ* zitoke nchini badala ya kuagizwa nje. Hoja hii vile vile imetolewa na Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah. Tunasema kwamba siyo busara kuliwekea sheria jambo hili lakini malighafi kwa kadri itakavyowezekana na kama itakuwa imekidhi viwango hitajika yanaweza yakatoka humu humu nchini.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa vile vile na hoja ya kujenga miundombinu kwa kutumia fursa za Mkoa wa Kigoma. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi.

Mheshimiwa Spika, tunakubaliana sana na fursa za kiuchumi zilizo katika Mkoa wa Kigoma na tunakubali kwamba jawabu ni kuboresha miundombinu ya barabara, bandari, uwanja wa ndege na umeme wa gridi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja vile vile inasema tunaiga mno kutoka nje kwa nini tusibuni sisi mipango yetu ya *SEZ.*Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa John Cheyo. Tunajifunza kutoka nchi nyingine lakini tunatambua mahitaji nchini mwetu, mazingira yaliyopo nchini na changamoto zinazotukabili za kuongeza ajira, kuongeza mauzo nje, kukuza uchumi haraka na kupiga vita umaskini.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kuinua utalii wa *Western Serengeti.* Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa John Cheyo. Chini ya *Tanzania Mini-tiger Plan ya 2020,* utalii utaendelezwa vile vile katika *SEZ* maalum.

Mheshimiwa Spika, hoja inayofuata ni misamaha ya kodi kwa viwanda vya samaki. Hoja hii vile vile ilitolewa na Mheshimiwa John Cheyo. Tunasema kwamba viwanda vya samaki tayari vinapata misamaha ya kodi hususan viwanda vya samaki vinavyouza nje.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni hoja ya mazao mbalimbali ya kilimo kuwa *SEZ.* Hoja hii vile vile imetolewa na Mheshimiwa John Cheyo. Mashamba yote ya mauzo mbalimbali hayawezi kuwa *SEZ* kwa vile *SEZ* ni *Custom Controlled Areas*, Eneo Lililo chini ya Udhibiti wa Forodha. Kwa hiyo, kwa hakika hatutaweza ku-*bond* mashamba yote.

Mheshimiwa Spika, vile vile kulikuwa na suala la ajira na hili nalo limetolewa na Mheshimiwa John Cheyo. Ajira 20,000 ambazo zitatolewa na *SEZ* ambayo imeanza Mabibo Dar es Salaam zitaweza kuchochea ajira nyingine zaidi na kupata kipato yaani *down stream benefits*.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kuwa vivutio vitapunguza mapato ya Serikali. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Esther Nyawazwa na sisi tunasema kwamba tuangalie faida kwa upana wake na sio kodi peke yake. Aidha, usipotoa vivutio hupati wawekezaji vile vile hautapata ajira na hutaweza kuongeza fursa za kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kutokagua mizigo yaani *pre-shipment inspection* na uwezekano wa kuingiza bidhaa haramu kwa mfano silaha. Hoja hii vile vile ilitolewa na Mheshimiwa Esther Nyawazwa. Ukaguzi wa mizigo kwenye *SEZ* utafanyika kwenye *SEZ* chini ya *Custom Officers* yaani itafanyika katika maeneo ya *SEZ rather than* kufanyiwa *pre-shipment inspection.* Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji iliandaa Muswada huu ikishirikisha wadau wote yaani Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, Wizara ya Ardhi, TAMISEMI, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, Benki Kuu ya Tanzania, *TIC, TRA, NDC, TBS,* Uhamiaji nakadhalika, kwa hiyo haya yote yalizingatiwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya ucheleweshwaji wa leseni za biashara. Hoja hii ilitolewa na Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Dr. Abadallah Kigoda na tunasema kwamba chini ya utaratibu *Best* na *reforms* nyingine, suala hili linafanyiwa kazi

chini ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba ili kuboresha utoaji wa leseni, *Business Licensing Act* ili kukidhi mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya kuharakisha utekelezaji wa *Tanzania Mini-tiger Plan ya 2020* na kujenga *SEZ* nje ya Dar es Salaam. Hoja hii ilitolewa na Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda. Tunasema kwamba Serikali inakubali ushauri wa kuharakisha utekelezaji wa *Tanzania Minitiger Plan ya 2020* na itazingatia na itaandaa *Master Plan* ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, vile vile kulikuwa na hoja ya bei nzuri kwa wakulima. Hoja hii ilitolewa na Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda. Chini ya *Tanzania Mini-tiger Plan ya 2020,* mkakati ni kuboresha mazao asilia ili kupata bei nzuri zaidi katika masoko ya nje na hivyo kuwanufaisha wakulima.

Mheshimiwa Spika, vile vile hoja kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda ilizungumzia juu ya mazao mapya. Serikali inadhamiria kuhamasisha uzalishaji wa mazao mapya kwa mfano *bamboo shoots, gatropha plants* na mbegu nyingine. Pia Serikali inajitahidi kuwepo kwa *value addition* kwa mazao yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, vile vile kulikuwa na hoja ya misamaha na unafuu wa kodi. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa William Ngeleja na tunasema kwamba sisi tunaona kuwa kwa kuzingatia malengo ya kuleta ajira nchini na kuongeza mauzo nje. Faida ni kubwa kuliko misamaha inayotolewa. Vipindi vya msamaha wa kodi vinatofautiana nchi kwa nchi, kwetu tunadhani miaka 10 inatosha. Zipo nchi zenye vipindi vya miaka 25 na hata miaka 50 kwa mfano *Egypt*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile kulikuwa na hoja juu ya mabadiliko katika umiliki wa miradi yaani kuuza hisa kabla ya muda wa msamaha wa kodi kuisha yaani mtu anaanzisha mradi lakini akiona siku zinakwisha anakimbia. Hisa za miradi zinaweza kuhamishwa lakini unafuu wa msamaha wa kodi hauhamishiki na kipindi hakiongezeki hata kama mmiliki atabadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba Serikali itekeleze fursa za uwekezaji maana zitaongeza uzalishaji, tija, ajira na kadhalika. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa David Mollel. Tunasema kwamba Serikali inakubaliana na ushauri huu mzuri na inaonyesha Mheshimiwa Mbunge ameelewa kabisa dhana ya *SEZ*.

Mheshimiwa David Mollel, ameendelea kutushauri kwamba tusiogope kupoteza tusichokuwa nacho mkononi. Hoja hii inahusiana na misamaha ya kodi tunayokusudia kutoa katika maeneo ya *SEZ*. Serikali imekubaliana na ushauri huu mzuri na unaonyesha uelewa mzuri wa Mheshimiwa Mbunge wa kutoa msamaha na unafuu wa kodi na kuanzisha shughuli za uchumi ambazo hazikuwepo. Mpango huu utatoa ajira ambazo hazikuwepo, tutapata *multiple effect* na tutaongeza mauzo nje. Waajiriwa vile vile watakuwa wanalipa kodi ya *VAT* na kodi nyinginezo ambazo zitaongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo unafahamu tunagawana majukumu mimi naomba niishie hapa, bosi wangu Mheshimiwa Waziri atakuja kumalizia hoja hizi, ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuhitimisha hoja yangu niliyoiwasilisha Bungeni.

Pili, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa maandishi na kwa kusema hapa Bungeni pamoja na wale ambao hawakuchangia kwa sababu nao waliunga mkono kwa makofi au kwa kicheko. Kwa hiyo nyote nawashukuruni sana. *(Makofi)*

Michango ya Waheshimiwa Wabunge mingine itasaidia katika utekelezaji wa utaratibu huu wa *SEZ* na mingine itatusaidia wakati tukipanga mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2006/2007. Kwa hiyo, kama hatukuyajibu hapa si kwamba tumeyapuuza, tumeyazingatia isipokuwa kutokana na muda hatuwezi kuyajibu yote.

Tatu, ningependa sasa niwatambue rasmi Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia hapa Bungeni na wale ambao wametoa Michango yao kwa Maandishi kama michango yao.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla kulikuwa na wachangiaji 28, 24 wamechangia kwa kusema Bungeni na 4 wamechangia kwa maandishi. Kama ilivyo ada hapa Bungeni ningependa niwataje Waheshimiwa hawa ambao wamechangia hoja hii, kwanza kwa kusema Bungeni nao ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Kilontsi Muhama Mporogomyi, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa William M. Ngeleja, Mheshimiwa Elisa D. Mollel, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Rishard Said Nyaulawa, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Sameer I. Lotto, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, Mheshimiwa Felister A. Bura, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mheshimiwa Adam K. Malima, Mheshimiwa Vedastusi Mathayo Manyinyi na Mheshimiwa Salome J. Mbatia, Naibu Waziri ambaye namshukuru kwa kipekee kwa kunisaidia kutoa maelezo kwa baadhi ya hoja. Lakini vilevile kwa kunisaidia katika kuendesha shughuli zetu za Wizara. Namshukuru sana. *(Makofi)*

Sasa na mimi nijibu kwa haraka baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Labda niseme tu moja kwa jumla nalo ni hili la wigo wa kodi, hili limezungumzwa kweli. Sasa mimi napenda niseme kwamba shabaha ya *SEZ* ni nini?

Jana nililisema hili labda nilirudie tu hapa kwamba shabaha ya *SEZ* ni kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wetu, ili tufanye nini. Ili tufikiri mambo yafuatayo:

Moja, kuongeza wastani wa kipato cha Mtanzania kutoka ilivyo sasa ya dola 286 mpaka dola 1000, wakati nikijibu swali la asubuhi la ughani wa uchumi moja ya jibu lake kubwa ni hili la kuongeza kipato cha Mtanzania. Ndiyo najibu vizuri, hilo la kwanza.

Pili, ni kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yetu kwa sababu mauzo ya nje ya nchi yaani *Foreign Exchange* ni muhimu katika uchumi wa nchi yetu kwa hiyo hii ni shabaha ya pili.

Tatu, ni kupanua nafasi ya ajira mathalani tumesema kama tukitengeneza *SEZ* ya Mheshimiwa Benjamin William Mkapa ile ya Dar es Salaam ikafikia ukamilifu wa utekelezaji itaweza kuajiri *direct employment,* watu 20,000. Sasa watu 20,000 kwa Dar es Salaam katika sehemu moja tu hii ni kitu kikubwa sana lakini hujasema bado ile *multiplier effect* yake kwamba pengine katika shughuli zile peke yake zita-c*reate employment probably for another 50,000 people.* Kwa hiyo, hizi faida hapana kuzipuuza ndiyo za Msingi sana kwa uchumi wa nchi yetu.

Nne, ni kuongeza uwezo wa kukabiliana na umaskini na hii maana yake vilevile unajibu hoja ya moja kwa moja ya wananchi. Sasa kodi ni muhimu sana lakini vilevile na haya mambo tunayoyazungumza ni muhimu vilevile.

Tano, ni kwamba wewe huna kiwanda utaongeza wigo wapi? Utaongeza wigo tu pale kiwanda kipo, sasa wewe huna kiwanda unataka waje wawekezaji wafanye haya mengine waongeze ajira, mauzo, biashara yako na wapunguze umaskini. Mambo haya manne au matano ni makubwa sana. Kiuchumi mimi naridhika kabisa kuyalenga haya tu bila kuyalenga ya kukusanya kodi.

Sita, ukishanza kuwa na uchumi huu utaapata kodi pia maana unapata *Income Tax* na utapata *VAT.* Kwa hiyo, kuna hoja hapa ya kimsingi ya kuitazama kwamba unaweza ukapata kodi *indirect taxes* lakini unaweza ukapata direct taxes. Sasa katika mazingira yetu haya ili uweze kupata haki hiyo *indirect tax* basi andaa vivutio vizuri ambavyo vitawezesha wawekezaji waje Tanzania. Kwa nini mpaka leo tujiulize sisi hapa Tanzania, kwa nini mpaka leo Kenya kwa mfano na Uganda wanatupita katika kuvutia wawekezaji? Kwa hiyo, hili ni muhimu kulijibu hili na tunalijibu sasa kwa kuandaa vivutio hivi bora ili waje kuwekeza.

Saba, ni lile la kusema kwamba kwa nini tusieneze *SEZ* nchi nzima nayo haiwezekani. Mwalimu Julius Nyerere mwaka 1969 alitufundisha tena alikuwa Mwanza siku hiyo ilikuwa ni wakati wa Mkutano Mkuu wa *TANU* kwamba kupanga ni kuchagua na uchague ili usonge mbele. Alitufundisha Mwalimu hii na Mzee Kingunge Ngombale Mwiru siku hiyo alikuwepo pale Mwanza na nina hakika atathibitisha jambo hili. Kwa hiyo, kupanga ni kuchagua ni lazima utachagua tu kwamba sehemu fulani huwa zinazo

kwa sababu gani unataka ziwe ndiyo *growth* pole zako na ili baadaye upate hizo *multiplier spread effect* katika uchumi wa nchi yako.

Kwa hiyo, mimi nawaomba sana kwamba sisi Serikali tuna nia nzuri, nia yetu ni kuibua uchumi huu ukue haraka na *it doesn't matter* unaanza wapi muhimu ni kwamba pale unapoanza pawe chachu ili uende sehemu nyingine. Kwa hiyo, hili ni Msingi wake wa kusema tutaanza wapi na ndiyo maana tunazungumza kwamba itakapofika mwaka 2020 tutakuwa na *SEZ* kati ya 25 mpaka 30. lakini katika miaka hii mitano tutakuwa nazo nne tu kwa nini? Kwa sababu kwanza tumepanga kuchagua kwa sababu hatuna uwezo wa kuzijenga hizi zote kwa mara moja lazima utajenga hatua kwa hatua.

Nane, tunatarajia vilevile kwamba *Private Sector* ndiyo maana tumewaundia mazingira mazuri hapa ya uwekezaji ili na wenyewe wasaidie kuwekeza lakini *Private Sector* hawawezi kuwekeza mahali kama Serikali yenyewe ninyi hamjaonyesha mfano ndiyo ile *Special Economic Zone* ya Benjamini William Mkapa ndiyo tunaisimami sisi wenyewe kama Serikali na tunaitaka iwe mfano wa kuvutia wawekezaji wengine waje ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo, hili jambo lina sura hii ambayo ninaomba Waheshimiwa Wabunge mtuelewe namna hii.

Mheshimiwa Spika, naomba radhi kwamba kumbe sikuwataja waliochangia kwa maandishi ambaio walikuwa ni hawa:-

Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Rita L. Mlaki, Mheshimiwa Yono Stanley Kevela na Mheshimiwa Dr. Mary Michael Nagu. Naomba radhi niliwaruka pale mwanzo wamenikumbusha wenzangu. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Sasa hoja ya Mheshimiwa Richard Nyaulawa ile ya Mkoa ya Kusini, tunaijibu kama tulivyosema kwa ujumla kwamba lazima kuna sehemu tutaanza na kwa kweli tunaanza na Mkoa wa Dar es Salaam, Mtwara, Tanga, Kigoma, Arusha, Mwanza na Morogoro na mwisho wake tutaenea sehemu ambazo zinahitajika kufanya *SEZ.* Hii *SEZ* ni moja tu ya mbinu za mikakati ya Serikali za kuwekeza kuna *EPZ* tutazungumza baadaye atakuja hapa na mwenzangu kuielezea, nayo ina maeneo yake ya kufanya uwekezaji ambayo yenyewe ni muhimu kwa maana ya kwamba inataka ku - *fast truck industrialization process* katika nchi yetu. Kwa hiyo, hizi program zitaji-*compliment* kwa hiyo kama hatukwenda *SEZ* watakwenda wenzetu wa *EPZ* kama hawatakwenda wenzetu hawa basi tutakwenda sisi katika mpango wa MKUKUTA ambao ni wa nchi nzima. Kama hatutakwenda huko basi tutatumia MKURABITA. Kwa hiyo, mipango ni mingi na yote hii ni lazima itaenea nchi nzima.

Uchambuzi yakinifu. Kwa *SEZ* utafanyika uchambuzi yakinifu kwa *level* mbili, kwa *level* ya sisi kama Serikali lakini kwa *level* ya wawekezaji binafsi wale hatutawafanyia sisi. Kwa hiyo, hakuna mtego pale hatutawafanyia.

Suala la vivutio nimeshalijibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Peter J. Serukamba na suala la kujenga miundombinu hili naliafiki tunakubali kabisa kwa vile bila miundombinu huwezi kuvutia wawekezaji na ndiyo maana suala la Kigoma la kuweka miundombinu linapata kipaumbele na Waziri juzi kasema hapa kwamba ameshita Wabunge wa mkoa wa Kigoma ameshazungumza nao na mimi namuunga mkono suala hili tutalishughulikia vizuri na hata katika eneo la kupanga Kigoma tutafanya priority katika suala la kuweka miundombonu maana bila ya kuweka miundombinu hamuwezi kufanya maendeleo ya maana.

Kwa hiyo, hili nalo tutalishughulikia kwa namna ile na sisi tunatambua kwamba Kigoma siyo tu Kigomayenyewe eneo la soko lakini vilevile nchi jirani, maana sisi Tanzania tunasema sisi ni lango kuu yaani gateway hatuwezi kuwa na gateway kama miundombinu hasa ya barabara, simu za mawasiliano na kadhalilka haikuwa imara, huwezi utafanyaje. Kwa hiyo, hili tunalitambua Serikali na tunalishughulikia kwa namna hiyo.

Wizara ya Elimu iboreshwe. Sawa kabisa tunaunga mkono na hatua zinafanywa. Juzi hapa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo alilizungumzia suala hili. Kwa hiyo, Serikali ina mipango mizuri ya kuboresha masuala ya Elimu na Mafunzo.

Mheshimiwa Jenista Mhagama amesema kwamba pawepo na mashauriano na wadau. Ni kweli tulifanya mashauriano makubwa sana na wadau, hatukufanya peke yetu.

Ruvuma kuwepo katika *SEZ,* ndiyo itakuwepo. Tena Ruvuma wana mradi mkubwa zaidi unaoitwa *Mtwara Development Corridor* ambao una miradi mingi lakini mikubwa tunayoiita *Core Projects* ambayo ipo Mtwara, Masasi, Tunduru, Songea na *Mbamba Bay,* kwa nini? Kwa sababu nchi za *Mtwara Development Corridor* ni Tanzania kwa maana ya mikoa sita ile ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Morogoro, Pwani, Iringa, Mbeya na Rukwa, Hiyo ndiyo *Mtwara Development Corridor.* Sasa kwa wenzetu kule ni Msumbiji Kaskazini, Malawi na Zambia, Zambia pia iko katika sehemu ile ya *Mtwara Corridor.* Kwa hiyo, katika kufanya mawasiliano yawe bora katika suala la *Mtwara Development Corridor* ambapo reli inakuwa mradi mkubwa wa kwanza.

Mradi wa pili ambao tumepiga hatua sasa hivi tumemaliza haraka *level* ya *design* ni wa barabara Mtwara, Masasi, Tunduru, Songea mpaka *Mbamba Bay,* na *Mbamba Bay* katika suala la ku-*develop ports* Mtwara itakuwa *developed* kama *deep port* lakini na *Mbamba Bay* itakuwa *developed* kama *port* ambayo itawezesha mabehewa yaingie kwenye *ferry* kubwa sana *huge ferry* itakuwa inaingia mizigo pale kwenda upande wa pili wa Malawi. Suala la maendeleo ya Ruvuma haijapuuzwa kwa maana ya maendeleo ya nchi yetu.

Lakini lipo pia suala lingine la kutengeneza barabara au reli itakayofika Ludewa na Liganga kama sehemu ya ku-*develop Mtwara Development Corridor* ili tuweze kupata:-

Madini ya chuma ambayo yapo Mundindi pale Liganga na yaliyopo Machimbo ya Madini ya Makaa ya Mawe yaliyopo mchuchuma na Kataweka, Mchuchuma upande huu na Kataweka upande wa pili. Mimi nasema hivi kwa sababu ni Waziri wa kwanza wa Viwanda na Biashara nimetembelea maeneo haya mara tatu na siyo mara moja siku zote walikuwa wanakwenda Manaibu Waziri tu lakini mimi kwa mara ya kwanza nimekwenda mwenyewe na ninapafahamu sehemu hizi ninazozizungumza na ninafahamu na mipango ambayo tumeiweka. *(Makofi)*

Lakini vilevile kama sehemu ya kuharakisha uchimbaji wa madini ya chuma tuna mpango wa kutengeneza barabara ya lami kutoka Madaba kwenda Mundindi ili tuweze kuanza kuchimba madini yale ya chuma. Kwa hiyo, mipango ya Kusini imeandaliwa na mimi nina hakika itatekelezwa vizuri.

Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, na Muswada wa *SEZ* umechelewa, nakubaliana na yeye kabisa 100% lakini sasa mahali tumechelewa basi tukubaliane tufanye kazi kwa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya, ili tuweze kufikia shabaha zetu.

Suala la misamaha ya kodi nimelizungumza kwa urefu na sina haja tena ya kulizungumza. Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo nakubaliana naye kabisa kwamba ili kuibua maendeleo katika Wilaya ya Kilindi au Jimbo la Kilindi na sehemu yote ya nchi yetu kama inafanana na eneo lile lazima jibu la kwanza ni kuandaa miundombinu, tukikamilisha hilo lazima tutafika.

Mimi nina hakika kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu suala la kuibua miundombinu tutalishughulikia katika Serikali hii tutaendelea kufuatilia uzoefu wa awamu ya pili na wa awamu ya tatu, wamefanya kazi kubwa sana katika suala la miundombinu tutaliendeleza katika awamu ya nne.

Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, sawasawa tunaafiki kabisa kwamba masuala yale ya utalii ni muhimu na yamo katika *SEZ* lakini lazima ni kama nilivyosema mwanzo tutakwenda kwa awamu maana uwezo wa kufanya yote kwa pamoja haupo.

Mheshimiwa Sameer Ismail Lotto, mwenzangu huyu kutoka Mkoa wa Morogoro Watanzania wangapi wataajiriwa. Pale *SEZ* ya Benjamini William Mkapa, tumesema itakapokamilika itaajiri watu 20,000 lakini kama nilivyosema kutakuwa na *multiply effect.* Kwa hiyo, kutakuwa na *huge change* ya watu wengine ambao watapata *employment indirectly ,* kwa hiyo hili tutalifanya.

Lakini tunasema *SEZ* yake kubwa ni kuongeza ajra kwa hiyo pale tutakapokuwa tunajenga *SEZ* kazi yake ya kwanza ni kuhakikisha kwamba ajira inaongezeka kwa hiyo kila mahali pataongeza ajira. Sasa *SEZ* ziwepo vijijini, sawa kwa sababu kutakuwa na *SEZ* za kilimo kwa hiyo hizo zitafika vijijini kabisa nina hakika tutafanya hivyo.

Wakurugenzi wa *SEZ* angalau wawepo Watanzania. sasa hili sijui kama linaeleweka vizuri kwa sababu Ukurugenzi unategemea na nani anamiliki ile *SEZ* kama

*SEZ* ile ni ya Sekta binafsi ninyi Serikali hamuwezi kusema wekeni akina Ngasongwa humu kwani kwa mwenye kiwanda chake utasemaje hivyo akae Ngasongwa humo wa nini?

Mimi hiki mali yangu, hii kwa kweli huwezi kusema lakini kama ni ya Serikali lazima watakuwa wakina Ngasongwa wamo maana ndiyo Serikali yenyewe tutawaweka wakina Aggrey Mwanri na kadhalika. lakini huwezi kuweka akina Mwanri katika kiwanda cha mtu binafsi haiwezekani, unaweza kuomba kwamba bwana naomba niwekee lakini akisema staki basi unasema mwenyewe kasema hataki ndiyo mambo yamekwisha.

Mikataba ya *SEZ* ililiwe na Bunge. Sina hakika kinachozungumzwa ni nini lakini iko mikataba ambayo inaelezwa Bungeni ile tutaileta lakini kuna mikataba mingine inamaliza Serikali kwa hiyo ile itafanyika kwa namna ambayo tumekuwa tukiifanya siku zote. Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro anasema Sekta Binafsi haikushirikishwa vizuri kwenye ile mamlaka ya *SEZ.* Sasa tumekubaliana hapa na Waheshimiwa wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwamba tuongeze wawili wengine na sasa watakuwa watano maana wanne binafsi na *Chairman* wa *Private Sector Foundation* watakuwa watano kwa hiyo wamo pale.

Lakini nataka kusema hawa si wafanyabiashara hawa, mamlaka si kufanya biashara, ili nikusimamia kiserikali namna ya ku-f*acilitate SEZ* zijengwe ndani ya nchi kwa hiyo wanachotaka pale ni Serikali ndiyo watakaosema Rais anasema toeni maji kwa *SEZ* ile sisi Mawaziri tunatekeleza bila ubishi ndiyo maana yake. Lakini wale tumewashirikisha pale mwanzo ni kuwataka tu na wao watusaidie kutupa maoni wakati wa mijadala kutoka *Private Sector* na hoja hapa siyo wingi wao, hapana.

Mheshimiwa Spika, hoja hapa ni *quality* ya ushauri wao kwa Serikali ili Serikali itekeleze mambo haya kwa ufanisi, kwa tija na kwa maarifa zaidi ndiyo hoja ya Msingi. Kwa hiyo, mimi naomba hili tulielewe hivyo halina maana ya kubagua sekta binafsi katika suala hilo, ina maana kwamba mtendaji mkuu ni Serikali *in fact* Kamati hii tunaiita kwa kingereza *Troubleshooting* ikitokea matatizo wao ndiyo wawe ndiyo wa kwanza ku-*shoot down* matatizo yale ili mambo yawe laini na yaendelee siyo kwamba wanafanya biashara, wale hawafanyi biashara.

Serikali iangalie sana wawekeza wa ndani. Ndiyo hili tunalisimamia kabisa na hata Rais alipokuja juzi kutembelea katika Wizara yangu moja ya jambo aliloniagiza ni kwamba niwe na mikakati ya kukuza *Private Sector* na hasa *Middle Class in Tanzania.* Ndiyo *Middle Class in Tanzania* mimi na Mwanri tuna ka-*theory* tunapishana kidogo lakini katika hili tunaelewana kwamba huwezi kujenga uchumi wa uhakika ndani ya nchi yako kama huna *Middle Class* ambayo ndiyo kiungozi, maana ukisema Sekta Binafsi ndiyo Kiongozi wa Nchi lazima uwe na *Middle Class* ambaye ndiyo *Leader* katika uchumi ule. Kwa hiyo, hiyo tunakubaliana tunafanya hivyo na tutashughulikia kikamilifu.

Kwa hiyo mikakati yote tuliyokuwa nayo ya MKUKUTA, *Small and Medium Enterprises Policy,* Biashara ya Tanzania tulifanya viwanda pale na policies zipo na ninyi Waheshimiwa Wabunge mlipata, MKURABITA, *Best Program* zote hizi ni sera ambazo tunalenga katika kuwawezesha Watanzania wawekezaji wa ndani ili waweze kushiriki katika uchumi wa Taifa lao.

Sera ya Uwezeshaji wenyewe pia shabaha yake ni hiyo hiyo, tutaandaaa semina kuhusu Sera ya Uwezeshaji na Sheria ya uwezeshaji. Nadhani katika kikao cha mwezi Aprili kwa Wabunge wote ili tuelewane tunazungumza nini maana ya uwezeshaji na maana ya kuimarisha uchumi wa Taifa letu ili ukue kwa haraka zaidi maana *8% to 10% GDP Growth* siyo kitu kidogo ni kikubwa sana lazima tujifunge mikanda kwelikweli na hii ndiyo peke yake itatuondoa katika umaskini. Kwa hiyo, tutazungumza zaidi.

Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, malighafi za hapa ndani zitumike. Hili tunalikuali 100% hatuna ubishi katika hili. Isipokuwa tu hatutaki tuliweke kisheria maana kuna malighafi nyingine Tanzania hazipatikani na wewe unataka uzalishaji hasa kwa mauzo ya nje utafanyaje? Niwape mfano mmoja wa *NIDA Textile Mills Limited* pale Dar es Salaam, wale wanatengeneza shule *King Size and Queen Size, huge* hana, unatakiwa uwe na *wide Loom* ili utengeneze zile sasa hutengenezi huna hapa kiwanda kinachotengeneza *wideroom* ili utengeneze zile, sasa hutengenezi huna kiwanda kinachotengeneza *wide Loom grey cloth* sasa utafanyaje? Ni lazima uagize malighafi nje ili uje kufanya hapa *printing* halafu ufanye *stitching* ndiyo mambo yaende. Kwa hiyo, usiweke sheria, utaweka sheria namna hiyo utajikwamisha lakini sisi tunalielewa hilo na tunalishughulikia kikamilifu.

Ajira tunalikubali na wafanyakazi waepuke tabia ya udokozi hili nalikubali 100% na uzoefu wangu wa viwanda kule nimeliona kule ndiyo tatizo. Baadhi ya viwanda hivi tunavyovijenga harakaharaka hivi vinakufa kwa sababu ya udokozi na uzembe. Wanataka mishahara zaidi kabla hata hawajazalisha zaidi, kiwanda kinaanza mwaka mmoja wao miezi minane tu wanataka waongezewe nyongeza ya mishahara. Haiwezekani Ndugu zangu na hiyo kama tusipoangalia itazuia wawekezaji kuja Tanzania, ndiyo. Kwa hiyo, lazima tukubali kulisimamia vizuri sana.

Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe na suala la kuchelewa miaka 40. Hatukuchelewa kwa maana kabisa kwamba hatukufanya lolote, tumefanya maendeleo makubwa hapa, ndiyo, tumefanya maendeleo makubwa sana hapa. Leo tunazungumza uchumi wa Taifa unaongezeka kwa 6.7% haijapata kutokea kha! Kwa hiyo tumepiga hatua lakini hii hatua haituridhishi tunataka tupige hatua zaidi, ndiyo maana yeke. Tunataka tuongeze uchumi wetu kati ya 8% mpaka 10% ili tufikie yale malengo ya maendeleo ya Millenium, kwa hiyo siyo kama tulisimama hapana ndugu yangu tulikuwa tunakwenda mambo mazuri lakini tunataka yaende mazuri zaidi ili tupate mazuri zaidi ndiyo hoja yenyewe.

Lakini vilevile tunataka kusogea sasa *Middle Income Status,* maana sasa sisi tulikuwa ni *Low Income* ninyi mliosoma Mwelekeo wa Sera za Chama cha Mapinduzi za mwaka 2000 - 2010 kama ilivyotafsiriwa katika ilani zile mbili za mwaka 2000 - 2005

tunazungumza kule kwamba uchumi wetu huko nyuma, uchumi wetu tegemezi sasa tumesema kwamba tutajenga uchumi wa kisasa. Sasa huwezi kujenga uchumi wa kisasa bila kuongeza ukuaji wa uchumi wa nchi yako kwa hiyo, hiyo ndiyo tunayofanya sasa tumekazania na tunaomba mtuunge mkono ili tufikie hapo.

*SEZ* anasema zinaweza kuzidisha tofauti za kimaendeleo miongoni mwa Mikoa, Wilaya na kadhalika, hilo nalo si jipya. Katika mpango wa pili wa maendeleo wa mwaka 1968/9 mpaka 1974/5 moja ya mambo tuliyoyazungumza ni kushughulikia *Regional Disparities* iko katika maandishi ukienda kusoma utaikuta hii.

Sasa *Regional Disparities* lazima tunazishughulikia lakini tukijibana sana kushughulikia *Regional Disparities* wakati kuna fursa nzuri zaidi maana mikoa hii haiko *homogeneous* kwa maana ya *opportunities* no! kuna *huge difference* za *opportunities.* Kwa hiyo, lazima uende kwenye *opportunities* zile maana Mbunge mmoja jana alitukumbusha akasema jamani msiringie *potentials* kwa sababu *potentials* hamzili, katuambia Mbunge mmoja jana na mimi namuunga mkono maana yeye ni mchumi na mimi ni mchumi tunaelewana katika jambo hili kwamba *potentials* hapana kujivunia peke yake lazima uziibue *opportunity for investment* halafu ndiyo unazalisha mali. Kwa hiyo, kuna sehemu nyingine zina *potential the same* lakini utaanza kwanza sehemu nyingine ili ufanya *investment* ili baadaye uibue na kule eeh! ndiyo maana yake. Kwa hiyo, kwa hilo naomba tuelewane namna hiyp.

La Mheshimiwa Bura kuhusu fidia. Ndiyo tutalipa na ile ya Dar es Salaam tumelipa tayari karibu milioni 900 kufidia ndiyo! kwa hiyo kufidia tutafidia hatuwezi kuchukua mali za watu bila kufidia, Serikali gani? Hii ya Chama cha Mapinduzi bado nzuri sana hii kwa hiyo tutafidia.

Ukaguzi wa mizigo. Ukaguzi wa mizigo utafanyika isipokuwa tunachokataza ni kufanyika *pre shipment* au *post shipment* kwa maana ya destination *inspection* pale kwenye harbour kwa sababu itachelewesha mambo. Ukitaka kufanya kwa kadri inavyoonesha wawekezaji ufanye mambo yako haraka, sasa ukifanya polepole utachelewesha mambo ukifanya hapa bandarini pale utachelewesha mambo kwa hiyo unafanya wapi?

Unafanya ndani ya *SEZ* yenyewe kwa sababu *SEZ* yenyewe ni Custom Territory unaweka pale ndiyo unakagua palepale kama wewe hapa umeleta kitu siyo chenyewe eeh! Sheria ile inazungumza kwamba hakuna kufanya kazi hizi bila kuzingatia mazingira lah! Mheshimiwa Mwalyosi kwa hiyo hili pia limo.

Hili la Mheshimiwa Mushi la wachimbaji wadogo hili linazungumzika katika Wizara ya Nishati na Madini na pia tunaliunga mkono lakini pia nakuunga mkono katika suala lile la kuwa na kiwanda nafikiri unataka kusema iwe *SEZ* ama *EPZ* na jambo tulishalifanyia uamuzi zamani kwamba Mererani itakuwa moja ya *SEZ* au *EPZ* yetu ya kwanza kwa ajili ya ku-*process* kusafisha *Tanzanite* ambayo katika nchi yetu ipo hapo tu, kwa hiyo itafanyika hiyo haina maneno na mimi nitahakikisha tunalishughulikia. Kwenye

*SEZ* pia tunao mpango wa namna hii kwa hiyo hili tutalishughulikia haliwezekani kudhalaulika.

Hili pia namjibu Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, alilileta hili pia yeye na mimi tunafahamiana kwa muda mwingi Serikalini. Kwa hiyo, hili namjibu kwamba nalo limo katika *SEZ*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Malima kwa tahadhari yake kwamba SEZ zote zinaweza zingine zikatuharibia mambo, ni kweli na ndiyo maana nakubali na sisi tunafanya kwa makini kabisa na kwa uangalifu, ndio maana tunazungumza *sure SEZs* kwa maana ya kwamba zitakuwa ishirini na tano mpaka thelathini. Sio zaidi lakini pili tunaanza na nne ili tufanye vizuri. Tukifanya ovyo itakuwa mbaya na ndio mara ya kwanza ya Benjamin William Mkapa itakuwa *the best* kwa maana ya *infrastructure* yenyewe na kweli safari hii hospitali tunaendelea kujenga na mimi nina hakika itakapokamilika labda kikao cha Juni, ahaa, tunafanyia hapa, tunavyokuwa Dar es Salaam tunaweza baadhi yetu tukawapelekeni pale mkaone mambo tunayofanya, *SEZ* ya kisasa kabisa katika nchi yetu ambayo inaweza kuvutia wawekezaji wengi na hii imeshavutia tayari, kuna wawekezaji saba wametaka kuja pale, tayari saba na tangu tuanze hatuna hata mwaka. Kwa hiyo tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, tuepukane kuiga pasipo kuzingatia mazingira ya nchini kwetu. Kweli kabisa tunaliunga mkono na hakuna mtu anayefanya hivyo. Sisi kama Serikali hatufanyi hivyo kwa sababu tunajua kabisa mazingira yetu tofauti ndio maana tunaandaa Muswada ambao uko *more specific,* kwetu sisi kwa mazingira yetu, kwa hiyo hakuna mtu ataiga hapa *wholesale,* hakuna.

Mheshimiwa Spika, nakubali vile vile ushauri wake kwamba ili uwekeze kwa mfano katika eneo la Kigoma au Dodoma, kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja alizungumzia suala la Dodoma. Ndio lazima uweke haya mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji mapema ili waje. Kwa hiyo, hilo tutalizingatia wakati wote kwa kuhakikisha kwamba mazingira haya ya uwekezaji yanavutia ili waje kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Manyinyi, Mbunge wa Musoma anasema tuandae nguvu kazi. Ndio tunaandaa mpango wa MMES, mpango wa MMES, *VETA* yenyewe, Vyuo Vikuu, Mheshimiwa Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ameambiwa na Rais na nadhani kwamba atatafuta uwezekano wa kujenga Chuo Kikuu kipya. Kwa hiyo, mambo haya hatuyapuuzi tunayafanya yote, sisi leo tunazungumza *SEZ* tu lakini mipango ya Serikali ipo mingi. Mimi nina hakika wakati wa Bajeti kila Waziri hapa atakapotoa bajeti mtaona mambo tunavyoyafanya na kutarajia kuyafanya kwa Serikali nzima. Kwa maana hiyo kuwafikia wananchi wote sio hayo tu wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji wa ndani nimeshalijibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba tena niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao yote ambayo wametusaidia katika

kuboresha Muswada na kama nilivyosema mengine tutayashughulikia wakati wa utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa hoja. (*Makofi*)

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Kusomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Kusimamia Maeneo Maalum ya Uwekezaji Rasilimali *(The Special Economic Zones Bill, 2006)***

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wanakamati kwa kuzingatia kwamba Muswada una ibara au vifungu vingi tu nitakuwa natamka sehemu halafu Katibu atatusaidia kutupitisha katika vile vifungu.

Sehemu ya 1

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Sehemu ya 2

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Sehemu ya 3

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu namba 13, nilikuwa napendekeza yale mabadiliko yaliyopendekezwa kwamba *with* iwe *between his and opinion* iwe katikati ya *together and his* naona itasomeka vizuri zaidi. Yaani iwe *together with his opinion*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shellukindo nakuomba urudie swali lako ili Mwanasheria Mkuu aweze kujibu.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye marekebisho imeandikwa kifungu cha 13 kwamba neno *with* liwe *inserted between his and opinion* lakini nilikuwa naona kwamba itasomeka vizuri zaidi likiwa *inserted between together and his opinion,* yaani neno lisomeke *submit the same to the authority together with his opinion*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo lake linakubalika.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba maelezo ya ziada kuhusu *section* namba 12 zaidi kifungu kidogo cha pili, *where the authority has approved the area under subsection one, the Minister by notice publishedin the gazette declare the same to be the special economic area. Now as economic zone*, maana ya kuomba maelezo hapa ni zaidi kwamba baadhi ya SEZ, ni SEZ za kilimo.

Sasa *SEZ* za kilimo sitaki kuwa mashamba na nachukua mashamba kwa sababu kuna sababu nyingi labda ni umwagiliaji na woga ambao mimi ninao hapa kwa mazoea ya zamani ni rahisi sana tukatengeneza SEZ ambayo inakuwa ndio chanzo cha kuwafanya watu wetu wasiwe na ardhi na zaidi ukizingatia kwamba mambo ya kutoa fidia katika nchi yetu hayazingatii thamani ya ardhi. Watu wanalipwa fidia zaidi kama ni wakulima wanalipwa fidia labda kwa miti iliyojengwa pale au labda kwa nyumba.

Kwa hiyo, nina woga hapa kwamba *section* hii haizungumzii kabisa ni jinsi gani watu ambao watachukuliwa mashamba yao wataweza kupata fidia ya uhakika ili kuhakikisha kwamba wawekezaji wakubwa hawachukui ardhi ya Watanzania, tukabakia kuwa watu ambao hatuna ardhi na ni watazamaji tu.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maelezo kutokana na hoja aliyoileta Mheshimiwa John Cheyo kama ifuatavyo.

Kwanza, hii ibara namba 12(2) inajieleza kikamilifu kwa maana ya kwamba eneo lile likishaamuliwa kwamba liwe *SEZ* basi lazima litangazwe kwenye gazeti la Serikali ili litambulike kisheria. Sasa hivi *SEZ* za kilimo zitakwenda katika maeneo mapya ambayo kwa nini tuwape wawekezaji hata wa ndani ya nchi, kuna wengine watakuwa wa ndani ya nchi, wale watajua maeneo yao. Kwa mfano, alikuwa analima Mungu aepushe mbali, alikuwa analima kahawa anataka alime soya *beans* kama zao jipya, lakini anataka sasa eneo lile liwe la *SEZ,* anagombana na nani mtu ni shamba lake huyu?

Lakini akiwa mgeni atakwenda katika eneo ambalo ni jipya na maeneo yapo mengi sana katika Mkoa wa Kigoma na wa kwangu wa Morogoro, *huge area and empty*. Pia katika Mkoa wa Lindi, Mtwara na Ruvuma huko ndiko watakwenda, hawatakwenda Shinyanga ambako hakuna ardhi. Hawawezi kwenda kule watakwenda kufanya nini sasa, kwanza kule kumeshakuwa kukavu, ng'ombe wenyewe wameshaanza kwenda kwangu, sasa hivi wapo Mahenge na Ulanga kule. Kwa hiyo, watakwenda katika eneo ambalo jipya na watapewa maeneo hayo na kama kutalazimika kulipa fidia basi watalipa fidia inayostahili, hawawezi kupunjwa na sisi kama Serikali tunahakikisha kwamba wanalipwa fidia inayostahili kwa mujibu wa sheria.

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na marekebisho yake)*

Sehemu ya 4

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Sehemu ya 5
Sehemu ya 6

*(Sehemu zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Sehemu ya 7

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Sehemu ya 8
Sehemu ya 9

*(Sehemu zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Sehemu ya 10

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Sehemu ya 11

**MHE. GOSBERT B.BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa makosa na adhabu ambazo zinapendekezwa humu ukisoma kifungu cha 48 na 49 kinaonyesha kwamba kwa mtu atakayefanya makosa chini ya Muswada huu au sheria hii atapewa adhabu za aina mbili. Adhabu ya kwanza itakuwa ni faini pamoja na kifungo au vyote vinaweza kwenda kwa pamoja.

Sasa maneno yanayotumika hapa yanasema *not exceeding* (isiyozidi) milioni hamsini na kifungo kisichozidi miaka minne. Wasiwasi wangu hapa ni kwamba naona kama haijakaa vizuri kwa sababu unaposema isizidi milioni hamsini kwa maana kwamba inaweza kuwa milioni moja, laki moja, elfu hamsini au elfu moja na naona hapa inaweza kuja kutumika vibaya.

Nilikuwa nashauri kwamba kiwekwe kiwango kwamba kuanzia kiwango hiki na kisizidi labda shilingi milioni hamsini na kwenye adhabu ionyeshe kwamba mtu atakayetenda hilo kosa na ikathibitika kwamba ametenda hilo kosa atatiwa hatiani kwa kifungo cha labda miaka fulani na isizidi miaka fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ndilo pendekezo langu.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi ufuatao. Kwanza labda kuna haya maneno ya *natural person and not a natural person*. *Natural person* maana yake ni mimi na yeye na *non natural person* ni kampuni ndio maana kuna kutenganisha zile adhabu. Kama kampuni inafanya makosa basi faini yake haipungui milioni hamsini. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo napenda kulifafanua ni kwamba katika utaratibu wa leo wa *good governance* hutakiwi kumbana sana Hakimu kwa kumwekea hivyo viwango, anatakiwa Hakimu ndiye aamue, maana yake anafanya *discretion* pale, kuna kosa lingine kubwa kweli kweli ndio linakwenda milioni hamsini, lingine la katikati hapa litakuwa milioni saba, lingine dogo kidogo litakuwa milioni sita au tano. Kwa hiyo, ndio gharama za kujenga demokrasi namna hii. Kwa hiyo, hili sio jambo jipya kwa Tanzania, sheria zote ukisoma zinasema hivyo kuweka *leeway*. Labda mtaalam atusaidie lakini *my understanding* kama Mzee mmojawapo katika Bunge hili ndio hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina la ziada la kuongeza katika aliyoyasema Mheshimiwa Waziri kwa sababu ni kweli yule atakayekuwa anasikiliza hilo shauri atakuwa na *discretion,* kama kosa ni kubwa sana atatoa adhabu kubwa, kama ni dogo atatoa adhabu ndogo. Kwa hiyo, nakubaliana naye kabisa Mheshimiwa Waziri.

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kusimamia Maeneo ya Uwekezaji Rasilimali *(The Special Economic Zones Bill, 2006)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada huu kifungu kwa kifungu na imekubali pamoja na mabadiliko yaliyofanywa, hivyo naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Maeneo Maalum ya Uwekezaji Rasilimali (*The Special Economic Zones Act*, 2006) sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Mpango wa Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje wa Mwaka 2006**
***(The Export Processing Zones (Amendments) Bill, 2006***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niwasilishe Muswada wa *EPZ* na marekebisho yake mbele ya Bunge ili uweze kujadiliwa na hatimaye pengine kupitishwa.

Mheshimiwa Spika, kabla pengine sijawasilisha Muswada huu naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia nampongeza Mheshimiwa Edward Lowassa kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu. Aidha nakupongeza wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kuchaguliwa kuongoza Bunge hili. Kwa namna ya pekee nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Bukoba Vijijini kwa imani kubwa ambayo wamenionyesha kwa mara ya pili kuwa mwakilishi wao katika Bunge hili, nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kuniteua ili niwe mmoja katika Baraza la Mawaziri. Nachukua vile vile nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuweza kuchaguliwa na wananchi ili wawe Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo napenda sasa niwasilishe Muswada wa marekebisho ya *EPZ.* Maandalizi ya Muswada wa marekebisho ya Sheria ya Mpango wa Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje *(The Export Processing Zones (Amendment) Act*, 2006) yamekamilika sasa na Muswada huu pamoja na jedwali la marekebisho unawasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu ili kusomwa kwa mara ya pili na hatua nyingine zikifuata.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani za dhati kwa wale wote waliotuwezesha kukamilisha Muswada huu. Nawashukuru wataalam na wadau wote waliohusika katika utayarishaji na utoaji wa maoni na mapendekezo ambayo yaliboresha maeneo mbalimbali ya Muswada huu. Aidha, shukrani zangu ziwafikie Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara kwa uchambuzi na ushauri wao muhimu chini ya uongozi wa Mwenyekiti Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii. Muswada huu unakusudia kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Mpango wa Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje. Sheria ya *EPZ* ilipitishwa na Bunge tarehe 17 Aprili, 2002 na kuanza kutumika tarehe 1 Julai, 2003. Lengo kubwa la

kuanzishwa kwa *EPZ* ni kukuza mauzo yetu nje na kuongeza mapato ya fedha za kigeni ambayo yatachangia katika kukuza uchumi na kuondoa umaskini pia kuchochea kwa kasi kubwa utumiaji wa malighafi zinazozalishwa nchini mwetu. Aidha, program ya *EPZ* inatoa fursa kubwa kwa ajira kwa watu wengi katika muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, uzoefu wa miaka miwili wa utekelezaji wa sheria hiyo umebaini kwamba pamoja na mafanikio yaliyopatikana kuna mapungufu ambayo yameashiria nia ya kufanya marekebisho ya Sheria ya *EPZ* kwa lengo la kuboresha utekelezaji. Mapungufu yameonekana katika muundo wa usimamizi, katika vivutio vilivyotolewa kwa wawekezaji wa *EPZ* na katika uwiano wa sheria ya *EPZ* na Makubaliano ya Ushuru wa Pamoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*East African Customs Union Protocol*).

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Muswada huu ni kurekebisha sheria ya *EPZ* ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa program ya *EPZ* na pia kuwavutia wawekezaji wengi. Mambo muhimu yaliyozingatiwa katika marekebisho ya Sheria hii ni kama ifuatavyo.:-

(i) Kuunda mamlaka ya kusimamia mpango wa *EPZ (EPZ authority*) badala ya utaratibu wa kutumia Wakala *(EPZ implementing agent*) ambaye kwa muda huu amekuwa ni Shirika la Maendeleo ya Taifa *(NDC);*

(ii) Kurekebisha vivutio vinavyotolewa kwa wawekezaji wa EPZ; na

(iii) Kurekebisha asilimia ya mauzo ya bidhaa zinazozalishwa katika maeneo ya *EPZ* kwenye soko la ndani.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza inaeleza jina na mahusiano ya marekebisho ya sheria. Sehemu ya pili inapendekeza kufanya marekebisho ya jumla kwa kufuta neno *Agent* katika sheria na kuweka badala yake neno *Authority*.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo mengine ni kufuta sehemu ya nne ya sheria na kuweka sehemu nyingine badala yake ambayo ina mapendekezo ya kuunda Mamlaka ya kusimamia mpango wa *EPZ* badala ya utaratibu wa kutumia wakala. Sehemu hii vile vile inarekebisha muundo wa Baraza la Kusimamia mpango wa *EPZ* kwa kulipa uwezo na majukumu zaidi, pia kuliongezea idadi ya wajumbe wakiwemo wawakilishi wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, aidha, inaelezea uteuzi wa Mtendaji Mkuu wa mamlaka na majukumu yake, inatoa mapendekezo ya vyanzo na matumizi ya fedha, pia taratibu za kusimamia na kukagua fedha za mamlaka. Sehemu hii pia inatoa mapendekezo ya marekebisho ya vivutio vya uwekezaji wa *EPZ.* Mapendekezo haya kwa mujibu wa uzoefu uliopatikana katika kipindi cha utekelezaji na nia ya kuainisha vivutio hivyo na vile vilivyotolewa na Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* na vile vya mpango wa maeneo maalum ya uwekezaji *SEZ.* Katika mapendekezo hayo vivutio (c), (d), (e), (g) na (m) vimebaki

kama vilivyo kwenye sheria ya sasa. Vivutio (b), (f), (h), (k) na (n) vimefanyiwa marekebisho na vivutio (a), (i), (j) na (l) vimeongezwa.

Mheshimiwa Spika, pia sehemu hii ya Muswada ina marekebisho ya asilimia ya mauzo ya bidhaa zinazozalishwa katika maeneo ya *EPZ* kwenye soko la ndani. Lengo la marekebisho haya ni kubadili kiwango cha asilimia thelathini kinachoruhusiwa katika sheria ya sasa na kukioanisha na kile cha asilimia ishirini kilichomo katika Makubaliano ya Ushuru wa Pamoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Customs Union)*.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuvunjwa kwa Bunge mwezi Julai mwaka jana Muswada huu ulikuwa umesomwa Bungeni kwa mara ya kwanza (*first reading*). Tarehe 9 Februari, 2006 Muswada huu ulijadiliwa na kikao cha wadau na baadaye kikao cha Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara. Katika vikao hivyo wadau pamoja na wanakamati walitoa michango muhimu ambayo iliboresha Muswada huu. Mapendekezo ya marekebisho yaliyotolewa na wanakamati ni kama ilivyobainishwa kwenye jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naomba sasa kuwasilisha rasmi Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mpango wa Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje *(The Export Processing Zone (Amendment) Act*, 2006) pamoja na jedwali la marekebisho ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ili aweze kutoa maoni ya Kamati. Wakati huo huo nawakumbusha kuwa nimepokea jina moja tu la mchangiaji sijui ndio hali halisi. Kama wapo basi walete majina.

**WABUNGE FULANI:** Anatosha.

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO – MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mpango wa Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje wa mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nichukue nafasi hii kwa mujibu wa Kanuni ya 70, Kanuni ndogo ya Kanuni za Bunge Toleo la 2004 kutoa maoni ya Kamati yangu

kuhusu Muswada huu ambao unarekebishwa kwa Muswada unaoitwa *Export Processing Zones Amendment Act,* 2006.

Mheshimiwa Spika, kabla sijafanya hivyo naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati wenzangu kuwapongeza Wabunge wote kwa kufanikiwa kuingia katika Bunge lako Tukufu baada ya Uchaguzi ambao ulikuwa wa muda mrefu wa kuvunja rekodi wa karibu miezi minne ambao ulifanyika tarehe 14 Desemba, 2005. (*Makofi)*

Aidha, napenda kukupongeza wewe kwa kuchaguliwa kuwa Spika kwa kura nyingi. Ishara inaonyesha kwamba Waheshimiwa Wabunge wana imani nawe. Vile vile napenda kumpongeza Mheshimiwa Anne Makinda, Mbunge kwa kuchaguliwa kwa kura zote kuwa Naibu Spika. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chini ya uongozi wenu tunaamini kuwa Bunge litatekeleza wajibu wake kwa ufanisi, kwa kuzingatia matakwa ya Katiba ya Nchi na Kanuni za Kudumu za Bunge. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa Muswada. Kwa mujibu wa Kanuni ya 69(2) Toleo la Kanuni za Kudumu za mwaka 2004 Kamati ya Kudumu ya Bunge inaweza kumwita mtu yoyote asiye Mbunge kuja mbele yake na kuishauri juu ya jambo lolote. Hivyo basi kabla ya kuanza uchambuzi wa Muswada huu Kamati iliwaalika wadau mbalimbali ili kuja kutoa maelezo au maoni kuhusu madhumuni na maudhui wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliwaalika *The Tanzania Chamber of Commerce Industries and Agriculture (TCCIA)* pamoja na *Confederation of Tanzania Industries (CTI)*. Napenda kuwashukuru sana *TCCIA* pamoja na *CTI* kwa kushiriki kwao kutoa maoni kuhusu Muswada huu. *Tanzania Chamber of Commerce Industries and Agriculture* waliotoa maoni yao wakiwepo wenyewe kwa kuhudhuria. Lakini *Confederation of Tanzania Industries* walitoa mchango wao kwa maandishi na sisi tuliutumia katika kushughulikia Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maoni ya Kamati. Miaka miwili tangu kutungwa kwa Sheria ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji wa Mauzo ya nje *(EPZ)* hayakupatikana mafanikio yaliyotarajiwa. Maeneo hayo hayajaanza kazi hivyo tunaamini kuwa kuletwa kwa Muswada huu wa marekebisho kutaleta msukumo mpya utakaowezesha Mamlaka kuanza kazi zake mara moja. Kutekelezwa kwa sheria hii ni hatua mojawapo ya mikakati ya kuiwezesha sekta ya viwanda kuongeza mchango wake katika pato la Taifa pamoja na kulifanya Taifa letu kuwa la viwanda vya ukubwa wa kati ifikapo mwaka 2025. Kutengwa kwa maeneo maalum ya uzalishaji kwa mauzo ya nje kutahamasisha uanzishwaji wa viwanda hapa nchini. Kwa hiyo, mkakati huu kwa kweli tunaunga mkono sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa shughuli za uwekezaji katika maeneo maalum *(EPZ)* zinasimamiwa na Shirika la Maendeleo ya Taifa *NDC* lakini tutakuwa tumeona

jinsi eneo peke yake la uzalishaji wa mauzo ya nje *Ubungo Millenium Business Park* ambayo ilijengwa kwa makusudio hayo halijapata kiwanda hata kimoja miaka miwili tangu eneo hilo litengwe. Hali hii kwa upande inatokana na kutokuwa na mikakati thabiti ya uendelezaji wa eneo hilo ambalo lilijengwa na wafanyabiashara binafsi, hivyo uamuzi wa kuunda Mamlaka ya kusimamia shughuli hii hapana budi upongezwe sana na utaharakisha uwekezaji katika maeneo hayo ya uzalishaji kwa mauzo nje.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya sasa naomba nitoe maoni kuhusu vifungu mbalimbali. Kifungu cha 12(1) kifungu hiki kinahusu uhuru wa maamuzi wa Mamlaka. Kamati inakubaliana na kifungu hiki ila inasisitiza kuwa ili Mamlaka iweze kufanya kazi zake vizuri ni vyema Mamlaka hiyo ikawa na uhuru wa dhati na wa kweli katika kutekeleza majukumu yake bila ya kuingiliwa na chombo chochote katika utekelezaji wa majukumu yake. Katika biashara ambapo kila nchi duniani inagombea wawekezaji hao hao ambao ni wachache ni vizuri Mamlaka ikaachwa ifanye shughuli zake kibiashara la sivyo wawekezaji watasita kuja kuwekeza. Aidha, Serikali itekeleze majukumu yake ya kujenga miundombinu kwa dhati ili utendaji wa Mamlaka uwe na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 14(2) hiki kinahusu ujumbe kwenye Baraza la *Export Processing Zones*. Kulikuwa na maoni mengi kuhusu ujumbe katika Baraza, lakini kwa jumla tulikubaliana kuwa Baraza lipewe uwezo wa kumteua *co-opt* mtu yoyote kwa kadri mchango wake unavyotarajiwa. Kifungu kama hicho hakikuwepo. Kwa hiyo, zilikuja hoja kwamba fulani labda wangeingia humo lakini ukiweka kifungu hiki cha kuwapa nafasi na inaweza pengine sio wakati wote isipokuwa kwa wakati maalum kwamba wanashughulikia suala fulani ambao unahitaji mchango wa watu wa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Wajumbe waliona kuwa katika ngazi hii si vizuri katika wa *Trade Union Congress of Tanzania* kuwa Mjumbe wa Baraza hilo kwa wasi wasi kuwa hataweza kutetea maslahi ya wafanyakazi katika ngazi hiyo ambayo amehusika na maamuzi yake na badala yake amekubaliana na maamuzi ya Baraza kuwa *compromise.* Tunadhani kuna sheria ambazo ziko kule kwa hiyo yeye ni haki yake kuzisimamia kuliko kuingia kwenye kutunga sera halafu baadaye aende akatetee. Tunashukuru Mheshimiwa Waziri kukubaliana na kutoa uwezo huu wa *co-option* lakini vile vile Kamati ilipendekeza kwamba katika hali hiyo kwa sababu sheria za kazi zinahusika sana ni vyema Waziri wa Kazi akaingia kwenye Baraza hilo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kuwa pamoja na uanachama wa Benki Kuu, Umoja wa Mabenki au *Banker's Association* wangehusishwa kwa sababu Mabenki yakihusishwa basi yataweza kuelewa mwelekeo na mahitaji ya mikopo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 18(1) kifungu hiki kinaeleza jinsi Mamlaka itakavyoweza kupata fedha zake za kuendeshea shughuli. Kifungu hiki ni muhimu sana kwa vile kama Mamlaka itapata fedha za kutosha ni dhahiri kuwa haitafanya kazi zake kwa ufanisi. Kwa mfano wakati tukiianzisha *EPZ* mwaka 2002 Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)* lilipewa shilingi milioni 50 tu kuanzisha *EPZ.* Fedha hizo ni kidogo sana na

ndiyo maana *Ubungo Millenium Bussiness Park* hadi leo haijapata wawekezaji. Kamati inasisitiza kuwa ili *EPZ* ziweze kushamiri hapa nchini ni lazima Mamlaka za wahusika zipewe fedha za kutosha na ziwezeshwe kutekeleza majukumu ambayo zimepewa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kifungu cha 20(2) hiki kinahusu kukaguliwa kwa hesabu za Mamlaka na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(Controller and Auditor General - CAG).* Hali iliyojionyesha sasa ni kuwa *CAG* amezidiwa na kazi kiasi ya kutomudu kukagua kwa wakati unaotakiwa hesabu zote ambazo anatakiwa azikague Kikatiba. Ni vyema Taasisi hizi mpya zijengewe misingi ya kukaguliwa hesabu zao kwa mujibu wa sheria. Kamati inamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kuliona hili na hivyo kukubali ushauri wa Kamati na kuweka kipengele cha kumtumia Mkaguzi mwingine kwa kibali cha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, wengine wanaweza kusema labda hili halina msingi lakini juzi hapa wiki hii Waziri wa Fedha alitegwa aliweka mezani hapa Hesabu za Serikali zilizokaguliwa zilizoishia mwaka 2003. Sasa hivi kuna hesabu ambazo zilizoishia Juni, 2005 ambazo kwa kweli ndio zingekuwa *tabled* kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo tumeweka kwa dhati kabisa kwamba tuna wakaguzi wengi tu ambao wangeweza kuteuliwa wakamsaidia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ili kuondoa dosari za hesabu katika hizi Taasisi mpya ambazo tunazianzisha.

Mheshimiwa Spika, kifungu 21(1) kinahusu vivutio. Kamati inakubaliana na utaratibu wa kutoa vivutio au *incentives* kwa wawekezaji kwenye maeneo hayo kama inavyoonyesha kwenye Muswada kwa vile ndiyo njia pekee ya kuwapata wawekezaji wengi zaidi. Lakini Serikali inatakiwa kuwa makini zaidi na kudhibiti matumizi ya vivutio hivyo. Baadhi ya wawekezaji ambao sio waaminifu huwa wanatumia vibaya fursa hizo za vivutio.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 21(1)(f) kinahusu misamaha ya kodi na ushuru. Kamati inakubaliana na misamaha ya kodi na ushuru mbalimbali unatozwa na Halmashauri. Hata hivyo Kamati inashauri kuwa kuwe na uangalifu na utaratibu uwekwe wa kufidia upungufu wa kodi hizo za Halmashauri ili Halmashauri nazo zisishindwe kufanya kazi zao. Pamoja na Serikali kuwa waangalifu sana na kudhibiti tabia sababu zimeshatokeza kwenye hoteli hapa nchini ambapo hoteli zilipata msamaha wa kodi na vivutio vingine na wawekezaji lakini hoteli hizo zimeuzwa hata mpaka mara tatu. Sasa Waheshimiwa Wabunge hatuelewi vivutio hivi kweli vilitumika kufaidisha hoteli ile au imemnufaisha yule mwekezaji na amechukua faida zake na ameondoka. Kwa hiyo, hapo tuna tahadharisha kwamba kuwe na uangalifu na vile vile mikataba inayohusu vivutio na misamaha ya kodi iwe inafuatiliwa kwa karibu sana na kudhibitiwa ili kuondoa dosari hizi ndogo ndogo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 21(1)(L) kinahusu mwekezaji kuingiza wafanyakazi wa kigeni hadi 5 kwa wakati mmoja. Yako malalamiko mengi kuhusu wawekezaji toka nje wanaokuja na wafanyakazi wao kufanya kazi hapa nchini, kazi ambazo hazihitaji utaalamu mkubwa na hivyo kujaza nafasi za ajira ambazo Watanzania wangeweza kuzishika. Hali hii isipodhibitiwa kwa dhati basi lengo la uwekezaji la

kuongeza ajira na kukuza viwango vya kiteknolojia kwa Watanzania halitafanikiwa. *(Makofi)*

Ni vyema mahitaji ya kuendeleza kuendelea kuwepo kwa wafanyakazi wa kigeni yalingane na jinsi ilivyoanishwa kwenye mpango wa shughuli za uwekezaji yaani (*Business Plan).* Mwekezaji vile vile kwa kwa amepitia Kituo cha Uwekezaji (TIC) basi mipango hiyo ioanishwe na Sheria ya *TIC* ambayo inazungumzia vivutio hivi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 21(1)(n)(iv) kinahusu *Remittances Proceeds (net of all taxes and other obligations.* Kivutio hiki kisipoangaliwa vizuri kinaweza kikatumika vibaya. Mathalan mhusika anaweza kutoa kwa makusudi taarifa za gharama zisizosahihi kwa faida yake, hivyo Kamati inaishauri Serikali iangalie hali hiyo na kuziba mianya ambayo inaweza kusababisha kutoa taarifa zisizo sahihi na hivyo Taifa kupata hasara.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 20(1)(b)(iv) kinahusu mauzo ya bidhaa kutoka kwenye maeneo ya *EPZ.* Kifungu hiki kinaeleza kuwa asilimia 20 ya bidhaa zinazozalishwa katika EPZ kwa mwaka zinaweza kuuzwa katika eneo la uzalishaji. Utaratibu huu ni mzuri ili wenyeji nao waweze kufaidi bidhaa zinazozalishwa hapo ambazo kwa kiwango kikubwa zina ubora zaidi. Lakini hapana budi pawe na udhibiti zaidi ili bei zake zisije zikaathiri mauzo ya bidhaa za aina hiyo hiyo zinazozalishwa kwa ajili ya soko la kawaida au soko la ndani.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko. Pia naomba nimshukuru sana Waziri Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mbunge kwa ushirikiano wake na Kamati hii tangu alipokuwa Mjumbe wa Kamati hii hadi sasa akiwa Waziri wa Viwanda, Wizara ambayo inashughulikiwa na Kamati ya Uwekezaji na Biashara. *(Makofi)*

Vile vile napenda kumshukuru sana Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Bwana Wilfred Nyachia, Wakuu wa Idara na Wakuu wa Mashirika ya Umma na Taasisi na Wizara hiyo ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati hii hadi kufikia kutoa taarifa hii leo.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuwashukuru wadau *Tanzania Chamber of Commerce Industries and Agriculture* pamoja na *Confederation of Tanzania Industries* kwa michango yao mizuri ambayo imesaidia kuboresha Muswada unaohusika na pia kuonyesha kwa dhati kabisa kwamba wanaunga mkono mapendekezo katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, maoni haya yamewezekana kutokana na michango ya makini ya Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara ambao nitapenda sasa niwatambue:-

1. Mhe. Dr. Harisson Mwakyembe, Mb - Makamu Mwenyekiti
2. Mhe. Asha M. Jecha, Mb.

3. Mhe. Siraju J. Kaboyonga, Mb.
4. Mhe. Mwajuma H. Khamis, Mb.
5. Mhe. Vuai A. Khamis, Mb.
6. Mhe. Godwin F. Kimbita, Mb.
7. Mhe.Stella M. Manyanya, Mb.
8. Mhe. Fatma A. Mikidadi, Mb.
9. Mhe. Herbert J. Mntangi, Mb.
10. Mhe. Mohamed H. J. Mnyaa, Mb.
11. Mhe. Luhaga J. Mpina Mb.
12. Mhe. Mbaruk K. Mwandoro, Mb.
13. Mhe. Savelina S. Mwijage Mb.
14. Mhe. Yahya K. Issa, Mb.
15. Mhe. Dr. Lucy Nkya, Mb.
16. Mhe. Christopher Ole Sendeka, Mb.
17. Mhe. Lucy F. Owenya, Mb.
18. Mhe. Ahmed Ally Salum Mb.
19. Mhe. Haji J. Sereweji, Mb.
20. Mhe. Ahmed M. Shabiby, Mb.
21. Mhe. Mohamed A. Chombon, Mb.
22. Mhe. Mohamed S. Sinani, Mb.
23. Mhe. Abdallah S. Sumri, Mb.
24. Mhe. Nazir Karamagi – Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko ambaye vile vile alikuwa Mjumbe wa Kamati hiyo.
25. Mhe. William H. Shellukindo – Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa napenda kuwashukuru sana Wabunge Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara kwa kunichagua bila ya kupigiwa kura na vile vile kumchagua Mheshimiwa Dr. Mwakyembe bila ya kumpigia kura. Ni Kamati ambayo ina watu makini sana. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati hii wameonyesha ukomavu wa kisiasa wa hali ya juu walipojadili Muswada huu wakiongozwa na hoja ya mwana mikakati ya siasa *Political Strategies* anaitwa Dick Morris ambaye katika kitabu chake kinachoitwa *"The New Prince*" napenda kumnukuu alisema haya. *"If politicians were truly pragmatic and did was real in the public interest political process would be a lot clear, more positive, non partisan and issue oriented". (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana Bwana Damian Foka, Katibu wa Bunge kwa kuwezesha Kamati hii kufanya kazi zake vizuri. Pia nimshukuru Ndugu Aggrey Nzowa, Katibu wa Kamati kwa kuhudumia Kamati vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE – MSEMAJI WA UPINZANI WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa

kifungu cha 43(5)(b) na (c) cha Kanuni za Bunge, naomba nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada tajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pongezi za dhati kwako wewe kwa kuchaguliwa kwa kauli moja ya Waheshimiwa Wabunge wote. Aidha, nawampongeza Mheshimiwa Naibu Spika, Mama Makinda ameonyesha njia sisi akinamama kuwa wachapakazi wa hali ya juu, inalipa. Hivyo wanawake tufuate nyayo zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa shukrani zangu za pekee kwa Chama changu cha Wananchi *(CUF*) na viongozi wake wakuu kuniteua kuwa Mbunge Viti Maalum kuwakilisha Mkoa wangu wa Kagera, nashukuru kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria iliyofanyiwa marekebisho imeanzishwa na Mamlaka kamili ambayo kazi imepewa nguvu zote za sheria kama kifungu cha 4 cha Muswada huu unavyosemekana.

Kambi ya Upinzani inapenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri nini kimetokea kwa Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)* ambalo katika Sheria ya Mwaka 2002 ya Uanzishaji wa Viwanda Maalum kwa ajili ya Uuzaji Bidhaa zake nje ya nchi lilikuwa kama wakala wa kusimamia shughuli zote kwa mujibu wa Sheria ya *EPZ.*

Mheshimiwa Spika, tunamwomba Waziri aelezee Bunge kuwa sasa Shirika la Taifa *(NDC)* wakala pekee katika Sheria ya *EPZ* mwaka 2002 limeshindwa kazi hiyo ubunifu wa miradi na kuitafuta wawekezaji, wabia wa ndani na nje kwa maendeleo ya kuongoza pato kwa nchi yetu. Aidha, kutokana na hali halisi ya *NDC* ilishakuwa na uzoefu wa kutosha kusimamia mahitaji kama Sheria ya *EPZ* inavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, kuundwa kwa Mamlaka mpya itakayosimamia shughuli zote za *EPZ* na kuiacha *NDC* ambayo ilikuwa ni wakala pekee wa kufanya kazi hiyo ni sawa kabisa na kuuza nyumba tayari kununua kiwanja ukaanza ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utunzi wa sheria na uanzishaji wa Mamlaka ambao kimuundo na kutimiza unashabiiana na vyombo ambavyo tayari vipo vinashabiiana watendaji wa Mamlaka nyingine kuwa na watumishi ambao kwa njia moja au nyingine wamegeuza matumizi kwa Serikali hivyo basi ni bora *NDC* ambaye ni wakala kama Sheria ya *EPZ* ya mwaka 2002 inaonyesha kuendeleza kufanya kazi hiyo kwani wameshindwa na uzoefu wa kutosha na kazi iliyofanyika inaonekana kama ni kurekebisha, kama ni marekebisho basi yangefanyika lakini sio kuunda Mamlaka mpya.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka hiyo kwa hali ya kawaida ni lazima iwe kipindi cha kujifunza kazi rasmi kwanza kuonekana. Kambi ya Upinzani inaona haya ni matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi walalahoi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kama hivyo ilikwisha gusia hapo awali ibara ya 13(2)(d) inasemekana kuwa hiyo Mamlaka inayoundwa itakuwa na majukumu na kutayarisha ratiba za ndani na nje kwa ajili ya maonyesho ya biashara ya ndani na nje.

Ipo Bodi ya Biashara ya Nje *(BET)* ambayo imepewa Mamlaka kisheria na kufanya hivyo. Jambo hili linaweza kusababisha migongano kiutendaji na kutoshindwa kufikia kile kilichokusudiwa. Ni vyema tukaelezwa Mamlaka hizo mbili zitakazofanya kazi vipi bila ya kuingiliana.

Mheshimiwa Spika, kuna Viwanda vya Nguo ambavyo tayari vimo ndani ya Mpango Maalum wa *EPZ.* Viwanda hivyo vya Nguo vimepata vivutio vya uwekezaji, Viwanda hivyo vimeajiri wafanyakazi ambao asilimia kubwa ni akinamama.

Lakini kwa kusikitisha ajira wanayolipwa wafanyakazi hao ndogo mno kwa kulinganisha na hali halisi ya vivutio vinavyopata toka Serikalini. Aidha, kumekuwa na matabaka ya wafanyakazi katika biashara kati ya wageni na Watanzania ambao wageni hupokea mshahara mara mbili au tatu ule mshahara wa Watanzania.

Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri aliangalie tatizo hili na suala lengo la uwekezaji wake hili lina maana Watanzania wafanye kazi maneno hayo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona ni vizuri Waheshimiwa Wabunge kujaribu kurekebisha mafanikio ya *EPZ* mpaka hivi sasa tangu mpango huo ulipoanzishwa Watanzania wengi wamepata ajira za kiasi gani na kodi wamesamehewa kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, kifungu kinachohusu Uanzishwaji wa Baraza la Maendeleo Maalum ya Uanzishaji Mauzo ya Nje ya *EPZ* ibara ya 14(2) Waziri Mwenye dhamana Mipango, Uchumi na Uwezeshaji hayumo katika Baraza hilo. Hivyo ni muhimu Kituo cha Uwekezaji kupitia kwa Waziri wake kiwakilishwe katika Baraza hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha hoja. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kwa mara nyingine tena niwe mchangiaji wa kwanza katika hoja iliyo mbele yetu ya *Export Processing Zones.*

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha sheria hii ambayo ni *amendment* ya sheria ya awali. Mimi nafikiri imetupa nafasi nzuri ya kuweka mambo yetu mazuri katika azma ya kuweka *EPZ.* Vile vile nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati husika kwa kuchanganua mambo haya jinsi yangeweza kufanikisha suala zima la *EPZ.*

Mheshimiwa Spika, mimi nataka nizungumzie sehemu mbili ambazo kwa njia moja au nyingine nataka kusisitiza Serikali ili kufanikisha azma hii ya *EPZ* na ilete mafanikio tuzingatie mambo muhimu ambayo kwamba bila ya kuwepo mambo hayo tutakuwa tunataka mambo mazuri lakini sisi wenyewe tutakuwa hatujajipanga.

Cha kwanza ninataka kumhakikishia Mheshimiwa Waziri azma hii ya *EPZ* Serikali lazima tuhakikishe kwamba suala zima la umeme katika maeneo haya au nchini yawe yamerekebishwa vizuri ili tuweze kuleta ufanisi wa viwanda ambavyo kwamba vitawekezwa katika maeneo haya. Wawekezaji watakuwa na matumaini mazuri na kufanya kazi zao kama sheria inavyosema ikiwa suala la umeme halitozingatiwa.

Kwa hiyo, nikitazama sheria imehusisha ile *Council* ambayo wanaita *Authority Council* kuna Mawaziri mle ndani wanaosimamia *authority* hii au wanaungana kwa pamoja kuhakikisha kwamba haya mambo yanakwenda vizuri.

Sasa Wizara ya Nishati na Madini pamoja na taarifa mbalimbali ambazo wametuletea hapa Bungeni na mikakati ya kuboresha suala zima la umeme nchini ni vyema sasa hivi Serikali ifikirie ku-*invest* zaidi katika kuboresha suala zima la umeme ili twende sambamba na hizi sheria ambazo tunazipitisha hapa ambazo zitahusisha wawekezaji wakubwa kutoka nje.

Lakini kigezo cha umeme kama hakitakuwa na uimara hakitakuwa na uhakika kwa kweli, wawekezaji watakuwa wanasitasita na hatimaye wawekezaji hawa wanaweza wakatafuta sehemu nyingine kwenda kuwekeza wakati sisi tunayo sheria nzuri lakini wakatafuta dosari ambazo kwamba labda zitakuwa ni sababu ya wao kutokuja kwetu kuja kuwekeza katika viwanda hivi.

Mheshimiwa Spika, sasa nasisitiza kabisa *program* ya Serikali ya kuboresha hali ya umeme iende kwa kasi itafutiwe fedha za kutosha, *investment* ya kutosha katika suala la umeme tunafahamu sasa hivi tuna *gas*. *Gas* ile ambayo kwamba bado tunainunua kutokana na mikataba ambayo tumesaini na makampuni yaliyowekeza pale *Songosongo.* Lakini itafika pahala Tanzania itafaidika zaidi na *gas* ile, lakini kwa hivi sasa ni vema Serikali ikajiandaa kama nilivyosema kuwekeza katika mitambo ya kutumia nishati mbadala badala ya maji na mafuta ya *diesel.* Tunayo *gas* tuitumie kwa vizuri kuhakikisha tunaboresha suala zima la umeme katika maeneo ya *Export Processing Zone*s pamoja na nchi nzima. Hilo moja nilikuwa nataka nisisitize Serikali ilitazame kwa makini kwa sababu hii sheria ni nzuri isije ikawa ni sababu ya wawezekaji kutukimbia.

Mheshimiwa Spika, jingine nilikuwa nataka kuzungumzie mafungu ya fedha kwa ajili ya *authority* hii au matumizi yake. Sheria inasema ni kuendeleza *EPZ infrastructure*. Mimi nataka kusema kwamba pale katika bandari ya Tanga. Bandari ya Tanga ambayo kuna *Master Plan* ya bandari mpya ya Mwambani ambayo imekwisha wekwa michoro mizuri ambayo ni ya kuanzisha bandari mpya pale Tanga. Ingekuwa ni sehemu nzuri kwa ajili ya *Export Processing Zones*. Michoro ile ipo na viwanja vimekwishagawiwa. Mimi nilikuwa nataka kufahamu Je, *Development Funds* hizi ambazo zipo katika sheria zitasaidia kujenga *infrastructure* hii ya bandari ambazo kwamba zingekuwa ni mwafaka kwa ajili ya kuendeleza hii azma ya *EPZ* nchini.

Vilevile tuna bandari ya Mtwara ambayo ni *natural harbor* yenye kina kizuri, pia ingeweza kutumika kama *Export Processing Zone* ikiwa tutaboresha bandari ya Mtwara

na hatimaye kuweza kugawa maeneo ya *EPZ* kutoa ufanisi mzuri zaidi. Hii itasaidia kusambaza maendeleo na kuongeza ajira katika nchi yetu kwa upana wake. Sasa mimi nilikuwa nataka kujua je, *Master Plan* ambayo Tanga *Port* mpya imekwishawekwa hizi *Funds* za *Authority* zitasaidia vipi katika kuendeleza bandari hii ili tuweze na sisi kujua tunaweza kusaidiana vipi na Serikali kama Mkoa wa Tanga ili tuharakishe na kuhakikisha *EPZ* inaweka mizizi mizuri na hatimaye tuwalete wawekezaji na kuweza kufaidika na sheria hii kama inavyosema.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa kifupi nilikuwa na haya machache ahsante na kushukuru. (*Makofi*)

**MHE. RIZIKI SAIDI LULIDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia kuweza kuwepo hapa na aliyetujalia kufanya uchaguzi uliofanyika kwa uhuru, amani na utulivu.

Pili napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kishondo. Pia natoa pongezi kwa Mheshimiwa Edward Lowassa kwa kuchaguliwa kuwa Waziri Mkuu. Napenda kutoa shukrani zangu za dhati na kukupongeza wewe Spika. Mheshimiwa Samuel Sitta kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge letu na kuja na sera ya *standards* na *speed*. Mwisho kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Anne Makinda kwa kuwa Naibu Spika na kutuwakilisha sisi akina mama na bila kuwasahau Mawaziri, Naibu Waziri na Wabunge wote waliochaguliwa.

Mimi napenda kuzungumzia upande wa miundombinu. Kwa kweli hii *Export Processing Zones* ni kitu kizuri sasa kama itatuwezesha Mikoa ya Kusini kuwa na miundombinu ambayo itatuwezesha kuwa na barabara nzuri ili kuleta mawasiliano mazuri ya kibiashara na kuwapa nafasi wawekezaji kuleta maendeleo katika Mikoa ya Kusini. Kwa mfano, Wilaya ya Liwale ni Wilaya nzuri sana ambayo ina vivutio vikubwa sana vya mazao kama korosho na ufuta. Lakini kutokana na miundombinu ya barabara mbovu ambayo haipitiki hivyo inaifanya Liwale iwe kisiwa cha matatizo makubwa ya mazao yao bila kuuzika nje.

Pili, Lindi tulikuwa na Bandari nzuri sana, mimi wakati nazaliwa Lindi kulikuwa na bandari nzuri meli zimejaa mpaka nyingine ziko mlangoni. Lakini kwa sasa hivi hakuna hata meli wala jahazi. Hii inaleta ugumu wa uwekezaji na uletaji wa huu mpango wa *EPZ*. Ningeiomba Wizara ya Biashara na Viwanda ikishirikiana na Wizara ya Miundombinu itupatie muafaka wa hilo suala.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika hoja hii muhimu ya *EPZ*. Mimi kama mjumbe wa Kamati hiyo ya Uwekezaji na Biashara nachukua nafasi hii tu kuongezea machache ambayo nadhani ni muhimu licha ya kwamba nilikwishatoa mchango wangu ndani ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kuwepo kwa *EPZ*, ni kujenga uwezo wa uzalishaji bidhaa maalum kwa ajili ya masoko maalum na hasa masoko ya nje ili kuwezesha taifa kupata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, ili haya yaweze kufanyika tena kwa ufasaha lazima yawepo mambo makubwa yafuatayo:-

Kwanza eneo linalochaguliwa lazima liwe ni eneo ambalo ikiwezekana liwe ni eneo ambapo malighafi inapatikana kwa urahisi.

Pili, eneo hilo pia lazima liwe ni eneo ambalo miundombinu yake ni ya kisasa na ipo ya uhakika. Kama barabara, simu na kadhalika.

Lakini la tatu, eneo hilo ni lazima liwe ni eneo ambalo umeme wa uhakika unapatikana. Sasa hili la umeme naliwekea msisitizo kwa sababu sasa hivi tuko katika hali mbaya na nina uhakika hali mbaya ya upatikanaji wa umeme itachangia kwa kiasi kikubwa katika kudhoofisha viwanda vyetu.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji hasa katika masoko ya nje, ni uzalishaji ambao walengwa wanaonunua bidhaa hizo wanaweka taratibu na kanuni mbalimbali. Lakini kubwa ni kwamba bidhaa lazima zipatikane kwa wakati na hii imo ndani ya mikataba ambayo wanaweka na wazalishaji. Hivyo bidhaa zisipofika kwa wakati uliokusudiwa anayeagiza bidhaa anakuwa na haki ya kufutilia mbali oda aliyokupa na inaweza ikawa tatizo na hasara kubwa kwa mzalishaji.

Kwa hiyo, ni vizuri tukajenga mazingira mazuri ya kuhakikisha kwamba tatizo la umeme tunalijengea kanuni nzuri na kuhakikisha kwamba tuna mchakato mzuri wa kuhakikisha kwamba mahitaji ya umeme wa taifa yanafikiwa katika mpango maalum ili kuwezesha uchumi kujengeka kama tunavyokusudia.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ya Biashara ambayo inashughulika na mpango huu wa uwekezaji *EPZ*. Imekuwa katika miaka ilyopita haipati fedha za kutosha ili kuiwezesha kuwekeza na kuweza kuvutia wawekezaji kuwezesha kuwekeza. Tunapendekeza kwamba Wizara hii sasa kwa mtizimo mpya kabisa iwezeshwe kupewa fedha za kutosha ili kutenga maeneo yakayowezesha mpango huu wa uzalishaji kufanyika kikamifu. Miaka iliyopita kwa mpango huu wa *EPZ* walikuwa wakitengewa fedha kidogo sana, shilingi milioni 50 sasa milioni 50 utatengeneza mkakati gani na mpango gani wa kuwezesha taifa kuwekeza vizuri.

Ni vizuri mwaka huu katika Bajeti inayokuja Wizara hii ikapewa nafasi ya kutoa mapendekezo mazuri ya mipango na mikakati mizuri ya kuwezesha kutenga maeneo haya na kuyaboresha ili wawekezaji waweze kuvutiwa na kuja kuwekeza. Vinginevyo tutakuwa na taratibu kama zilizokuwa katika miaka iliyopita ambazo hazikuweza kusaidia kuibua uchumi.

Pamoja na kuwezesha Wizara hii kuangalia mapendekezo ambayo yalitolewa na Kamati ya kuitaka Wizara hii iangalia uwezekano wa kununua lile eneo la M*illennium Business Park*. Basi gharama za kununua eneo hilo ziwe pia limeangaliwa katika kipindi cha bajeti cha Wizara hii mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, eneo lile la *Millennium Business Park* ni eneo zuri la kisasa kabisa. Lakini sio eneo ambalo linafahamika vizuri. Kwa hiyo, natoa pendekezo kwamba tujaribu kutafuta njia ya kuwezesha eneo hilo likafahamika vizuri kwa wawekezaji na njia ambayo ingefaa sana na ambayo napendekeza ni kujaribu kuangalia namna ya kufanya maonyesho maalum katika eneo lile. Tunayo maonyesho ya sabasaba sawa, lakini tunaweza tukawa na maonyesho maalum basi tukafanya eneo lile likawa eneo la maonyesho maalum kwa nia hiyo ya kuwafanya wawekezaji waweze kulifahamu na umuhimu wake na kwa hivyo likatumika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, katika sheria hii ya *EPZ*, ambayo tunaifanyia marekebisho kipo kipengele kimoja ambacho mimi nadhani ni vizuri tukakiangalia upya. Kuna kipengele ambacho kinasema ni wajibu wa Wizara husika kusaidiana na wawekezaji pale wanapokuwa wanahitaji ardhi na tukasema tutashirikisha na vyombo vinavyo husika kusaidia kuondoa tatizo au kushughulikia maombi yale ya ardhi. Lakini ndani ya sheria hiyo tukasema kwamba pale ambapo Wizara itakuwa imeandikiwa isipojibu basi itakuwa na maana kwamba sasa ombi hilo limekubaliwa. Katika sheria za ardhi ombi kukubaliwa kuna hitaji vile vile kuwa na Hati ya kumiliki ardhi. Sasa haiwezekani tu tukasema tu *silence* kwa sababu hawakujibu basi tumepata ardhi tukadhani vile vile mwekezaji atalikubali hili. Ni vema tukaiangalia vizuri tukairekebisha hii sheria ili kuhakiki kwamba mwekezaji anakuwa na imani. Sidhani mwekezaji atakuwa na imani kwa kusema tu kwamba tuliwaandikia ardhi na hawakujibu na kwa hivyo wewe una haki na eneo hili, mwekezaji bado atahitaji kupata Hati ya kumiliki eneo hilo. Kwa hiyo, tujaribu kuirekebisha sheria hiyo

Mheshimiwa Spika, ningeomba vilevile kuangalia kwamba hiki kipengele cha ardhi nilichokizungumzia kinafanyiwa kazi. Kifanyiwe kazi kibadilishwe ili kwa kweli kiweze kuwavutia wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa nchi utaboreka kwa kuwa na maeneo maalum ya uzalishaji na mnapoingia katika mikataba yapo mambo ambayo sisi Watanzania hatuyafahamu. Lakini kwa wale ambao ni wawekezaji na wale ambao wanataka bidhaa kutoka kwetu mara nyingi wanaweka masharti maalum katika bidhaa wanazotaka zizalishwe.

Kwa mfano wazalishaji wale wa shuka, ambazo Mheshimiwa Waziri katika mpango ule wa *Special Economic Zones* alizungumzia. Wanaweka masharti maalum kwamba wewe utatengeneza shuka za upana fulani za urefu fulani kwa kiwango fulani. Lazima zinaposafirishwa kwenda kwao hazitakiwi kuwekwa *label* yoyote ya kuonyesha kwamba zimetengenezwa Tanzania. Hayo ni masharti ya biashara kwa hiyo ukilazimisha kutaka kuandika shuka hizo *Made in* Tanzania unakuwa umekiuka masharti ya kanuni zile za mkataba wa mauzo. Bidhaa zinaweza zikakataliwa.

Kwa hiyo, wakati mwingine ni vizuri na sisi tukajifunza kuelewa kanuni hizi za biashara masharti ya biashara na tukazingatia masharti ya biashara ili bidhaa zetu tunapozipeleka nje ya nchi ziweze kupokelewa bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kuchangia katika maeneo hayo machache na kama nilivyosema mimi nilikwishachangia katika Kamati yangu lakini labda nisema tu kwamba *EPZ* inatoa nafasi nzuri sana na sisi katika Wilaya yetu ya Muheza tunaweza tukaitumia sana *EPZ* hasa katika zao hili la machungwa na tusidhani kwamba ni lazima ukiwa na machungwa basi utengeneze *juice*. Kwa kupitia mpango huu wa *EPZ* tunaweza tukatengeza *concentrate* maalum zinazotokana na machungwa na tukapata soko maalum ambalo litanunua *concentrate* hizo na wao wakaenda kuzitumia kwa mahitaji yao maalum. Kwa hiyo, tuwe tayari kutumia *opportunities* kama hizi. *Business opportunities* kama hizi hasa za *EPZ*, kama Muheza ambako tunazalisha machungwa mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makosa*)

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hii hoja ya *Export Processing Zones*. Nianze na kuipongeza Serikali kwa kuleta hii hoja ya *amendment* ya *Export Processing Zones*.

Mheshimiwa Spika, *Export Processing Zones*, ni eneo linalozalisha bidhaa kwa ajili ya kuuza nchi za nje na bidhaa zinazouzwa nchi za nje dunia nzima wakati unauza bidhaa nje hulipi kodi. Kabla hatujaingia kwenye *export* ku-*encourage* viwanda kwa ajili ya kuuza nje kwanza tujiulize je, tunavyo viwanda ambavyo vinazalisha kwa ajili ya matumizi ya hapa nchini. Unapokuwa na kiwanda kinachozalisha kwa ajili ya matumizi ya hapa nchini baadaye unai-*improve* unasema sasa ngoja nihamie kwenye masoko ya nje ndiyo uneenda kwenye *Exports Processing Zones*, ama kiwanda chako kile kile unaweza kutenga eneo ukasema sasa bidhaa hizi zitazalishwa kwa ajili ya kuuza nje tu.

Sasa tujiulize nchi yetu ili iweze kuendelea lazima uhame kutoka kwenye kilimo uende kwenye viwanda na halafu uingie kwenye viwanda vya kuuza nje. Basi tuanze je, viwanda vingapi tunavyo kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa zetu hapa hapa nchini. Tuangalie tuanze labda hebu angalia wewe nguo unayovaa ina vifungo je, hebu tujiulize Waheshimiwa Wabunge, tunakiwanda kinachozalisha vifungo hapa nchini? Hebu tujiulize tuna viwanda vinavyozalisha sindano hapa nchini? Tuna viwanda ambavyo vinazalisha kalamu hapa nchini, kama tunavyo ni vingapi, je vinatosheleza?

Tunapo- *encourage* wawekezaji waje Tanzania wakazalishe kwa ajili ya kuuza nje ya nchi tujiulize je, umeme wetu upo, bei ya umeme ukilinganisha na nchi za *East Africa* kwa sababu mwekezaji anakuja Tanzania ili awekeze apate faida na ili aweze kupata faida lazima umeme uwe rahisi, maji yawepo, wataalam wawepo na mazingira mazuri ya uzalishaji yawepo. Sasa kama umeme ndiyo hakuna, maji hakuna, watalaam sina uhakika nadhani wataalm tunao. Je, wanajituma kiasi gani? Kwa sababu mwekezaji

anapokuja anataka apate hali ya uzalishaji iwe ni *conducive* ili bidhaa ile anayozalisha aweze kuiuza nje kwa bei ya chini, kwa sababu ni mashindano; na ukimleta mzalishaji anataka azalishe ile bidhaa auze nje kama bidhaa inayotengenezwa China. Anakuja anazalisha anaandika kwamba bidhaa hii imetoka China na anahama China anakuja kuhamia Tanzania kwa sababu ile *environment* itamwezesha yeye azalishe ile bidhaa kwa bei rahisi.

Sasa tunapozungumza *Export Processing Zones* tujiulize tunaweza tukawafanya hawa wawekezaji wakazalisha kwa bei nzuri na bidhaa ikawa bora na je, kabla hatujawaomba wazalishe kwa ajili ya *export* tunawaomba wazalishe kwanza kwa ajili ya kuuza hapa nchini? Kwa sababu unaweza ukashituka wewe bidhaa iliyozalishwa Tanzania inaenda nje ya Tanzania wewe unakwenda nje ya Tanzania inarudi Tanzania na Ikawa wale wanaonunua nje wakaja wakaiuza tena hapa nchini kwa bei ambayo ni chini.

Mheshimiwa Spika, ya kwangu ni hayo machache, naomba kuunga mkona hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mswaada huu.

Mheshimiwa Spika, kwanza naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa hai na wenye afya njema na kupita katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005. Pia nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kura za kishindo. Pia nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Aman Abeid Karume, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nikupongeze wewe na Naibu Spika, kwa kuweza kuchaguliwa na Wabunge na kuweza kuliongoza Bunge hili kwa umahiri mkubwa. Pia napenda kuwapongeza Mawaziri na Manaibu Mawaziri kwa kushika nyadhifa mbalimbali pamoja na Wabunge wote waliochaguliwa na walioteuliwa kuingia ndani ya Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza kwa dhati wana CCM wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa kunichagua kwa kura za kishindo kuingia katika mchakato kwa kupitia UWT nakuingia katika Bunge kupitia Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kaskazini Pemba; na pia nawapongeza wanaCCM wa Tanzania nzima kwa kuweza kukipigia kura Chama cha Mapinduzi kwa kura za kishindo.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nichangie machache kwenye mswaada huu wa sheria ya kurekebisha mpango wa maeneo maalum ya uzalishaji kwa mauzo ya nje wa mwaka 2005.

Kwa kuzingatia kuendelea kuongezeka kwa bei ya mafuta ya *petrol* duniani uzalishaji wa *ethanol* na *bio-diesel* kwa ajili ya kuchanganywa na *petrol* na *diesel* umekuwa na faida kubwa kibiashara duniani na mazao yanayofaa kuzalisha bidha hizi ni

pamoja na miwa, mafuta ya michikichi alizeti na *jetrofa.* Kinachotakiwa ni kuendeleza uzalishaji wa mazao haya na kuweka sera na sheria zitakazo endeleza matumizi.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri kuwa, kwa vile Zanzibar tunayo mazao ya aina hiyo na maeneo ambayo tunaweza kuzalisha mazao hayo na yakanawili sana visiwani humo. Ili kuwezesha kuzalisha zaidi mazao hayo naomba tuletewe wataalam wa kuwaelimisha wakulima wa Zanzibar yaani Pemba na Unguja suala la upandaji wa mazao haya na kuweza kuwekeza viwanda katika nchi yetu ya Tanzania ili kupunguza ongezeko la bei ya mafuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa vile kwenye zao la karafuu kumekuwa na kushuka kwa bei katika soko la dunia kwa hiyo naomba wawekezaji waje katika nchi yetu kuwekeza viwanda na kuzalisha bidhaa zinazotokana na karafuu; kwa mfano kama mafuta, sabuni dawa za meno na kadharika. Pia tuendelee na uuzaji ule ule huku tukiangalia kuwa tuendelee kuuza nje na pia soko la ndani linakuwepo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja nashukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Dakika za mwisho nimepokea ombi la Mheshimiwa Peter Serukamba, kwa sababu yuko mpakani na nchi ya jirani ya *DRC* naomba nimruhusu kwa kifupi kwa sababu *EPZ* inahusika.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, na mimi naomba kuchukua nafasi hii kushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia, ni kweli kwa sababu nipo mpakani.

Mheshimiwa Spika, najua *EPZ* katika maeneo ambayo yamepangwa na Kigoma imo lakini najaribu kuangalia toka ilivyoanza Julai 2003 sioni jambo lolote lililofanyika la kuwezesha hii *EPZ* kweli kutokea Kigoma. Kwa sababu unawezaji ku-*export product* zozote wakati Kigoma mpaka leo hatuna umeme, Kigoma mpaka leo hakuna miundombinu yakutosha.

Mheshimiwa Spika, labda Kigoma iliwekwa kwenye *EPZ* ili tusijione tumeachwa sana. Lakini nadhani ilikuwa haiwezi kutekelezeka ilipokuwa inaanzishwa. *EPZ* ni jambo la maana sana na ingekuwa kweli mkombozi katika uchumi wa nchi yetu na hakuna nchi iliyoendelea bila ku-*export*.

Lakini wakati Waziri anasema tulianzisha *agency* ambayo nadhani ilikuwa ni *NDC* kwa ajili ya kusimamia mambo ya *EPZ*. *NDC* kwenye Bunge lako hapa ilipitisha bajeti ya milioni 50, ukiangalia milioni 50 unawezaji kuanzisha kitu kikubwa kama *EPZ*.

Kwa hiyo, kwa vyovyote vile *NDC* toka mwanzoni ilikuwa imeandaliwa mazingira ya kushindwa, wasingeweza, maana milioni 50 huwezi kuanzisha kitu kama hiki

Hawa *NDC* waliomba shilingi bilioni 3, hawakupewa na Serikali ambayo maana yake nadhani hizo bilioni 3 wangeweza kufanya kitu katika hii *EPZ*. Lakini jambo ambalo linashangaza, kuna hii *Millennium Park*.

*Millennium Park* iko pale Ubungo, yalikuwa mwanzoni ni majumba tu, *PSRC* wakayauza, mfanyabiashara akayanunua kwa Bilioni 3. Baada ya muda mfupi akaweka uzio, akaiuzia Serikali kwa Bilioni 40.

Mheshimiwa Spika, haliingii kichwani hili, Serikali hii aambayo imekataa kuwapa *NDC* bilioni 3 kwa sababu hakuna uwezo ili waweze kuanzisha *EPZ* na iweze kuwa na maana kwa nchi yetu, lakini mtu mwingine anakuja tunaruhusu inanunuliwa hayo maeneo kwa Bilioni 40.

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani sasa wakati umefika, tuondoke kwenye siasa tuanze kufanya kazi ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba sana, *EPZ* ina nia njema kama kweli nia yetu ni kutaka nchi yetu iweze kuendelea basi ni mambo haya tuyanzishe ili *Authority* hii tunayo ianzishe tuipe nguvu iweze kufanya kazi ya kweli kweli. *(Makofi)*

Hii A*uthority* tunayoianzisha tusipo ipa nguvu haitafanya kazi labda tutakuja tena kuletewa sheria kwa mara ya tatu, tubadilishe tuanzishe jambo lingine, ambayo mimi nisingependa tuende huko.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja lakini naomba mambo haya niliyosema yachukuliwe kwa umakini mkali ili kweli *EPZ* iweze kufanya kazi kwa maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukrani sana kwa hoja zilizotoka kwa Wabunge katika kuchangia hoja niliyoitoa leo. Naomba kuwatambua Wabunge wafuatao waliotoa michango yao mizuri sana ambayo bila shaka itatuwezesha kuuboresha zaidi huu Muswada.

Kwanza, nitangulie na Mheshimiwa William H. Shellukindo ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Uwekezaji na Biashara. Pili, Mheshimiwa Savelina S. Mwijage, ambaye ni Mzungumzaji Mkuu wa Kamati hii katika Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah na Mheshimiwa Peter J. Serukamba.

Mheshimiwa Spika, hoja mbali mbali zimejitokeza. Sitaweza kuzijibu zote moja kwa moja lakini zile ambazo zitabakia Waheshimiwa Wabunge mtaziona katika utekelezaji. Lakini katika kujibu hoja, lazima nianze na Kamati muhimu ambayo ilijadili kwa kina ilikutana na wadau kwa hiyo wameuangalia Muswada huu kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati amependekeza kwamba Mamlaka iachwe kufanya kazi zake kwa uhuru thabiti, na mimi naungana naye mkono kabisa kwamba hili jambo tuhakikishe kwamba linafanyika. Kama ni Mamlaka iwe huru kusudi hata na wale wawekezaji waone kwamba inafanya maamuzi yake huru.

Amesema kwamba Serikali iwajibike katika kuandaa miundombinu muhimu, na hili tumeliweka humu kwamba kwa sasa kwa kiwango kikubwa ili kiwe kichocheo pamoja na kwamba tutawahamasisha, wawekezaji binafsi nao wawe na miundombinu hii ya kuweza kuwezesha *EPZ*. Lakini Serikali kama kichocheo kwa sasa, tutaweka umuhimu kwamba *EPZ* ambazo ziko kwa sasa kwa wingi zitakuwa ni za Serikali. Kwa hiyo tunakubaliana na ushauri wake.

Mamlaka iweze kuwa na uwezo wa kumwita mtu yoyote kwenye mikutano yake. Nafikiri hili ni jukumu la Mamlaka itakuwa mtendaji, wataendesha kwa taratibu walizonazo. Lakini kwa upande wa Baraza nafikiri hili pendekezo lilitolewa na Kamati na limekubaliwa na liko katika hii *schedule of amendments* kwamba wanaweza kum-*co-opt* mtu yeyote ambaye wanafikiri kwamba anaweza kuwasaidia kwa watu ule kitu wananchokijadili, anaweza kuwa na mchango mkubwa.

Tulipokuwa tunajadili palitokea mapendekezo mengi, watu wangapi wanaweza kuwa kwenye hili Baraza. Wengine wakasema Waziri wa kazi, wengine wakasema Mawaziri wa aina mbali mbali na wengine Baraza la Mabenki ambalo wanalo. Kweli *EPZ*, tunaweza kusema , kwa sababu ni jambo la uchumi ni mtambuka linahusu sekta zote.

Kwa hiyo huwezi ukamhusisha kila mtu vinginevyo unaweza kukuta umeunda Baraza la Mawaziri pamoja na Baraza lile la Wawekezaji ama wa sekta binafsi ambayo tayari tunalo Baraza ambalo liko chini la Rais ambalo linajumuisha Serikali pamoja na watu binafsi.

Sasa ukitaka kumjumuisha kila mtu kila mmoja ni mdau. Kwa hiyo ndiyo sababu tumekubaliana kabisa na pendekezo la Kamati kwamba Baraza liwe na uwezo wa ku-*opt* mtu yeyote kwa jambo linalojadiliwa ambalo wanaona anaweza akatoa mchango wake mkubwa.

Serikali iwe makini katika utoaji wa misamaha ya kodi ya ushuru kusudi isije ikatumika vibaya. Hili nafikiri tunazo sheria tayari. Tanzania tunao uzoefu mkubwa ambao tumeupata toka tulipoanza hivi vivutio kwa Tanzania. Kabla ya *Tanzania Investment Centre* tulikuwa na mamlaka nyingine, tulianza kule mbali, kulikuwa kuna mamlaka iliyoanza mwanzoni kabisa kabla hatujaweka hii *Tanzania Investment Centre* ambayo ilikuwa inaongozwa na Mheshimiwa George Kahama.

Tukaibadili ikawa *Tanzania Investment Centre*. Tumejifunza mengi kutoka hapo mpaka leo hii na kuweza kuboresha na kuziba mianya mbali mbali ambayo ilikuwa inatumiwa na wawekezaji ambao hawakuwa, naweza kusema siyo makini, wale ambao

walikuwa hawana nia kabisa ya kuwekeza labda kutumia tu mianya ya ushuru inayotolewa. Nafikiri sasa hivi sheria ambazo tunazo zinatosheleza. Lakini pale tunapozigundua kwamba kuna mwanya kuna Taasisi zinazohusika, Waziri wa Fedha, *AG* na Taasisi mbali mbali zinapendekeza ili mianya izuiwe kwa sababu tunataka Tanzania inufaike na hivi vitega uchumi vinavyokuja katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kutoa *compensation* kwa Halmashauri. Sisi tunafikiri kwamba hizi *concept* ya *EPZ*. Na *SEZ* ambayo tumepita, kwa mawazo ya haraka haraka unaweza ukaichukua kwamba ni nchi ya nje ambayo iko ndani ya nchi. Mtu ameamua kutoka huko aje afanyie kazi yake pale kama nchi ya nje. Anatumia kasehemu ka Tanzania kama nchi ya nje azalishe pale kusudi aweze kuuza nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Slpika, sasa, Tanzania tunafaidi nini kufanya hivyo, kwa sababu atakapotumia umeme ni umeme wetu ataulipia, maji ni maji yetu atayalipia, wafanya kazi ambao atawatumia ni wa kwetu watapata ajira, lakini vile vile watapata utaalam. Hiyo ndiyo maana ya *SEZ* na maana ya *EPZ* kwamba tunapata hilo. Halafu na vile bidhaa inavyotolewa nje, inahesabika imetoka Tanzania. Kwa hiyo, inaingia katika pato la taifa kama mauzo ya nje.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hii ni njia ya haraka haraka kuleta viwanda katika Tanzania na kuweza kupunguza hili tatizo la ajira kwa wengi. Na hii kuna Mheshimiwa Mbunge ameuliza hilo suala huko tunakokwenda kwamba Watanzania tunanufaikaje na *EPZ* ama *SEZ*. Ni Hayo ambayo ndiyo tunayapata, na nchi nyingi zimeweza kunufaika kwa njia hiyo na ndiyo sababu tunaweka hivi vivutio kusudi walete nchi yao ndogo katika nchi yetu, wafanye vitu vyao ndani humu. Sisi tutajifunza kwao, na sisi huko nje baada ya kujifunza ule utaalam na kupata ile taaluma, tunaweza kutoka kwenye hizo tunaweza kutoka kwenye hizo tukaweza kuzifanya katika maeneo yetu huko nje.

Mheshimiwa Spika, nizungumze wawekezaji kuleta wafanyakazi wao wataalam, wapatikane hapa hapa ili wasichukue fursa za Watanzania. Tunakubaliana na hilo na ndiyo sababu katika sheria inzungumza kwa sababu hii inaoana na sheria ya *Tanzania Investment Centre (TIC)* iliyopo sasa na ya *SEZ* na hii kwamba mwekezaji anaweza kuruhusiwa kuingiza wataalam watato, lakini baada ya hapo akitaka kuingiza mtu yeyote kwanza itaangaliwa kama yule anayetaka kumwingiza utaalam huo uko hapa Tanzania ama haupo hata Tanzania.

Kwa hiyo haitakuwa *automatic* kwa sababu anawekeza pale basi atamleta mtaalam wake, watano tu ni katika sheria zetu kama kivutio kimoja wapo, kwanza ni mwekezaji mwenyewe inabidi alinde mali yake, pili ana wataalam aliokuwa nao kwa sababu anawaleta hapa lazima aendeleze nao, hawezi akaja tu akaleta tu halafu akaachia vitu vyake. Halafu tatu, kuna uangalizi wa mali zake.

Lakini kwa hayo yote ukiyajumuisha, huwezi kuwa na zaidi ya watu watano, na hakuna *EPZ* ambayo utaiweka hapa iwe inaendeeshwa tu, kiwanda kinaendeshwa na watu watano, lazima wawe wengi tu na katika wengi hao , tunasema hao wengi waliobaki wawe ni Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja iliyotokana na Mheshimiwa Savelina S. Mwijage, Kambi ya Upinzani ya kusema kwamba kwa nini tunatoa *NDC* kama wakala kuanzisha Mamlaka kwa hiyo *NDC* imeshindwa kazi yake. Tunasema la, hasha, ni katika uboreshaji. *NDC* tumekichukua kama chombo chetu ambacho kitakuwa kinaanzisha viwanda vikubwa vikubwa, tunasema ni viwanda mama.

Vile viwanda vikikua ndiyo vinatoka kwenye *NDC* vinakwenda kujitegemea huko nje. Ina majukumu makubwa, kati ya hayo majukumu sasa hivi ndiyo ina jukumu la kuendeleza miradi yote ambayo ni ya *Mtwara Development Corridor, Central Development Corridor*, miradi ambayo tulikuwa tunazungumza hapa Waheshimiwa Wabunge, tunazungumzia kwamba lazima tuendeleze uchimbaji wa Makaa ambayo yako Mchuchuma, Liganga, *Soda Ash*, kuna miradi mikubwa mikubwa. Sasa tumeona kwamba ili *NDC* iweze ku-*concetrate* katika hiyo miradi mikubwa ambayo ni muhimu sana katika kuendeleza Taifa hili, mnajua sasa hivi tuna tatizo la umeme na ninyi hapa katika kuzungumza Wabunge waliochangia wanasema umeme linaweza kuwa tatizo moja wapo la kuwafanya wawekezaji wasije hapa Tanzania. Katika *Master Plan* ya kuhakikisha kwamba umeme una-*stabilize* Tanzania ni pamoja na kuondokana kutegemea *Hydro*. Tutegemee gesi, tutegemee Makaa ya Mawe.

Sasa, *NDC* acha ishughulikie hayo. Tuwe na mamlaka ambayo itashughulikia hili jambo la Mamlaka peke yake, na sisi siyo peke yetu tunaofanya hivi. Mamlaka zimeundwa, nafikiri Mheshimiwa Ngasongwa alipokuwa anatoa *speech* yake jana, amezungumzia juu ya nchi mbali mbali ambazo zimefanikiwa katika upande wa *SEZ* na zilizofanikiwa katika upande wa *EPZ*. Kwa hiyo, sasa tuwe na Mamlaka ambayo itashughulikia na hilo tu la kutafuta wawekezaji waje kuwekeza hapa Tanzania katika Miundo yetu ya *EPZ*. Vile vile vile amezungumza, Mheshimiwa Savelina S. Mwijage, amezungumza kwa nini sasa *EPZ* na *Board of External Trade* mbona zinaingiliana? Kuna tofauti gani?

Mheshimiwa Spika, kwa mchango wake Mheshimiwa Savelina ni mzuri lakini, inabidi ajue tofauti kati aya *EPZ* na *Board of External Trade*. *Board of External Trade* inashughulikia bidhaa za nje, kuuza bidhaa za Tanzania nje na vile vile kutafuta masoko huko huko nje bidhaa gani ambazo Tanzania tunaweza tukaleta hapa tukazalisha katika viwanda vyetu. Lakini *EPZ* inashughulikia viwanda hapa Tanzania ambavyo vitaweza kuzalisha bidhaa hapa kwetu na kuweza kuziuza nje. Na bidhaa ambayo inazalishwa humu katika haya maeneo ya *EPZ*, huyu ni mwekezaji ambaye tayari amekwishapata masoko.

Anazalisha maalum kwa kulenga soko. *Board of External Trade* ni jumla bidhaa zote, yawe ni mazao ambayo hayajasindikwa, yale yaliyosindikwa. Iwe bidhaa yoyote iwe ngozi, iwe ndege, ili mradi kuna soko, *Board of External trade* italitafuta huko nje na kuwambia Watanzania kutoa taarifa mahali fulani kuna soko, bidhaa hii inaweza kuuzwa kule. Lakini wenyewe hawajihusishi na kuzalisha, *EPZ* inazalisha.

Mheshimiwa Spika, ameuliza toka *EPZ* kuanza mpaka sasa hivi, Watanzania wangapi wameajiriwa katika *EPZ*. Takwimu tulizonazo hadi mwaka 2005, Watanzania 1,800 walipata ajira katika viwanda vya *EPZ*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ameuliza vile vile kwa nini Waziri wa Mipango na Uwekezaji hayupo katika Baraza la *EPZ*. Mchango wake tumeuchukua na mimi nakubali kwamba Waziri wa Mipango aongezwe katika Baraza la *EPZ*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rished Abdallah amezungumzia masuala ya ujumla. Kwanza, la umeme na limezungumziwa na Waheshimiwa wengine ambalo tunakubaliana nalo. Kweli bila kuwa na umeme, bila kutatua tatizo la umeme, hapa wawekezaji hawataweza kuchukua nchi yetu kama kivutio kimojawapo. Kwa sababu umeme ni mojawapo ya vitu ambavyo vinaweza kuwa *disincentive* kwa sababu vitaongeza gharama ya uzalishaji. Ili Tanzania tuwe kivutio cha wawekezaji hawa, wanaangalia gharama. Gharama zetu zikiendelea kuwa za juu pamoja, siyo umeme kukatika katika tu, hata na ubora wa umeme. Kama unasema ni Voti 440, ziwe 440, 220 ziwe 220 kusudi kuhakikisha kwamba vyombo vyao viko salama. Hili tunakubaliana nalo na Serikali tayari imekwishalichukua na sasa hivi ndiyo changamoto ya Awamu ya Nne na ndiyo tunachukulia kuhakikisha kwamba sasa kutoka sasa hivi tumepata mafundisho ya kutosha ni wakati wa kuwa na umeme wa uhakika. Hata kama itatugharimu sana, lakini tuhakikishe kwamba tunaupata kwa sababu ndiyo msingi wa maendeleo ya nchi yoyote.

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Tanga, Bandari za Mtwara kuwa maeneo ya *EPZ*; Katika mpango wetu ambao tumeuweka, hizi Bandari zote mbili zimo katka maeneo ambayo tumeangalia kwamba yanaweza kuwa ya *EPZ*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mntangi amezungumzia sana juu ya umuhimu wa kuwa na umeme, tunakubaliana naye, kupatikana kwa pesa za kutosha kama tunataka kweli kweli, tuna dhamira ya kuanzisha haya maeneo ya *EPZ*, sisi tutahakikisha kwamba hilo Serikali tumelichukua na mtaliona katika Bajeti ya mwaka ujao ambayo tutaiweka. Tutaweka umuhimu wa hilo kusudi kuanzisha kwamba tunayaanzisha haya maeneo na Bajeti inatosheleza. *Millennium Park* kufanywa kama maonyesho, ni mchango mzuri ambao ametoa. Ni kweli, kujitangaza tutatumia mbinu mbali mbali pamoja na hilo, pamoja na kuziweka kwenye *Website*, ni mbinu tu ili mradi tunatangaza Tanzania kwamba tunavyo vivutio na vingine tayari vipo tayari tunaweza kuvitumia.

Mheshimiwa Spika, pia amezungumzia juu ya sheria ya nchi, *amendment* kama inaweza kuwa *disincentive* kwa wawekezaji; Wakati Serikali inatafakari hayo, lakini kwa sasa hivi *EPZ* tunaona kwamba Serikali itasimamia na kuwa na miundombinu ya Serikali kusudi hili na lenyewe lisijelikaanza kuwa kikwazo. Kwa hiyo, miundombinu ambayo itakuwa imetayarishwa na Serikali itakuwepo. Kwa hiyo, mwekezaji anaweza kuja moja kwa moja akaingia katika Miundombinu ya Serikali. Hiyo *land* itakuwa tayari imechukuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, amezungumzia sana juu ya kuboresha miundombinu ya Kusini, Liwale, Lindi. Nakubaliana naye kama tutaweka *EPZ* huko, nimezungumzia Mtwara, tumekwishaiweka katika mipango hiyo. Lakini ili tufanikiwe tutahakikisha kwamba miundombinu ambayo inahitajika ili kuweza kuwavutia wawekezaji wawekeze pale, itakuwa imetengezezwa. Lindi, Liwale kama zitatokea kwamba kuna *SEZ*, ama vingine hata siyo lazima sehemu iwe imepangiwa *EPZ* ama *SEZ* ndio miundombinu ya pale iboreshwe. Sehemu ambayo ni muhimu ya Tanzania ambayo kuna wazalishaji wengi ambayo bidhaa inabidi kuweka kule, inabidi kuwaweka humu. Kwa hiyo, suala la miundombinu pamoja na kwamba tunaliwekea umuhimu sana wakati tunataka kuwavutia wawekezaji lakini hata sisi Watanzania wenyewe ambao tuko humu tunahitaji ili tuweze kupitisha mazao yetu yaweze kufika maeneo yote ya Tanzania.

Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro amezungumzia suala la umeme ambalo nimekwishalizungumzia na amezungumzia jambo la kulazimisha bidhaa ambayo inatoka *EPZ* iuzwe hapa nchini ili kusudi isije ikatoka hapa nchini ikaenda nje, halafu ikarudi kule. Hilo suala nafikiri kwa sasa hivi kwa huu mpango *EPZ* haliruhusiwi, wanaruhusiwa asilimia 20 tu kama mnavyoona kwenye Muswada. Lakini, kama mtu anataka kulenga soko la ndani, kuna nafasi maanake fursa zimetolewa hapa nyingi sana tu. Kuna nafasi ya *SEZ (Special Economic Zones)* akienda huko anaweza kutumia nafasi hiyo akauza hata humo ndani. Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah amezungumzia Karafuu na kuwashawishi wawekezaji waje kusindika hapa yatoke mafuta ya Karafuu ana Marashi. Na mimi nakubaliana nayo, kwa sababu mkakati wetu wa kwanza katika Wizara na Biashara ambao si lazima katika *EPZ*, ni kuhakikisha kwamba mazao yetu kwa wingi yanasindikwa kabla hayajauzwa nje. Nilikuwa nazungumza na Umoja wa Wafanyabiashara wa Korosho, nikawambia Korosho ndiyo kitu rahisi ambacho tunaweza kuanza nacho ili kuhakikisha angalau kwa miaka miwili, asilimia zaidi ya 75 korosho inasindikwa hapa Tanzania, sio kuuzwa nje kama malighafi. Kwa hiyo, tunakubaliana na wazo lake. Huo ndio mkakati wetu ambao tunao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Peter J. Serukamba; amezungumzia ya *EPZ* Kigoma. Mimi kwa mawazo yangu binafsi Kigoma kama Kigoma, siyo *EPZ* tu, tunaweza kuifanya *SEZ*. Kwa sababu Kigoma kama Kigoma, tayari tuna soko kubwa la Kongo ya Mashariki, tuna Rwanda, tuna Burundi, imejiweka katika sehemu nzuri. Kwa hiyo, ndiyo sababu Mheshimiwa Msabaha alipokuwa anazungumza juu ya mpango wa umeme, Mheshimiwa Rais alipokuwa anazungmza na Mheshimiwa Mramba alipokuwa anazungumzia juu ya Miundombinu. Suala la Kigoma na lenyewe limo kwa sababu Kigoma ina *potential*, ni mlango wetu kwa upande wa huku, lazima tutumie. Kwa hiyo, napenda kukubaliana na yeye juu ya hilo kwamba tutaliangalia. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, *Millennium Park* amesema iliuzwa kwa shilingi Bilioni 3, halafu ikanunuliwa kwa shilingi Bilioni 40. Nafikiri *Millennium Park* haijanunuliwa. *Millennium Park* ipo, Serikali tulikuwa atunazungumza namna sasa tuichukue, bado tunashindana; mwekezaji anapenda mibilioni zaidi, sisi tunafikiri kwamba thamani yake ni karibu bilioni 14, 16, lakini bado hatujakubaliana namna gani. Kwa hiyo, *Millennium Park* bado haijanunuliwa.

Kwa hayo, machache nimejitahidi kujibu kwa haraka haraka hoja zilizotolewa na Wabunge. Napenda kushukuru kwa mchango wao na tutautekeleza. Ahsante sana. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.*(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Mpango wa Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje wa Mwaka 2006 *(The Export Processing Zones (Amendments) Bill 2006)*

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3

*(Vifungu ilivyotajwa hapo juu vilipitiswa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 4

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 5

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 6

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 7

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Mpango wa Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje wa Mwaka 2006 *(The Export Processing Zones (Amendments) Bill, 2006)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada uitwao *The Export Processing Zones (Amendments Act), 2006*, pamoja na marekebisho yake kifungu kwa kifungu na kukubali. Hivyo basi, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa *Export Processing Zones (Amendment Act), 2006*, Sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. ZAKIA H. MEGHJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**(Hoja ilitolewa iamuliwe)**
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliobaki hauturuhusu kuingia katika shughuli zile za Uchaguzi ambazo sasa zitafanywa wakati wa Jioni Saa 11. Kwa hiyo, nasitisha Bunge kabla ya muda wake ili tuweze kusimamia na kwenda kupumzika.

*(Saa 06.58 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Bunge lilirudia)*

## UCHAGUZI WA WAJUMBE KWENYE TAASISI MBALIMBALI ZA KIBUNGE

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu katika chaguzi hizi za Bunge, *Returning Officer* ni Katibu wetu wa Bunge. Kwa hiyo, sasa nitamwachia aweze kuendelea kwa utangulizi na maelezo mengine yanayohusu nafasi mbalimbali na idadi ya wagombea.

**ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, leo hii Bunge lako Tukufu litafanya chaguzi za kujaza nafasi mbalimbali. Tayari ofisi yako ilishatoa matangazo kwa nafasi za *ACP-EU,* Vyuo Vikuu yaani Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Sokoine (Kilimo), Chuo Kikuu Huria, Chuo Kikuu cha Mzumbe, *SADC PF,* Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki, Bunge la Afrika na Makamishna wa Tume ya Huduma za Bunge. Tulitoa matangazo hayo na Waheshimiwa mbalimbali wameshaleta maombi ya kugombea nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba tuanze na nafasi ya kwanza. Lakini kabla ya hapo nadhani ni vizuri kama tungepiga kengele ili wale Waheshimiwa Wabunge walioko nje waweze kuingia ndani. Utaratibu mwingine utakaofuata ni kwamba, kwa wale ambao tutawataja kama wagombea basi watatoka nje ili kila mmojawao apewe nafasi ya kujieleza kwa muda wa dakika tatu.

Mheshimiwa Spika, naomba tuendelee.

*(Hapa kengele ilipigwa ili Waheshimiwa Wabunge waliopo nje ya ukumbi waweze uuingia Ukumbini)*

**SPIKA:** Katibu, tuendelee na nafasi hiyo ya kwanza.

**UCHAGUZI WA UJUMBE WA *ACP-EU***

**ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE:** Kwa mujibu wa mkataba mpya wa ushirikiano kati ya nchi za Afrika, Caribbean na Pacific na Jumuiya ya nchi za Ulaya uliosainiwa tarehe 23 Juni, 2000, Tanzania kama mwanachama, inatakiwa iwe na mjumbe mmoja atakayewakilisha Bunge la Tanzania. Kwa mantiki hiyo, leo tarehe 16 Februari, 2006 wagombea wawili wa nafasi hiyo waliojitokeza watasikilizwa na hatimaye kupigiwa kura baada ya kuwa wameulizwa maswali. Wagombea hao ni Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama na Mheshimiwa Kilontsi Muhama Mporogomyi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza, wote hawa kwanza watatoka halafu atakuwa anaitwa mmoja mmoja na atajieleza kwa muda wa dakika tatu. Ahsante.

**SPIKA:** Haya, tunawaomba Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi watoke nje. Anayetangulia ni nani, maana anayetangulia hana haja ya kutoka. Nani anatangulia? Balozi Mshangama?

*(Hapa Mhe. Kilontsi Mporogomyi alitoka nje ya Ukumbi wa Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani tukubaliane. Anayefika hapa bila maneno zaidi aendelee tu kuongea kwa sababu anajua ukomo ni dakika tatu na kama kuna maswali ni yasiyozidi matatu.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mimi ndiye Abdi Hassan Mshangama. Kwa vile ndiyo mara yangu ya kwanza kuzungumza hapa, pamoja na muda mfupi niliopewa, napenda niwapongeze viongozi wote wa ngazi zote kwa uteuzi na vile vile niwakumbuke wapigakura wa Jimbo la Lushoto kwa kunipigia kura asilimia 90 kufika hapa.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nafasi hii nikiamini kwamba ninao uzoefu, ujuzi na umahiri wa kuwezesha kufanikisha matarajio ya Tanzania katika ushirikiano huu wa nchi za Ulaya Magharibi na nchi za *ACP* Afrika, Caribbean na Pacific.

Kama nilivyoeleza kwenye maelezo mafupi, nilifanya kazi katika Wizara ya Fedha kwa miaka 20 kuanzia ngazi ya Mchumi mpaka Naibu Katibu Mkuu na miaka yote hiyo nimekuwa nikihusika na mambo ya *negotiations* Ulaya na nchi nyingine za dunia. Kwa miaka mitano, 1990 hadi 1995 nilikuwa Balozi wa Tanzania pale Brussels na *agenda* yangu kubwa ni ushirikiano wa nchi za Afrika na Caribbean.

Katika muda huo, kwa heshima kubwa sana ya Tanzania na mimi mwenyewe, wale wenzangu 71 wakaniteua mimi kuongoza majadiliano na Wazungu mpaka kufanikisha sehemu ya pili ya Mkataba wa Lome. Wale ndugu zangu wa Hazina mliowaona juzi pale watasema kwa umahiri, wale ni sehemu ya *product* ya Hazina, Hazina pale ni kisima cha uzoefu. Kwa hiyo, naomba mnipe kura zenu zote za ndiyo nikawakilishe.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali.

**WABUNGE FULANI:** Hamna.

**SPIKA:** Maswali.

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Balozi Mshangama. Sasa aitwe Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi.

*(Hapa Mhe. Kilontsi Mporogomyi aliingia ndani ya Ukumbi wa Bunge)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mporogomyi, endelea tu.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Kiswahili, Kiingereza?

**WABUNGE FULANI:** Vyovyote.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** *Honourable Speaker, honourable Ministers, Deputy Ministers and my fellow Members of Parliament; my name is Kilontsi Mporogomyi, currently a member of the African Caribbean, Pacific and European Union Joint Parliamentary Assembly and now saving as Chairman of the Negotiations of the Economic Partnership Agreement. (Applauses)*

*When I joined the ACP-EU JPA, I was made a member of the Development Finance and Trade Committee, in which I served very well in that Committee and I was appointed to a number of other Sub-committees. I am now also a member of the Conflict Resolution and Management Committee of both the ACP and the EU in the Join Parliamentary Assembly. (Applauses*
*)*

*Now, let me just finish one thing. The current issues in the negotiations in the Economic Partnership Agreement involve around negotiations on the budgetization process of the EDF, a resourc envelope of the European provided by the European Commission and I recognize that many of the issues that are current being discussed are issues that concern all the African, Caribbean and Pacific Countries. (Applauses)*

*Ladies and gentlemen,* nawaombeni kura zenu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali.

**WABUNGE FULANI:** Hamna.

**SPIKA:** Maswali?

**WABUNGE FULANI:** Hamna.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mporogomyi.

Vijana gawa karatasi sasa za kupigia kura.

*(Hapa Karatasi za kupigia kura ziligawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani tutapiga kura hapo hapo tulipoketi ili kuokoa muda.

Vijana, haraka kugawa karatasi, tuna chaguzi nyingi sana. Karatasi zigawiwe. Kuna Waheshimiwa hawajapata karatasi za kupigia kura?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Lo, lo, lo, aisee! Waheshimiwa, wote tumepata karatasi za kupigia kura?

**WABUNGE FULANI:** Bado.

**SPIKA:** Bado! Pale Mheshimiwa mmoja, pale na pale.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Kuhus utaratibu Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU SPIKA:** Sina Kanuni ya hii, lakini walivyojieleza sivyo walivyokaa kwenye karatasi ya kupigia kura.

**SPIKA:** Oooh! Ahsante kwa kutukumbusha hilo ingawa kwa baadhi yetu inakuwa limeshapita. Lakini aliyejieleza wa kwanza ni wa pili kwenye karatasi ya kura na bahati njema wala hawafanani sana. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla ya kukusanya kura naomba tutulie, vijana wanafanya hesabu, watuhesabu idadi yetu tuliomo ndani ya ukumbi, naomba tutulie.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walihesabiwa)*

**SPIKA:** Katibu, umepata idadi?

**ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE:** Bado.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuliomo humu tuliotulia hivi sasa na nadhani ndiyo tuliopiga kura ni Waheshimiwa 250. Wanaohesabu kura ni vijana wetu wale Makatibu wa Kamati *(Committee Clerks),* wako nyuma hapa hawawezi kuingia humu kwa utaratibu kwa sababu sasa ni Bunge. Ila pengine kwa kuhakikisha mambo ni sawa, labda tutafute miongoni mwetu Waheshimiwa wawili wakashuhudie tu zinavyohesabiwa. Mnaafiki hilo?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Mapendekezo? Sasa 251 siyo 250, tumekuwa 251. Mheshimiwa Lotto na Mheshimiwa Mbunge wa Kigoma Mjini, Serukamba.

**WABUNGE FULANI:** *Gender.*

**SPIKA:** *Gender?*

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Niliona wagombea wote ni wanaume sasa nikasema...

Mheshimiwa Grace Kiwelu, aende. Tukusanye kura sasa, kura zikusanywe, onyesheni kwamba masanduku ni matupu.

*(Hapa masanduku matupu ya kukusanyia kura yalionyeshwa kwa Waheshimiwa Wabunge na kura zilianza kukusanywa)*

**WABUNGE FULANI:** Bado hatujapata karatasi.

**SPIKA:** Hamjapata karatasi za kupigia kura?

**MBUNGE FULANI:** Wawili wameongezeka.

**SPIKA:** Wawili, wawili. Kwa hiyo, 253 sasa. Pale Mheshimiwa Mbunge wa Mtera Mzee John Malecela pia.

**WABUNGE FULANI:** Wameongezeka wengine.

**SPIKA:** Wangapi hao?

**WABUNGE FULANI:** Wameongezeka wanne.

**SPIKA:** Wanne! Wamekuwa 255. Ooh, Mheshimiwa Dorah Mushi anaingia. Daah, 256. Mheshimiwa Mushi umepiga kura au bado?

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Bado Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Bado, mpeni karatasi Mheshimiwa Dorah Mushi. Mzee John Malecela pale hajapata karatasi.

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli nimechelewa, lakini nimekuta wenzangu wameniwekea. Kwa hiyo, nimepiga kura, isije ikaleta matatizo ya hesabu. Nimeona niwe mkweli. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana kwa taarifa hiyo. Katibu, mzingatie hilo.

Kwa hiyo, Katibu 255 eeh. Kusanyeni kura ya Mheshimiwa Dorah Mushi pale. Mheshimiwa Mzee Kingunge Ngombale-Mwiru, anaingia, kwa hiyo 258. Aah, Mheshimiwa Zabein Mhita, looh. Sasa nadhani ni 259. Jamani kura zote zimekusanywa? *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Tayari eeh. Kuna moja nyingine tena!

Aaah, Mheshimiwa Athumani Janguo, 260. Mpeni karatasi tumalize jamani. Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, 261. Mpeni karatasi. Wanaoingia wapeni basi. Aah, hapana hiyo siyo ziada, tunarudi pale pale 260. Alikwenda kupiga simu huyo. Tayari zote zimekusanywa?

**WABUNGE FULANI:** Bado.

**SPIKA:** Katibu, tuingie hatua ya pili. Nawaomba Mheshimiwa Sameer Lotto na Mheshimiwa Grace Kiwelu, mfuatane na masanduku ya kura na vijana, mtawakuta *Committee Clerks* kule ndani ambao wanafanya zoezi la kuhesabu.

## UCHAGUZI WA WAJUMBE WA BARAZA LA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

**ND. DAMIAN S. L . FOKA - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, sasa tunaingia katika uchaguzi wa Wajumbe wa Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *(University of Dar es Salaam).*

Kwa mujibu wa sheria namba 12 ya mwaka 1970 iliyoanzisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam inatamka kuwa Baraza litaundwa pia na Wajumbe watatu kutoka Bunge la Tanzania. Kwa mantiki hiyo, leo tarehe ya 16 Februari, 2006 wagombea watatu wa nafasi hiyo mtawasikiliza na hatimaye kuwapigia kura.

Wa kwanza ni mwakilishi toka Kambi ya Upinzani, wawili ni wawakilishi toka Chama Tawala. Majina niliyopokea ni kama ifuatavyo, kutoka Chama cha Upinzani yupo Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo wa CHADEMA na kutoka Chama Tawala ni Mheshimiwa Ruth Msafiri, wa pili ni Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, wa tatu ni Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji na wa nne ni Mheshimiwa Profesa Feethan Filipo Banyikwa. Hao ndiyo wagombea ambao nimepokea kwa ajili ya kugombea nafasi hiyo.

**SPIKA:** Naomba Mheshimiwa Susan Lyimo, abaki, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji na Mheshimiwa Prof. Feethan Banyikwa, watoke nje wataitwa.

*(Hapa Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Prof. Raphel Mwalyosi, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji na Mheshimiwa Prof. Feethan Banyikwa walitoka nje ya Ukumbi wa Bunge)*

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu utaratibu

**SPIKA:** Utaratibu.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, tunafanya uchaguzi na tumewateua wenzetu wawili waende wakahakiki kura kule. Wanapataje na wenyewe nafasi ya kutoa uamuzi wao kwa watakaojieleza hapa wakati wenyewe watakuwa hawapo?

**SPIKA:** Aah! Kuna ushauri mwingine?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Nadhani tuendelee, tutawaarifu kwa sababu wanawafahamu wanaogombea. Wao watapelekewa karatasi ya kupiga kura. *(Makofi)*

Sasa namwita Mheshimiwa Susan Lyimo, dakika tatu na wajumbe wanaweza wakauliza maswali yasiyozidi matatu.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Kwa kuwa nafasi ya upinzani ni moja tu na hakuna mtu mwingine anayegombea naye. Kama wa upinzani wangekuwa ni

wawili wangepigiwa kura, lakini kwa sababu ni mmoja tu hakuna sababu ya kupiga kura. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed anasema kwamba, kwenye Kambi ya Upinzani mgombea ni mmoja na hakushindana na mwingine yeyote, kwa hiyo, yeye anadhani kwamba huyo anakuwa amepita kama mwakilishi, lakini sijui Katibu, Katiba yao hawa inasemaje? *(Makofi)*

**ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kiutaratibu ni kwamba kama anakuwa mmoja anapita bila kupingwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mmeyasikia hayo.

**WABUNGE FULANI:** Sawa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, tunaafiki Mheshimiwa Susan Lyimo ...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, tunaomba aje mbele tumuone. *(Makofi)*

*(Hapa Mhe. Susan Lyimo alikwenda mbele ya Ukumbi kwa ajili ya kujitambulisha)*

**SPIKA:** Wasalimie basi.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Wabunge wenzangu, nawashukuru sana kwa kunipitisha bila kupingwa. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa aitwe Mheshimiwa Ruth Msafiri.

*(Hapa Mheshimiwa Ruth Msafiri aliingia ndani ya Ukumbi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Naibu Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa heshima na taadhima naomba nijitambulishe kuwa ni Ruth Blasio Msafiri, Mbunge wa Jimbo la Muleba Kaskazini, kwa kipindi cha pili.

Kipindi kilichopita nilikuwa Mjumbe wa Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, uwakilishi ambao mlinipa ninyi wenyewe. Hata hivyo katika uchaguzi huu, mimi nagombea nafasi ya *SADC Parliamentary Forum* na nimekampeni kwa nafasi hiyo kwa sababu ningependa kuwa mwalikilishi wa Bunge hili katika Bunge hilo. Kwa heshima na unyenyekevu na kwa kuwa nafasi tulizobaki nazo kwa Chama cha Mapinduzi ni mbili nilikuwa naomba msinipigie kura katika ujumbe wa Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili wenzangu waliobaki muweze kuwachagua. Ahsanteni sana. Naomba mimi mnifikirie kwa ajili ya *SADC* ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, kwa hiyo, hakuna haja ya maswali maana yake amejitoa yeye. Kwa hiyo, tumebaki na wagombea sasa watatu. Aitwe Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi. *(Makofi)*

*(Hapa Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi aliitwa na kuingia ndani ya Ukumbi)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika na ndugu zangu Wabunge, mimi naitwa Raphael Benedict Mwalyosi, kwa miaka zaidi ya 20 iliyopita nilikuwa Mtafiti au Mhadhiri, Mtafiti Mwandamizi au Mhadhiri Mwandamizi kwa miaka yote hiyo. Lakini kwa miaka sita iliyopita nilikuwa nashika nafasi ya ngazi ya juu pale Chuoni nikiwa kama Mkurugenzi wa Taasisi ya Kutathmini Rasilimali. Kwa hiyo, nakifahamu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinavyofanya kazi, taratibu zake na sheria zake. Kwa hiyo, mkiniruhusu niende, nitawawakilisha vizuri, naombeni kura zenu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali.

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Mwalyosi, aitwe Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji.

*(Hapa Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji aliitwa na kuingia ndani ya Ukumbi)*

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, niliyesimama hapa mbele yenu ni Dr. Haji Mwita Haji, Mbunge wa Jimbo la Muyuni, Zanzibar. Nina heshima kubwa kwenu kusimama mbele kujieleza kwamba katika kipindi kilichopita mlinichagua hapa kwa kura nyingi ili kukiwakilisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kipindi kilichopita. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima kubwa mara hii nimekuja mbele yenu, lakini kwa bahati njema imetokea na nafasi ya Bunge la Afrika na niliziomba nafasi hizi mbili. Kwa hiyo, kwa heshima na taadhima Waheshimiwa Wabunge, naomba sana mniwie radhi kwa nafasi hii ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam msinipigie kura na muweke kura zenu wakati wa Bunge la Afrika kwa ile nafasi ya Zanzibar. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mwongozo wa Spika.

Mheshimiwa Spika, waliobaki sasa hivi ni wagombea wawili na CCM nafasi zao ni mbili labda kiti kituongoze iko haja ya kupiga kura tena?

**WABUNGE FULANI:** Hamna.

*(Hapa Mheshimiwa Prof. Feethan Banyikwa aliitwa na kuingia ndani ya Ukumbi)*

**MHE. PROF. FEETHAN F. BANYIKWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa makofi yenu.

**WABUNGE FULANI:** Angalau basi tumuone huyu mgombea mwingine.

**SPIKA:** Subiri kwanza, wewe una bahati, walichotaka ni kukuona tu hakuna zaidi. Kwa kuwa majina ni mawili hatuna haja ya kupiga kura. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, wawakilishi wetu huko ni Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi na Mheshimiwa Profesa Feethan Banyikwa. Katibu tunaendelea na Chuo cha Sokoine Kilimo *(SUA). (Makofi)*

**UCHAGUZI WA WAJUMBE WA BARAZA LA CHUO KIKUU CHA SOKOINE KILIMO *(SUA)***

**ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE:** Kwa mujibu wa Kifungu cha 13 (1) (m) cha sheria ya mwaka 1984 Bunge huteua Wabunge watatu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa wajumbe wa Baraza la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. Kwa mantiki hii, leo tarehe 16 Februari, 2006 wagombea hao wa nafasi hizo watatu mtawasikiliza na hatimaye kuwapigia kura kwa utaratibu ufuatao:-

Utaratibu wake ni sawa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, nafasi ni tatu, moja inachukuliwa na mwakilishi kutoka Kambi ya Upinzani na mbili toka wawakilishi toka Chama Tawala. Wagombea ni hawa wafuatao:-

Kutoka Kambi ya Upinzani ni Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe, kutoka Chama Tawala ni hawa wafuatao, Mheshimiwa Dr. Mzeru Omar Nibuka, Mheshimiwa Dr. James Mnanka Wanyancha, Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama na Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo. Hao ndiyo wagombea wa nafasi hiyo na kama tulivyokubaliana watatoka nje wakati mwenzao wa kwanza anajieleza na kila mmoja atapewa nafasi ya dakika tatu na baadaye kuulizwa maswali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Hayo uliyoyasema yanahusu wale Wabunge wa CCM peke yao. Kwa upande wa Kambi ya Upinzani, ningemuomba Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe, asimame hapa tuweze kumuona. Mheshimiwa Wangwe nakuruhusu usalimie tu maana yake wewe umekwishapita. (*Makofi/Kicheko)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge wote, nashukuru sana kwa kunipitisha bila kupingwa. *(Makofi)*

*(Hapa Mheshimiwa Dr. Mzeru Omar Nibuka aliitwa na kuingia ndani ya Ukumbi)*

**WABUNGE FULANI:** Simama basi! *(Kicheko)*

**MHE. DR. MZERU O. NIBUKA:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wote mimi niliyesimama mbele yenu hapa naitwa Dr. Mzeru Omar Nibuka, Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini. Kwa heshima na taadhima na unyenyekevu mkubwa kabisa naomba mnipe kura zenu zote za ndiyo kwa sababu zifuatazo:-

Sababu kwanza uwezo ninao, lakini ya pili Chuo cha Sokoine kipo ndani ya Jimbo langu na wao ndiyo wapiga kura wangu. Kwa hiyo, mwisho nawakaribisha Wabunge wote Morogoro, karibuni sana. Naomba kura zenu zote za ndiyo kwa unyenyekevu mkubwa. Shikamoni wazee. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Maswali.

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Dr. Mzeru. Aitwe Mheshimiwa Dr. James Wanyancha.

*(Hapa Mheshimiwa Dr. James Wanyancha aliitwa na kuingia ndani ya Ukumbi)*

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge, aliyesimama hapa ni Dr. James Wanyancha, Mbunge wa Jimbo la Serengeti.

Ukweli nilikuwa nimewania kuwania kuwakilisha Chuo Kikuu, lakini kwa sababu nawania Bunge la Afrika, siyo vizuri tena niwanie nafasi hii. Kwa hiyo, natoa nafasi kwa wenzangu na wenyewe waweze kugombea cheo hiki. Kwa hiyo, naomba kwa heshima na taadhima kujitoa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, ahsante sana. Aitwe Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama.

*(Hapa Mheshimiwa Castor Ligallama aliitwa na kuingia ndani ya Ukumbi)*

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, niliyesimama mbele yenu naitwa Castor Ligallama, Mbunge wa Kilombero, Mkoa wa Morogoro.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nafasi hii ya kuwakilisha Bunge katika Chuo cha Sokoine. Mimi ni *Retired Development Banker* na naomba nitumie uzoefu wangu wa miaka 22 katika Taasisi ya Benki katika Chuo cha Kilimo. Naomba kura zenu. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali.

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Castor Ligallama. Aitwe Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo. *(Makofi)*

*(Hapa Mheshimiwa Gaudence Kayombo aliitwa na kuingia ndani ya Ukumbi)*

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wenzangu Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi, inaelekeza Serikali kuleta *modernization* ya kilimo. *SUA* ni Chuo Kikuu cha Kilimo. Rais wetu ameelekeza Serikali yake ihakikishe mafanikio ya Awamu ya Tatu ya kiuchumi yatafsiriwe sasa na Awamu ya Nne katika mifuko ya wananchi. Kwa awamu hii ya Rais wetu ya kuhakikisha kwamba yale mafanikio yanatafsiriwa mifukoni mwa wananchi na mimi nina hamu hiyo hiyo ya kutafsiri tafiti zinazofanywa na Chuo Kikuu cha Kilimo kwa wananchi wetu na kwa Wabunge wetu. Hili ni jambo la dharura kwa sababu tunayo miaka mitano tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima sasa niruhusu nikuombe kura wewe, Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri pamoja na Wabunge wenzangu. Mimi ni Gaudence Cassian Kayombo, kwa taaluma ni mchumi na *banker* kwa miaka 27. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali.

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Gaudence Kayombo.

Karatasi za kura zigawiwe. Naomba nikumbushe Waheshimiwa Wabunge, ifuatavyo, kura unazopiga sasa ni mbili, majina ya kupigiwa kura ni Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama na Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, usipigie kwa Mheshimiwa Dr. James Wanyancha ambaye amejitoa. Kwa hiyo, ni majina matatu Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Castor Ligallama na Mheshimiwa Gaudence Kayombo, hata kama majina mtayaona ni zaidi ya hapo hatukutarajia kwamba wengine watakuwa wamejitoa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika karatasi hii inasema kwamba hapa chini weka alama ya “V” kwa mgombea mmoja tu kwenye chumba kilichowazi ya mbele ya jina unalochagua. Hayo ni maelekezo ya karatasi yako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Yamekosewa. Ni wawili. Sote tumepata karatasi za kura?

**WABUNGE FULANI:** Bado.

**SPIKA:** Naomba wanyooshe mkono wale ambao bado. Loo! Vijana tufanye haraka kidogo. Pale bado karatasi.

Nadhani sasa sote tumepata karatasi, ambaye bado hajapata anyooshe mkono tafadhali. Tayari. Piga kura mbili dhidi ya majina mawili unayochagua weka alama ya vema. Ukiweka tatu kura yako itakuwa imeharibika, ukiweka moja imeharibika. Sote tumepiga kura?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Haya vijana mkusanye hizo karatasi. Kuhusu utaratibu Mheshimiwa William Lukuvi.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba radhi nilichelewa lakini nimeongezeka nimepiga kura moja.

**SPIKA:** Kwa hiyo, sasa idadi ni 266. Mheshimiwa Waziri umehesabiwa tayari.

**MHE. TEDDY L. KASELA-BANTU:** Mheshimiwa Spika na mimi nilichelewa samahani. Nilichelewa lakini nimepiga kura sasa hivi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mnapoingia tu kuna kijana anawahesabu na analeta hapa idadi. Kwa hiyo, kila mtu anahesabiwa. Kwa hiyo, wote tumepiga kura?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Katibu tunakwenda hatua ya nne. Chuo Kikuu Huria.

**ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE:** Uchaguzi wa Wajumbe wa Baraza la Chuo Kikuu Huria.

Kwa mujibu wa sheria iliyoanzisha Chuo Kikuu Huria Na. 17 ya mwaka 1992 iliyorekebishwa na sheria Na. 18 ya mwaka 1995 Baraza hilo linaundwa na wajumbe 3 wanaochaguliwa kutoka Bunge la Tanzania.

MheshimiwaSpika, kwa mantiki hiyo, leo hii tarehe 16 Februari, 2006 wagombea watatu wa nafasi hiyo watasikilizwa na hatimaye mtawapigia kura. Nafasi hizo ni kama ifuatavyo:-

Nafasi moja ni kwa mwakilishi toka Kambi ya Upinzani na nafasi mbili kama ilivyotangulia na kwa wawakilishi wa kutoka Chama Tawala. Waliojaza fomu za kugombea nafasi hizo ni hawa wafuatao, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo, Mheshimiwa Benson Mpesya na kutoka Kambi ya Upinzani ni Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali. Utaratibu tutakaofuata ni kama tulivyokuwa tumekubaliana hapo mwanzo. Ahsante.

**SPIKA:** Naomba tumuone Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali.

Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, wewe umekwishapita kutoka Kambi ya Upinzani kwa hiyo, unaweza kusalimia tu. *(Makofi)*

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge, niliyesimama mbele yenu ni Dr. Ali Tarab Ali, Mbunge wa Jimbo la Konde, kwa miaka 15 nimekuwa ni mwalimu *Muhimbili University College of Health Sciences* na sasa nitatumikia kwenye Bunge lako Tukufu kama mwakilishi kwenye Chuo Kiku Huria cha Tanzania. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali. Mheshimiwa Naibu Spika, naona ana *agenda* maalum. Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo abaki, atoke Mheshimiwa Beatrice Shellukindo na Mheshimiwa Benson Mpesya.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge, habarini za mchana.

Waheshimiwa Wabunge, mimi naitwa Juma Abdallah Njwayo Mbunge wa Tandahimba, Mkoa wa Mtwara. Naomba mnichague ili niwawakilishe katika nafasi ya Bodi ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Waheshimiwa Wabunge, mimi *degree* yangu ya kwanza ya sheria niliipatia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Kwa hiyo, nina uzoefu wa kujua matatizo mengi yaliyopo pale. Natumaini mkinipa nafasi hii nitawawakilisha Watanzania vizuri sana. Nawaomba kura zenu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali.

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Njwayo. Aitwe Mheshimiwa Beatrice Shellukindo. *(Makofi)*

*(Hapa Mheshimiwa Beatrice Shellukindo aliitwa na kuingia ndani ya Ukumbi)*

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge wenzangu itifaki imezingatiwa. Niliyesimama hapa mbele naitwa Beatrice, mtoto wa Matumbo na mke wa Shellukindo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nimeamua kujitoa lakini baada ya kuona ni wanaume watupu, nikasema sina sababu ya kujitoa. Pamoja na maelezo yangu mliyoyaona, nimepata bahati ya kufanya kazi Wizara ya Sayansi na Elimu ya Juu kwa miaka sita, nilishughulikia masuala mbalimbali ya kiutawala, ya wakufunzi na wanafunzi. Nimefanya kazi utumishi najua sheria za kazi na mambo mengine mengi. Kwa hiyo, naomba kura zenu ahsanteni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali.

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Beatrice Shellukindo.

*(Hapa Mheshimiwa Benson Mpesya aliitwa na kuingia ndani ya Ukumbi)*

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, nasimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa unyenyekevu na adabu nyingi kutoka sakafu ya moyo wangu ili Mheshimiwa Spika, nikuombe kura yako, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge, mimi ndiye Benson Mwailugula Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge, mimi ndiye mwanafunzi wa kwanza wa Chuo Kikuu Huria niliyevunja rekodi ya kusoma kwa kipindi cha miaka minne badala ya miaka sita. Kwa njia hiyo, nimekuwa ni chachu. Mimi ni ufagio wa zamani ninaostahili kurudishwa, ninayezijua kona zote za nyumba ile ya Chuo Kikuu Huria. Kwa heshima na taadhima Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kura zenu niwajengee heshima tena ya Chuo Kikuu Huria. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mpesya. Karatasi za kura! Haraka, haraka karatasi za kura jamani.

Nakumbusha tena wanaopigiwa kura ni hawa wafuatao, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo na Mheshimiwa Benson Mpesya, kati ya hao watatu unachagua wawili baina ya watatu.

Waheshimiwa Wabunge, nani hawajapata karatasi za kura wanyooshe vidole ili waonekane. Mmoja pale katikati upande wa kushoto. Sote tumepata karatasi ya kura?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Basi masanduku ya kukusanyia kura. Haya kusanyeni kura sasa.Kuna kura ambazo hazijakusanywa? Moja ile pale, Mheshimiwa Mwimchoum Msomi. Pale mwisho pale kuna kura mbili zile.

Katibu naona tayari twende kwenye kundi la tano sasa. Chuo Kikuu cha Mzumbe.

## UCHAGUZI WA WAJUMBE WA BARAZA LA CHUO KIKUU CHA MZUMBE *(MU)*

**ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE:** Uchaguzi wa Wajumbe wa Baraza la Chuo Kikuu cha Mzumbe. Kwa mujibu wa Sheria iliyoanzisha Chuo Kikuu cha Mzumbe *(The Mzumbe University Act, No. 21 of 2001)* Kifungu cha 14(j) kinatamka kwamba Bunge litakuwa na Mjumbe mmoja atakayewakilisha kwenye Baraza la Chuo hicho. Naomba kutoa taarifa kuwa nimepokea jina la mgombea mmoja tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huyo ni Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Godfrey Zambi, tunaomba uje mbele hapa tukuone. *(Makofi)*

Mheshimiwa Godfrey Zambi, unaombwa utusalimie.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, niliyesimama mbele yenu ndiyo naitwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Jimbo la Mbozi Mashariki. Kwa wale waliokuwepo Bungeni kipindi lilichopita cha mwaka 2000 hadi 2005 lile Jimbo lilikuwa chini ya Mheshimiwa Edson Halinga na nilisikia mlikuwa mnamwita Mwenyekiti wa Wanaume Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba tu nichukue nafasi hii kuwashukuru sana kwa kuniunga mkono na kwamba hakuna mwingine aliyejitokeza, kwa maana hiyo kuwapunguzia usumbufu wa kupiga kura. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea kundi lingine. Wagombea wa *SADC Parliamentary Forum.*

## UCHAGUZI WA WAJUMBE WA *SADC PARLIAMENTARY FORUM*

**ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE:** Uchaguzi wa Wajumbe wa Uwakilishi *SADC Parliamentary Forum.* Kwa mujibu wa Ibara ya 6 ya Katiba ya Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika yaani *SADC PF,* inatamka kuwa kila nchi mwanachama itawakilishwa na Mwenyekiti na wajumbe wengine wanne watakaochaguliwa na Bunge.

Katika Wajumbe wanne wa kuchaguliwa mmoja lazima awe Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake kama vile *Tanzania Women Parliamentary Group.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo nafasi zilizopo ni tatu ambazo leo hii wagombea wake watasikilizwa na kupigiwa kura kama ifuatavyo:-

Tutakuwa na nafasi moja ya mwakilishi toka Kambi ya Upinzani. Nafasi mbili ni kwa ajili ya Mjumbe mwingine yeyote. Majina ambayo nimepokea ya wagombea ni haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Dr. Lucy Sawere Nkya, Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mheshimiwa Richard Said Nyaulawa na Mheshimiwa Halima Mamuya. Kutoka Kambi ya Upinzani ni Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutazingatia utaratibu kama ule uliotangulia. Ahsante.

**SPIKA:** Kwa utaratibu huo ningemwita Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, kama angekuwepo humu ndani, lakini hayupo. Basi namtangaza kwamba yeye ndiyo amepita kuiwakilisha Kambi ya Upinzani katika *SADC Parliamentary Forum. (Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, aliniachia barua angalau ya kumsemea basi nataka kuchukua nafasi hii kulishukuru Bunge hili kuwa amechaguliwa bila kupingwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, shukrani zimepokelewa. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge waliotajwa sijui mngependa Mheshimiwa Ruth Msafiri, ajieleze tena?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Ndiyo eeh! Haya Mheshimiwa Ruth Msafiri, uje wakati huo huo Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Richard Nyaulawa na Mheshimiwa Halima Mamuya, mtoke nje. Mheshimiwa Ruth Msafiri, unatakiwa kujieleza. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** *Honourable Speaker, Honourable Ministers, Honourable Deputy Ministers, Honourable colleagues members of Parliament. My name is Ruth Blasio Msafiri. I am a Member of Parliament from Muleba North Constituency for the second term. (Applauses)*

*Honourable Speaker, it is the great honour today that I present myself as a candidate for SADC Parliamentary Forum. (Applauses)*

*My long experience within the ruling party, Parliament and my academic qualifications I would assist that allow me to perform the responsibilities of furthering the property growth of SADC Parliamentary Forum in Tanzania. I am interested in this organization.*

*Honourable Speaker, Honourable Members of Parliament, humbly requesting your voice to be your representative in the SADC Parliamentary Forum. Thank you. (Applauses)*

**SPIKA:** Kuna swali?

**MBUNGE FULANI:** Hamna.

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Msafiri.Aitwe sasa Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya. *(Makofi)*

*(Hapa Mheshimiwa Stella Manyanya aliitwa na kuingia ndani ya Ukumbi)*

**MHE. STELLA M. MANYANYA:** *Thank you Honourable Speaker, Honourable Secretary and my fellow members of Parliament. Standing before you I am Engineer Stella Martin Manyanya. I am forty three years old. I have two profession electrical engineering and entrepreneurship and enterprise development skills.*

*Kindly, I would like to request you to elect me to represent you in the SADC Parliamentary Forum. (Applauses)*

*I am familiar with Tanzanian political and business environment and a woman been an engine for economic growth. I believe I will represent you in a positive way. Please I request again, vote for me. You are the best, I love you all. (Laughter/Applauses)*

**SPIKA:** *Any questions?*

**WABUNGE FULANI:** *No.*

**SPIKA:** Maswali?

**WABUNGE FULANI:** Hamna.

**SPIKA:** Ahsante *Engineer* Stella Manyanya. Aitwe Mheshimiwa Dr. Lucy Sawere Nkya. *(Makofi)*

*(Hapa Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya aliitwa na kuingia ndani ya Ukumbi)*

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Naibu Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge wenzangu. *Asalaam aleykum.*

**WABUNGE FULANI:** *Waaleykum salaam.*

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mimi naitwa Dr. Lucy Sawere Nkya, mimi nazungumza Kiswahili. Kiingereza nakijua, nina *Masters Degree* mbili. Mimi nimesimama mbele yenu Waheshimiwa Wabunge, ninaomba mnichague niweze kuwawakilisha katika Bunge la *SADC.*

Mimi uwezo wa kuwawakilisha ninao, kwa sababu mimi kuanzia mwaka 1990 nilikuwa mwasisi wa shirika moja ambalo linatoa ufadhili wote wa UKIMWI, *Tanzania* na *Southern African Region* linaitwa *Southern African Aids Trust. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hilo shirika lilikuwa nalazimika kwenda kwenye Bunge la Canada kila baada ya miaka miwili kwenda kuzungumza na kujenga hoja kwa nini fedha za UKIMWI zije Kusini mwa Afrika. Nilifanikiwa mara nyingi kwa muda wa miaka 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu ninaomba kura zenu niweze kuwawakilisha. Mimi nitawawakilisha kwa uadilifu na uaminifu. Nitafanyakazi kwa bidii nihakikishe kwamba ushirikiano unaotakiwa kuwa kati ya Mabunge yetu unaleta tija kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Kwa heshima na taadhima Waheshimiwa Wabunge wenzangu naomba kura zenu, kwa heshima na taadhima Mheshimiwa Spika, naomba kura yako, kwa heshima na taadhima Waziri Mkuu naomba kura yako. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali?

**WABUNGE FULANI:** Hamna.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dr. Nkya.

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Nawashukuruni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa nadhani tumalize na hawa Waheshimiwa Wabunge wa jinsia moja. Mheshimiwa Halima Mamuya.

*(Hapa Mheshimiwa Halima Mamuya aliitwa na kuingia ndani ya Ukumbi)*

**MHE. HALIMA M. MAMUYA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwa sababu sina nia ya kuomba mnipigie kura. Ninaomba niendelee kuzungumza kwa Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, mimi nilichukua fomu ya kuomba Ubunge huu kuwakilisha Bunge hili katika *SADC.* Lakini baada ya kutazama majina ya wenzangu waliogombea pamoja nami na kwa sababu mimi ni kiongozi wa Umoja wa Wanawake wa Tanzania. Wenzangu wote walioko katika karatasi hii hawana nafasi zingine za uwakilishi zaidi yangu. Mimi ninawakilisha vile vile Wabunge wa Mkoa wa Arusha katika *ALART.*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaamini sana katika kugawana nafasi za uwakilishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Wabunge wenzangu ninawaomba sana wanawake waliobaki wachaguliwe angalau mmoja wao ili asindikizane na wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuruni nyote. Ahsanteni . *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimefafanuliwa hapa na sekretarieti kwamba uwakilishi ni wa kijinsia kumbe. Kwa hiyo, itabidi ipigwe kura moja kwa kundi la wanawake na kura moja kwa kundi la wanaume. Sasa kwa bahati nilikwishamaliza orodha ya wanawake. Kwa hiyo, sasa zitagawiwa kura ili tumpigie mmoja kati ya wale watatu. Nafasi zilizobaki Waheshimiwa Wabunge ni mbili, moja ya mwanamme na moja ya mwanamke. Ile ya upinzani imekwishakwenda. Sasa waliojieleza mbele yetu ukiacha Mheshimiwa Halima Mamuya ambaye amejitoa ni Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya na Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya. Hapo unachagua mmoja. Karatasi? Wajieleze kwanza? Wanaume wajieleze kabisa. Haya, tunawaita sasa Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro. *(Makofi)*

*(Hapa Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro aliitwa na kuingia ndani ya Ukumbi)*

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwa heshima na taadhima ninasimama mbele yenu mimi Mbaruk Kassim Mwandoro, nikiomba mnipe kura zenu kwa nafasi ya *SADC PF,* ili niwe mwakilishi wenu.

Kutokana na uzoefu wangu wa miaka mingi katika Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na taasisi zake nilibahatika kupata fursa ya kufanya mambo mengi yanayohusiana na ushirikiano wa Kimataifa pamoja na *SADC.* Vile vile muda mrefu nilibahatika kuwa Mwenyekiti na Mjumbe wa Chuo cha Diplomasia. Kutokana na uzoefu huo na kutokana na uzoefu wangu nilioupata Bungeni kwa kipindi kilichopita nina imani kubwa mkinipa fursa hii nitaweza kuwatumikia kwa uadilifu na ukamilifu. Kwa heshima na taadhima naomba mnipe kura zenu zote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali Waheshimiwa Wabunge?

**WABUNGE FULANI:** Hamna.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, sasa Mheshimiwa Richard Nyaulawa. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD S. NYAULAWA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwanza ningeomba niwajulishe kwamba sasa hivi nimesimama siyo kwamba nimekaa. *(Makofi/ Kicheko)*

Akinamama shikamoni, akina baba shikamoni. Mimi nimekuwa mfanyabiashara kwa zaidi ya miaka 20. Naitwa Richard Said Nyaulawa, ni Mbunge wa Mbeya Vijijini.

Nina imani kwamba nina uzoefu, nina ujuzi, nina uwezo na nina nguvu ya kuweza kuwatumikia. Naomba kura zenu. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali

**WABUNGE FULANI:** Hamna.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nyaulawa. *(Makofi)*

Sasa zile karatasi za kwanza zigawiwe za kundi la wanawake ili tusizichanyange. Pitisheni *round* ya kwanza ya kura za wanawake. Mmoja kati ya hao watatu ukiacha jina la Mheshimiwa Halima Mamuya ambaye amejitoa, wale watatu unachagua mmoja vema moja.

Kuna ambaye hajapata karatasi Waheshimiwa Wabunge anyooshe mkono, wahudumu wamwone. Ambaye hajapata karatasi ya kura, pale kushoto kwa Spika. Sote tumepata karatasi za kupigia kura?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Mmepiga kura?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo

**SPIKA:** Vijana kusanyeni hizo kura. Nadhani Katibu unaweza kuanza kugawa zile za kundi la wanaume. Kwa sababu majina ni tofauti. Hapa pote mlipokusanya tuokoe muda. Sasa kundi la wanaume.

Waheshimiwa Wabunge, katika kundi hili majina ni mawili, Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro na Mheshimiwa Richard Said Nyaulawa. Unachagua mmoja. Karatasi za kundi la pili la wanaume, sote tumepata karatasi hiyo? Waheshimiwa ambao bado hawajapata karatasi wanyooshe mikono, sote tumepiga kura? Haya zikusanywe.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua inayofuata ni Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki na wagombea siyo Wabunge wa Bunge hili na kwa Kanuni zetu hawawezi kuruhusiwa kuingia humu hadi tutengue Kanuni ya 114. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kupitia Kanuni ya 124 atoe hoja ili tuweze kutengua Kanuni ya 114, waruhusiwe waingie tuwaone.

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI YA KURUHUSU WAGOMBEA AMBAO SIYO WA BUNGE KUINGIA NDANI YA BUNGE

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Kanuni ya 114 itenguliwe ili kuwapa nafasi wagombea ambao siyo Wabunge waweze kuingia ndani kuja kuomba kura. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

## UCHAGUZI WA WABUNGE WA BUNGE LA AFRIKA MASHARIKI

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja ya kutengua Kanuni ya 114 ambayo kwa kutengua hiyo Kanuni tutapata idhini ya kuwaingiza watu wasio Wabunge ndani ya ukumbi huu ili muwaone hawa wagombea imeamuliwa na kuafikiwa. Katibu waite wagombea wa Bunge la Afrika Mashariki.

**ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE:** Uchaguzi wa Wajumbe wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa mujibu wa Ibara ya 50 ya mkataba ulioanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki kila Bunge la nchi wanachama linapaswa kuchagua Wabunge tisa. Mwezi Novemba, 2001 Bunge hili lilichagua Wabunge tisa kwa ajili hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, itakumbukwa kuwa katika Uchaguzi Mkuu uliopita waliokuwa Wabunge wa Bunge hilo yaani Mheshimiwa Beatrice Shellukindo na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe waligombea katika uchaguzi huo na kuchaguliwa na sasa ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kutokana na hali hiyo nafasi ya Ubunge kwenye Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki zimebaki wazi na matokeo yake ni uchaguzi utakaofanyika hivi leo ili kujaza nafasi hizo. Chama cha Mapinduzi kimewateuwa wagombea wafuatao nao ni Dr. Norman A. Sigalla na Bibi Hulda Stanley Kibacha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa kama Katibu alivyosoma, majina hayo yanajaza nafasi mbili na kwa zote hawana wapinzani. (*Makofi*)

Katibu naomba waingie ili tuweze kuwaona. (*Makofi*)

*(Hapa Ndugu Hulda Kibacha na Ndugu Norman Sigalla waliitwa na kuingia ndani ya Ukumbi wa Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hawa ndio wagombea waliopitishwa na CCM kuingia katika Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki, mmoja anaitwa Dr. Norman Sigalla na mwingine ni Hulda Stanley Kibacha, sina haja ya kutambulisha yupi ni yupi kwa sababu kwa majina inaeleweka.

Waheshimiwa mmepewe nafasi hii kwa kweli baada ya kupitishwa ili muweze kuwasalimia Waheshimiwa Wabunge, nakuomba Mheshimiwa Hulda Stanley Kibacha, uje usalimie. *(Makofi)*

**ND. HULDA S. KIBACHA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge, awali ya yote kama ambavyo ametutambulisha Spika, mimi mnanifahamu ni Hulda Stanley Kibacha. Nichukue nafasi hii kuwapongezeni kwa dhati wote kwa pamoja, pia niwashukuru sana kwa kuweza kutupitisha tuweze kuwawakilisha katika Bunge la Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naahidi ushirikiano na uwakilishi ulio bora, naomba msiwe na wasiwasi wowote nitawawakilisha kwa kadri ya uwezo wangu. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**ND. NORMAN A. SIGALLA:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nirudie na mimi pia kuwashukuru kwa dhati kwa kuweza kutupitisha bila kupingwa, ninasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Nirudie kusema ninatambua nafasi ambayo mmetupa ya kwamba ni nafasi ambayo ninatakiwa niitumikie kwa ujasiri na kwa manufaa ya Taifa langu la Tanzania na kwa Afrika Mashariki, sitawaangusha. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana, nawaruhusu muweze kwenda huko Arusha, nafikiri Nairobi au Kampala. *(Makofi)*

Mmoja wa hawa Waheshimiwa nasikia ana ndugu yake humu humu ndani ya Bunge. *(Makofi/Kicheko)*

## UCHAGUZI WA WABUNGE WA BUNGE LA AFRIKA

**ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, tuna nafasi mbili za Ubunge wa Bunge la Afrika zilizo wazi. Kundi (b) ni Mbunge kutoka Zanzibar ambaye ni Mheshimiwa Omar Yusuf Mzee, aliyeteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Naibu Waziri na kundi (d) ni kundi kutoka Tanzania Bara ambapo Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mbunge aliyeteuliwa kuwa Waziri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, waliojitokeza kuchukua fomu walikuwa Wabunge watano, muda wa mwisho kurudisha fomu hizo ilikuwa ni jana tarehe 15 Februari, 2006 saa 10.00 jioni. Muda huo ulipofika Waheshimiwa Wabunge waliorudisha fomu walikuwa ni hawa watano ambao wameorodheshwa hapa.

Kutokana na maelezo hayo mafupi na kwa mujibu wa Kanuni za Bunge zinazohusika na uchaguzi wa Wabunge kuwasilisha katika Bunge la Afrika kila mgombea anatakiwa afike mbele ya Waheshimiwa Wabunge ajieleze na baadaye kuulizwa maswali kama tulivyokuwa tumekubaliana hapo mwanzo. Baada ya kujieleza karatasi za kupiga kura kama kawaida zitapitishwa na ninyi mtachukua hatua ambazo ni uamuzi wa kuchagua.

Mheshimiwa Spika, waliogombea ni hawa wafuatao Mheshimiwa Dr. James Mnanka Wanyancha, Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mbunge, Mheshimiwa William Jonathan Kusila na Mheshimiwa Omar Sheha Mussa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaratibu utakaofuata ni kama ulivyokuwa umetangulia kueleza.

**SPIKA:** Katibu, ni kura za makundi?

**ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE:** Hizi ni kura za makundi Zanzibar na Tanzania Bara.

**SPIKA:** Ndio, inavyotakiwa muwakilishi mmoja awe ni kutoka Zanzibar na mwingine kutoka Bara. (*Makofi*)

Sasa tutawaita kwanza wale wa Zanzibar.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** *Honourable Speaker, Honourable Prime Minister, Honorable dears, my colleague members of Parliament. Standing in front of you is the same person who was here few hours ago who are contested for the request to join the University of Dar es Salaam parts. For the benefit of others, he resigned or withdrew his name so that I could contest for this Pan-African Parliament.*

*Well, it is very clearly known that Swahili may also be used in this Parliament so I would kindly use Kiswahili.*

*(Hapa umeme ulikatika kwa muda na kurudi)*

**SPIKA:** Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa kuturejeshea umeme. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji anza upya.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima na tahadhima nina hakika kwamba ninaweza nikawawakilisha vizuri katika Bunge la Afrika. Kwa hiyo, bila ya kupoteza wakati kwa heshima na taadhima naomba kura zenu ili niweze kuwawakilisha katika hili Bunge la Afrika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali?

**WABUNGE FULANI:** Hamna.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dr. Mwita Haji. *(Makofi)*

*(Hapa Mheshimiwa Omar Sheha Mussa aliitwa na kuingia ndani ya Ukumbi)*

**MHE. OMAR SHEHA MUSSA:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mimi naitwa Omar Sheha Mussa, Mbunge wa Chumbuni. Nimesimama hapa ili kuomba nafasi ya uwakilishi kwenye Bunge la Afrika kundi la Zanzibar, elimu yangu nina Shahada ya kwanza ya mambo ya Uongozi niliyoipata Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1980 na vile vile nina Shahada ya pili kwenye mambo ya Fedha yaani *MA in Finance* kutoka Uingereza mwaka 1987.

Uzoefu wangu nimekuwa Kamishna wa Bajeti Hazina au Wizara ya Fedha kule Zanzibar kwa muda wa miaka saba na vile vile nimekuwa Katibu Mkuu Hazina kwa muda wa miaka 10. Zaidi ya hayo katika utumishi wangu huo nimekuwa mjumbe wa Bodi za Taasisi za Fedha hapa Tanzania kwa muda wa miaka 15 kama vile *LAPF,* naomba mnichague ili nimsaidie Rais wetu wa Bara la Afrika mama Balozi Dr. Getrude Mongella. Ahsanteni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Subiri kwanza, maswali?

**WABUNGE FULANI:** Hamna.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Omar Sheha Mussa. *(Makofi)*

Karatasi za kura? Basi tupige kura za Zanzibar kura moja, wagombea wa kundi la Zanzibar ni wawili ni Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji na Mheshimiwa Omar Sheha Mussa, unachagua mmoja.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, karatasi za kupigia kura zilizogaiwa sasa hivi zina watu wawili wanaogombania. Lakini bahati mbaya imeandikwa ndiyo na hapana, kwa hiyo, tunataka mwongozo wako asije mtu akaweka kwenye hapana ikawa kura mbele ya jina husika, kwa sababu kuna wengine wameshakosea wameshaweka kura kwenye hapana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mjitahidi kuwa upande wa jina linalohusika na vizuri iwe kwenye ndiyo, ndiyo unakubali lakini hata ikiwa kwenye hapana ili mradi ni mstari ule ule wa jina basi ni sahihi. *(Makofi)*

Waheshimiwa ambaye hajapata karatasi anyooshe mkono, wote tumepata nadhani tumeshapiga kura, vijana mkusanye.

Waheshimiwa, kundi la Bara tunao wagombea watatu Mheshimiwa Dr. James Mnanka Wanyancha, Mheshimiwa William Jonathan Kusila na Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama. Hao wawili watoke atatangulia Mheshimiwa Dr. James Mnanka Wanyancha kujieleza. *(Makofi)*

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge aliyesimama mbele yenu ni Dr. James Wanyancha, Mbunge wa Jimbo la Serengeti.

Kielimu nina Shahada tatu ikiwa moja nimepatia hapa nyumbani na nyingine Uingereza na nyingine Canada, kikazi nina uzoefu wa miaka 18 wa kufanya kazi nyumbani. Nina zaidi ya miaka 10 ambayo nilifanya kazi katika nchi za *SADC* kwanza nilienda Zimbabwe, nikaenda Zambia, nikaenda Lesotho. Kwa kufanya hivyo niliweza kujifunza namna ya kutetea maslahi ya nchi yako ukiwa katika Taasisi za Kimataifa.

Kwa heshima na taadhima ndugu zangu nipeni kura niweze kuwa mwakilishi katika Bunge la *SADC. (Makofi)*

**SPIKA:** Subiri kwanza, maswali?

**WABUNGE FULANI:** Hamna.

*(Hapa Mheshimiwa William Kusila aliitwa na kuingia ndani ya Ukumbi)*

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Waheshimiwa Wabunge, niliyesimama mbele yenu ndiye William Jonathan Kusila ni Mbunge wa Jimbo la Bahi, hiki kikiwa ni kipindi changu cha nne.

Nimesimama hapa kuwaomba kura zenu ili niwawakilishe katika Bunge la Afrika, muda ambao nimekaa ndani ya Bunge hili nina nafasi mbalimbali za uongozi ambazo nimebahatika kuzitumikia katika kipindi hiki, zimenijengea uelewa na uzoefu mkubwa katika kuchambua masuala mbalimbali ya Bara letu la Afrika, kwa hiyo, kuniwezesha kuwa mwakilishi wenu mzuri.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, naombeni kura zenu ili niweze kuwawakilisha katika chombo hiki muhimu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali?

**WABUNGE FULANI:** Hamna.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa William Kusila.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri nilipokuwa nimejaza nafasi mbili *ACP-EU* na hii ya Afrika nia yangu haikuwa kugombea nafasi zaidi ya moja, nilitarajia kwamba majibu yalikuwa yameshajulikana lakini kwa vile utaratibu mpaka kura zote ziishe, bado naomba muwapigie wenzangu wale wawili na ningeomba wale ambao wanataka kunipigia kura wazielekeze kwa Mheshimiwa James Wanyancha. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana, sina hakika kama utaratibu unaruhusu hili alilolifanya lakini ndiyo basi tena ndiyo maji yameshamwagika hivi sasa. Kwa hiyo, tutapata karatasi ya kupigia kura yenye majina matatu, jina la Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, mnaliacha kati ya yale majina miwili Mheshimiwa William Kusila na Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, mnapiga kura moja vema moja.

Ukipiga kwa Balozi Abdi Mshangama, yeye amekwisha jitoa kwa hiyo haina maana, karatasi.

Sote tumepata karatasi hiyo kundi la Bara? Alaa! Kwa Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, pale bado au imezidi hiyo, kuna karatasi ya ziada ile pale katikati na nyingine hapa. Hebu kusanya hiyo ya ziada.

Sasa tumekwisha piga kura sisi sote siyo? Haya kusanyeni kura basi. Wote tumekwisha piga kura?

## UCHAGUZI WA MAKAMISHNA WA TUME YA HUDUMA ZA BUNGE

**SPIKA:** Sasa tunaingia kundi la mwisho ambalo ndiyo kubwa sana, wagombea 16 kuchagua 5.

**ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE:** Uchaguzi wa Makamishna wa Tume ya Huduma za Bunge. Kwa mujibu wa sheria ya Tume ya Huduma za Bunge Namba 14 ya mwaka 1997 Tume inaundwa na Wajumbe 9 ambao kati yao 4 wanapatikana kwa nyadhifa zao, Wajumbe ni sita ni Naibu Spika, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulika na masuala ya Bunge na Katibu ni Katibu wa Bunge.

Wajumbe watano wanapatikana kwa kuchaguliwa kwa kuomba na kupigiwa kura na Wabunge kwa mantiki hiyo leo tarehe hii ya leo 16 Februari, 2006 wagombea watano wa nafasi hiyo mtawasikiliza kwa utaratibu ufuatao:-

Nafasi moja ni mwakilishi toka Kambi ya Upinzani, nafasi moja ni ya mwakilishi toka kundi la wanawake, Wajumbe wengine watatu watapatikana kutoka kundi lolote lile.

Mheshimiwa Spika, kama *Returning Officer* nimepokea *form* za wanaoomba kugombea nao wapo 16 nitawasoma wote kwa pamoja bila kutenganisha kundi kama ifuatavyo, heshimiwa John Magalle Shibuda, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo,...

*(Hapa umeme ulikatika kwa muda na kurudi)*

**ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Abdi Mshangama, Mheshimiwa Dr. Zainab Amir Gama, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa,

Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Abdulkarim Hassan Shah, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe na Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hao wote wamewekwa katika taratibu za makundi ambayo kwa jinsi watakavyopigiwa kura naomba tuzingatie utaratibu ambao tulikuwa tumekubaliana.

**SPIKA:** Napendekeza Waheshimiwa tuanze na kundi la wanawake, Katibu hebu tusomee sasa wagombea wanawake.

**NAIBU SPIKA:** Kuhusu utaratibu. Katika nafasi kama hii kwa upande wa upinzani hatuna matatizo, ya pili angalau mwanamke mmoja atapigiwa moja katika hii wanaobaki wanaungana na wale wanaume wengine halafu wanapigiwa wote watatu.

**SPIKA:** Sawa tutafika huko. Sasa ndiyo uchaguzi wote wa makundi wagombea ambao wametambuliwa katika makundi wana nafasi mbili ndiyo mantiki yao watapigiwa kwenye kundi lao na baada ya hapo watarudi kupigiwa kwa jumla. Siyo? Waheshimiwa mnasemaje kuhusu hili?

**WABUNGE FULANI:** Sawa!!

**SPIKA:** Tuanze na makundi, anayeshindwa kwenye kundi ndiyo ametoka. Tunaafikiana?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!!

**SPIKA:** Haya Katibu waite kundi la wanawake sasa, kwa hiyo mwanamke aliye Mzanzibari anaweza kuamua vipi sasa au hakuna kundi la Zanzibar?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Aha! Hapana basi. Mwanamke mpinzani, haya wanawake, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Estherina Kilasi na Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, wako watatu tu?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!!

**SPIKA:** Ooh! haya, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, abaki lakini Mheshimiwa Estherina Kilasi na Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe watusubiri. Karibu Mheshimiwa Dr. Zainab Gama.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mimi niliyesimama hapa naitwa Dr. Zainab Amir Gama, ni Mbunge, nina uzoefu ndani ya Bunge kwani nilikuwa kama Viti Maalum kwa awamu tatu sasa hivi ni Mbunge wa Jimbo.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama alivyosema Spika nichagulieni watu wasiokuwa na woga na mimi ni mmojawapo na watu wote wanajua sina woga, ninaomba ndugu zangu tushirikiane na ninyi kwamba hata hii sheria mkitaka ibadilike sasa hivi nashughulikia tu wafanyakazi, ndiyo. Baada ya kuisoma nimekuja kuigundua wafanyakazi lakini nia yetu ilikuwa na maslahi ya Wabunge kwa hiyo, tutashirikiana na ninyi kama tukikubaliana irudi pia ishughulikie maslahi ya Wabunge.

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu, Waziri Mkuu, Wabunge wenzangu wote naomba kura zenu, chonde ndugu zangu.

**SPIKA:** Maswali?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zainab A. Gama, aje sasa Mheshimiwa Estherina J. Kilasi.

*(Hapa Mheshimiwa Estherina Kilasi aliitwa na kuingia ndani ya Ukumbi)*

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Naibu Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, niko hapa mbele yenu kwa heshima na taadhima kubwa kuwaomba kura zenu zote ili niweze kuwa Kamishna wa Tume ya Huduma za Bunge, naombeni sana kura zenu.

Kwa jina naitwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Jimbo la Mbarali na hiki ni kipindi changu cha pili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa taaluma mimi ni Mhasibu nina Cheti cha *CPA II, CPA* ya Tanzania, nimeshawishika kabisa kuja kugombea nafasi hii na hasa baada ya kuwa na uzoefu wa muda mrefu. Kabla sijawa Mbunge nimefanya kazi hizo muda mrefu. Ninaombeni kura zenu zote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa subiri kidogo, Maswali?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna!

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Estherina Kilasi. Wa tatu ni Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe.

*(Hapa Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe aliitwa na kuingia ndani ya Ukumbi)*

**MHE. KIDAWA HAMID SALEHE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mwenzenu niliyesimama hapa naitwa Kidawa Hamid Salehe, Mbunge Viti Maalum Wanawake.

Mheshimiwa Spika, kielimu mimi ni mchumi na mwanamipango na nina *Master Degree* ya mambo hayo pia nina *Diploma* katika mambo ya Kodi kwa maana ya *Fiscal Studies.*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nimesimama hapa kwa dhumuni moja tu la kuomba kura zenu mniwezeshe kuwa mmoja kati ya Makamishna wa Tume wa Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bila kusema mengi naombeni kura zenu nyote, Waheshimiwa Wabunge wenzangu shikamooni, Mheshimiwa Spika shikamoo.

**WABUNGE FULANI:** Marahaba.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEHE:** Naomba kura zenu na niko tayari kuwatumikieni kwa nguvu zangu zote na mashirikiano mazuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali.

**WABUNGE FULANI:** Hakuna!

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Kidawa Salehe.

Haya tugawe karatasi kundi la wanawake, Waheshimiwa majina ni matatu Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Estherina Kilasi na Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe. Unachagua jina moja tu, kundi hili linatoa mshindi mmoja.

Waheshimiwa Wabunge, sote tumepata karatasi? Ooh! mikono pale katikati bado na mwisho upande wa kulia huku, viti vya nyuma upande wa kulia.

Naamini sasa wote tunazo karatasi na sina shaka tumeshapiga kura, ambaye hajapata karatasi anyooshe mkono. Hakuna, basi zikusanywe sasa.

Waheshimiwa tunaendela kundi la Upinzani Ndugu Katibu wagombea ni nani sasa?

**ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE:** Kundi la Upinzani wagombea ni Mheshimiwa Philemon Ndesamburo toka CHADEMA na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa kutoka Chama cha *CUF,* ni wawili tu kwa hiyo, naomba walivyojipanga hivi atajieleza kwanza Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa.

Kwa hiyo Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa utupishe kidogo, naomba tusikilizane.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mimi naitiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Jimbo la Moshi Mjini.

Mimi ni mzoefu nimekuwa Mbunge kwa miaka mitano na hii ni miaka mingine nakwenda mitano ijayo.

Mimi naomba kura zenu ili niweze kuwa Kamishna katika Tume ya Huduma za Bunge niweze kuwashughulikia wafanyakazi. *(Kicheko)*

**SPIKA:** *Order, Order.* Naomba utulivu.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Waheshimiwa Wabunge, si kuwashughulikia kwa ubaya ni kwa uzuri.

Wabunge wenzangu na Waheshimiwa naomba kura zenu ili niweze kufanya kazi yangu kama Kamishna wa Tume ya Huduma za Bunge. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna!

**SPIKA:** Maswali?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna!

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Philemon Ndesamburo.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Ahsante sana.

**SPIKA:** Aitwe Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa sasa.

*(Hapa Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa aliitwa na kuingia ndani ya Ukumbi)*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mimi jina langu ni Khalifa Suleiman Khalifa, nina hakika umelijua jina langu na utendaji wangu wa kazi katika Bunge hili.

Nimesimama hapa kuomba nafasi hii ya Ukamishna ili mimi na wenzangu tushirikiane pamoja na Serikali kuliweka Bunge letu katika *standard* inayotakiwa. Naomba kura zenu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali? Aah! Kuna maswali. Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Naomba nimuulize swali moja Mheshimiwa mgombea. Amesema anaomba nafasi hii aweze kutumikia Bunge hili na kuitumikia Serikali lakini taarifa nilizonazo ni kwamba Chama chake hakiitambui Serikali. Ni Serikali gani ambayo ataitumikia ambayo haitambui? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Aah! Lakini ni kulitumikia Bunge siyo kuitumikia Serikali.
Maswali?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna!

**SPIKA:** Haya gawa karatasi wagombea ni wawili tu. Sote tumepata karatasi ya kundi hili la Upinzani, wasiopata karatasi wanyooshe mikono. Tayari wote tumepata, basi anzeni kukusanya, kusanyeni karatasi.

Waheshimiwa Wabunge, sasa hivi ni saa moja na nusu, tumebakiza robo saa tu kufikia kipindi cha kuahirisha Bunge na nilikuwa nadhani ingekuwa vema angalau basi tumalize kuwasilikiliza na kupiga kura ili hata kama matokeo ni kesho basi sisi tukienda...

**WABUNGE FULANI:** Leo hii.

**SPIKA:** Leo hii hii enhee?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Basi hiyo inazidi kuimarisha hoja ambayo nataka kumwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi aitoe kwamba Bunge likae hadi baada ya muda wake kwa jioni hii hadi hapo tutakapomaliza kazi ya kupiga kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, karibu.

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI YA MUDA WA KUMALIZA BUNGE ILI BUNGE LIENDELEE NA SHUGHULI MPAKA ZITAKAPOKAMILIKA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Spika, kufuatana na Kifungu cha 21, Kanuni ya 21, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako liendelee na shughuli mpaka pale shughuli hizi zilizopo mbele yetu leo zimekwisha, lakini kufuatana na Kanuni isizidi nusu saa kuanzia saa mbili kasoro robo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba tuendelee. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Hoja ya kutengua Kanuni ya muda wa kumaliza shughuli za Bunge ilikubaliwa na Bunge)*

**SPIKA:** Tunaendelea na zoezi hili la kuwachagua wenzetu. Karatasi zote zimekusanywa?

**WABUNGE FULANI:** Ndio.

**SPIKA:** Sasa kwa Makamishna kundi la wote lililosalia sasa wapo kumi na moja, Mheshimiwa John Magale Shibuda, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Aggrey Mwanri. Kwa hiyo, abaki Mheshimiwa John Shibuda ambaye ataanza.

Sasa hawa ninaowataja sasa hivi watoke, Mheshimiwa Balozi Mshangama, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Leonard Mrope, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Abdulkarim Shah na Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa John Shibuda, aje kuanza. Jamani naomba utulivu ili tuwasikilize kwa haraka wagombea. Karibu Mheshimiwa John Shibuda.

**MHE. JOHN M. SHIBUDA:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, shikamooni. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge pamoja na maelezo yangu ya awali niliyotanguliza asubuhi, nasimama mbele yetu mimi Magale John Shibuda, Mbunge wa Jimbo la Maswa, kuomba kura zenu zote ili niweze kuwa Kamishna wa kushirikiana nanyi katika kufaulisha mahitaji ya Wabunge pamoja na watumishi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nakuombeni mjiandae kushirikiana na Tume hii kutujengea kasma ya kufaulisha utendaji wetu katika Majimbo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wana kazi ya kuchangia pale wanapohitajika kwenda kuhamasisha ujenzi. Waheshimiwa Wabunge msitu mpya, komba wapya. Naombeni kura zenu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa John Shibuda.

**MHE. JOHN M. SHIBUDA:** Shikamooni.
*(Hapa Mheshimiwa Abdi Mshangama aliitwa na kuingia ndani ya Ukumbi)*

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge, kwa wale ambao wamenisahau mimi ndio Balozi Abdi Hassan Mshangama, naomba nafasi hii ya Ukamishna ambayo kwa mujibu wa Sheria ya mwaka 1997 naona ina kazi kubwa tatu.

Kwanza, ni kuhakikisha kwamba huduma za Bunge ni za kisasa kabisa, pili maslahi ya watumishi wa Bunge na mwisho na muhimu zaidi maslahi ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeshawishika kuomba nafasi hii kwa sababu kwa uzoefu wangu wa miaka ishirini Wizara ya Fedha nina uzoefu na ujuzi wa kusaidia kujenga hoja ya kufikisha kwa Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa sheria ile kuhusu namna ya kuboresha vizuri zaidi huduma za Bunge na huduma za Wabunge. Kwa hiyo, naomba kura zenu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali Waheshimiwa Wabunge?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

*(Hapa Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud aliitwa na kuingia ndani ya Ukumbi)*

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Naibu Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, *asalaam aleykum.*

**WABUNGE FULANI:** *Waaleykum salaam.*

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Niliyesimama hapa naitwa Mohammed Rajab Soud, Mbunge wa Jang'ombe. Kilichonisimamisha hapa nataka kukutumikieni Wabunge wenzangu. Kwa heshima na taadhima naomba kura zenu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa jina naitwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Jimbo la Siha. Nimesimama hapa kuomba Ukamishna katika Tume ya Huduma za Bunge.

Mheshimiwa Spika, ulipokuja hapa ulileta kauli mbiu ambayo inasema kwamba, ni *standards na speeds* na Mheshimiwa Waziri Mkuu akatuongezea na *courage,* naamini tunachohitaji katika Tume yetu ni ujasiri na mimi nina hakika Waheshimiwa Wabunge mkinipa nafasi hiyo nitauwakilisha huu ujasiri. Naomba mnipe nafasi hiyo, Waheshimiwa Wabunge naomba kura zenu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali.

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sijui wenzetu wawili waliokwenda kusimamia kule sijui tuwaongeze wengine wawili kwa sababu ili kuharakisha na kuwasimamia vijana twende kwa haraka zaidi. Kwa hiyo, kama hiyo inakubalika basi huwa mnaniruhusu kuteua.

**WABUNGE FULANI:** Ndio.

**SPIKA:** Mheshimiwa Haroub Said Masoud na upande wa akinamama Mheshimiwa Diana Chilolo. Unaona tena wameshikana mikono hawa. *(Kicheko)*

Tunaendelea sasa aitwe Mheshimiwa Mgana Msindai.

*(Hapa Mheshimiwa Mgana Msindai aliitwa na kuingia ndani ya Ukumbi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa wapiga kura, mimi naitwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, kipindi changu cha tatu kuwa Bungeni na ni Kamishna mwanzilishi.

Kamisheni ya Bunge ilipoanza mimi nilikuwa miongoni mwa Makamishna na wenzangu wote hawapo, nimebaki mimi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mambo yote ya Kamisheni nayafahamu, nawaomba mnichague mimi na mimi uwezo wa kuwatumikia ninao na ninyi ni mashahidi, nawaomba kura zenu wote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Mawaziri pamoja na Naibu Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wenzangu nasimama hapa kwa kweli kuja kuwaomba kura ili nisaidie Tume yetu ya Huduma za Bunge kwa utaalam ambao ninao. *(Makofi)*

Mwaka 2000 niliombwa kugombea, lakini nikawaambia wenzangu hapana, lakini Bunge wamekuwa wakinitumia kama *freelance manager consultant* kwenye mambo yake na bado naendelea nayo, hata kuomba kura sikuwa na muda kwa sababu kuna mambo nilikuwa nayashughulikia na niliona niyape umuhimu wa kwanza. Kwa hiyo, sasa naomba kura zenu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

*(Hapa Mheshimiwa Lucas Selelii aliitwa na kuingia ndani ya Ukumbi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Kwanza shikamooni. *(Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Marahaba.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mimi ndiye Lucas Lumambo Selelii. Nimekuwa Mbunge wa kawaida kwa muda wa miaka kumi iliyopita, naelewa matatizo ya Wabunge na watumishi wao, shida zao na kiu yao. Mimi ni Mnyamwezi, nipeni kazi mnitume, mzigo mzito...

**WABUNGE FULANI:** Mpe Mnyamwezi.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Naomba kura zenu zote. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

*(Hapa Mheshimiwa Raynald Mrope aliitwa na kuingia ndani ya Ukumbi)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, jina langu ni Raynald Alfons Mrope, Mbunge wa Masasi Mkoa wa Mtwara.

Waheshimiwa Wabunge, kama mtakumbuka mwaka jana mwezi Julai katika Bunge hili hili tulijadili hoja kali sana inayohusu kiinua mgongo cha Wabunge. Katika kiinua mgongo kile mimi ndio niliongoza kuhakikisha kwamba Serikali inaongeza kile kiinua mgongo kutoka shilingi milioni 26 na kufikia shilingi milioni 33.

Waheshimiwa Wabunge nilieleza tu kazi mojawapo niliyoifanya, sasa naomba niingie mle ndani ili nichacharike kwa nguvu zote kuhakikisha maslahi ya Wabunge na hali zao yanaimarika katika Bunge hili. Naomba kura zenu Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

*(Hapa Mheshimiwa yahya Kassim Issa aliitwa na kuingia ndani ya Ukumbi)*

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Naibu Mawaziri, niliyesimama mbele yenu hapa naitwa Yahya Kassim Issa. Katika Bunge hili ni kipindi cha tatu na sijapata kuomba nafasi katika Bunge hili. Lakini hivi sasa wakati umefika baada ya uzoefu mkubwa

kuupata katika Bunge hili. Kwa muundo ule ule wa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya na ninakuhakikishieni nitakutumikieni.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wote, naomba kura zenu ili niwawakilisheni katika Bunge hili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, niliyesimama mbele yenu hapa naitwa Abdulkarim Esmail Shah, Mbunge wa Jimbo la Mafia.

Kwa heshima zote nasema hivi, kazi kubwa na jukumu kubwa la kuwa Kamishna katika Tume ya Bunge ni kuhakikisha maslahi ya Waheshimiwa Wabunge yanaboreshwa na kuliimarisha Bunge letu kama yalivyokuwa Mabunge mengine.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge, naombeni kura zenu ili niweze kuwatumikieni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, mimi niliyesimama hapa mbele yenu naitwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mbunge wa Jimbo la Kwela.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wote tutakubaliana kwamba hii ni mara yangu ya kwanza kugombea nafasi ya aina hii na nimegombea kwa sababu nilijisikia kwamba baada ya kuona uongozi wako na msimamo wako, nimefarijika kwamba naweza kuchangia katika kuliimarisha Bunge letu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa niwathibitishie kwa unyenyekevu mkubwa kwamba ikiwa mtaniamini, nitahakikisha kwa kushirikiana na ninyi na wenzangu mtakaotuchagua kwamba tunatazama upya sheria yenyewe iliyounda Tume hii. Kwa sababu sheria yenyewe tangu tumeipitisha haijafanya kazi yake na inahitaji watu wa kuiwezesha ifanye kazi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, kwa unyenyekevu mkubwa naomba kura zenu zote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, karatasi ya kura itakuwa na majina kumi na moja unachagua matatu kati ya hayo kwa sababu wawili wale ni makundi tayari wamepatikana. Kwa hiyo, majina kumi na moja karatasi hii inayopitishwa sasa, unachagua Waheshimiwa Wabunge watatu.

**MHE. HASSAN RAJAB KHATIB:** Mheshimiwa Spika, kuhusu mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Khatib.

**MHE. HASSAN RAJAB KHATIB:** Mheshimiwa Spika, kutokana na uzoefu tuliokuwa nao katika Tume ya Bunge aghalabu huwa anatoka mmoja kutoka Zanzibar. Sasa hii ieleweke vizuri kama huo utaratibu bado upo na bado unaendelea. Itakuwa ni vizuri zaidi kabisa kwa kufanya kazi vizuri zaidi. Ahsante.

**SPIKA:** Katibu hebu rejea yale maelezo yako ya awali, nadhani...

**ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, inasema kwamba tunachagua katika makundi matatu. Nafasi moja, labda nisome yote, moja ni mwakilishi toka Kambi ya Upinzani. Moja, ni mwakilishi toka kundi la wanawake na wajumbe wengine watatu kutoka kwa Wabunge wengine wote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hivyo ndivyo ilivyosimama hivi sasa. Sasa kama tunataka kubadili itabidi kubadili labda kwa uchaguzi mwingine kwa sababu hata kura tumekwishapiga.

Waheshimiwa Wabunge, tumepiga kura sisi sote, basi zikusanywe. Ndiyo zinakusanywa hivyo. Hakikisheni vijana kura zote zinakusanywa. Kura zote zimekusanywa?

**WABUNGE FULANI:** Ndio!

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 9(1) kulitakiwa pia katika kikao hiki tuchague Wenyeviti wawili *(Presiding Officers)*. Hawa hutokana kwa mujibu wa Kanuni hiyo niliyoitamka, hutokana na Wenyeviti wa Kamati yaani kutoka Kamati ya Uongozi. Nimearifiwa kwamba utamaduni umekuwa ni kuiachia kwanza Kamati ya Uongozi ipendekeze na majina yanaletwa hapa na kwa kawaida yanakuwa ni rahisi kukubalika. Badala ya kuwa na majina ya Wenyeviti wetu wote halafu waendeshe kampeni hilo nadhani siku za nyuma mliliona si zuri mkaona ni vyema Kamati ya Uongozi yenyewe wapige kura wakuleteeni majina mawili na kama mnayaafiki basi hao ndio wakubalike kuwa ni Wenyeviti ndani ya Bunge. Mpaka hapo nadhani tunakwenda sawa.

**WABUNGE FULANI:** Sawa.

**SPIKA:** Sasa nawapeni taarifa basi kwamba Kamati ya Uongozi imekaa leo mchana imeifanya hiyo kazi na nina heshima kupendekeza mbele yenu majina hayo mawili yaliyozingatia jinsia.

Kwa upande wa Wabunge wanawake walio Wenyeviti wa Kamati, Kamati ya Uongozi imempigia kura Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho na kwa upande wa Wabunge wanaume Kamati ya Uongozi ilimpigia kura Mheshimiwa Job Ndugai. *(Makofi)*

Kwa makofi hayo nadhani tunakubali uchaguzi au mapendekezo ya Kamati ya Uongozi. *(Makofi)*

Kwa hiyo basi, kwa mpangilio wa jinsia nawaomba Mheshimiwa Jenista Mhagama na baadaye Mheshimiwa Job Ndugai, waje mbele waweze kusema maneno machache ya shukrani kwa kupewa heshima hiyo, karibuni. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Naibu Mawaziri, Mheshimiwa sana Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge na watendaji wote wa Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa ya Bunge lako Tukufu nasimama hapa mbele yako kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wakiongozwa na wewe mwenyewe kwa kukubali kuidhinisha uteuzi wetu uliotokana na Kamati ya Uongozi ya Bunge lako Tukufu. Imani tulioipata kuanzia leo mchana katika Kamati ya Uongozi na inapodhihirishwa na Bunge letu Tukufu inaonyesha ni namna gani tunatakiwa leo kupokea jukumu hili kubwa la kukusaidia wewe Mheshimiwa Spika, kumsaidia Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kusaidiana na Wabunge wengine wote kuendesha shughuli zetu za Bunge kwa ajili ya kuisaidia Serikali yetu na mihimili mingine katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme ninashukuru sana kwa maidhinisho haya yaliyofanyika leo katika kikao chako. Ninaahidi kufanya kazi kwa uaminifu mkubwa na kwa ushirikiano kwa kiasi cha hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Mawaziri wote, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nimesimama hapa kutoa shukrani kubwa sana kwa imani kubwa niliyoipata kutoka kwenye Kamati ya Uongozi kwa Wenyeviti wenzangu. Lakini pili imani kubwa ambayo nimeipata kutoka kwenu Waheshimiwa Wabunge wote ya kunikubali kumsaidia Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika katika kuliendesha Bunge hili.

Nawashukuruni sana na nawahakikishia nitajitahidi sana kuona kwamba mambo yote yanakwenda vizuri na kwa Kanuni na kuanzia leo kazi yangu kubwa ni kusoma Kanuni sasa. *(Makofi)*

Nitawaomba neno moja Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge wenzangu mnisaidie sana nitakapokuwa kwenye kiti kile.

Baada ya kusema hayo naomba niseme ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa Waheshimiwa Wabunge taarifa kutoka chumba cha kuhesabiwa kura ni kwamba makundi yote yamekamilika ila tu hili la mwisho. Kwanza wanastahili pongezi sana mimi sikutazamia hilo. *(Makofi)*

Kundi la *ACP* tayari, kundi la Chuo Kikuu Dar es Salaam tayari, kundi la Chuo Kikuu cha Sokoine tayari, Chuo Kikuu Huria tayari, Chuo Kikuu cha Mzumbe sawia, *SADC* tayari, Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki hilo ilikuwa inajulikana na Bunge la Afrika pia tayari. Wamesalia tu Makamishna wa Tume. Sasa mimi nasubiri kuelewa sijui mna...

**WABUNGE FULANI:** Tangaza!

**SPIKA:** Tutangaze kwanza?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo

**SPIKA:** Lakini kiporo tunakifanyaje? Tukimaliza tu. Sasa Mheshimiwa Amina Mpakanjia una hoja hapo.

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Hoja yangu ni kwamba wakati tunaendelea kusubiri yale matokeo ya kundi la mwisho, tunaomba basi tutajiwe washindi halafu kwa sababu kuna ile shukrani wakiwa wanaendelea kutoa shukrani tutaendelea kusubiri matokeo, wakimaliza majibu yatakuwa tayari. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Spika, tuna tatizo la Kikanuni kwamba tunapaswa kuongeza sio zaidi ya nusu saa kuanzia pale kwenye saa mbili kasoro robo.

Sasa Kanuni hiyo inasema wazi wazi kwamba ombi la kuongeza muda halitazidi nusu saa. Liko wazi kabisa halina ubishi. Kwa hiyo, pengine pendekezo katika dakika zilizobaki basi utangaze haya yaliyopo tukabakiza kile kifungu kidogo tukatangaza kesho. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hilo linaweza kuwa zuri, lakini tatizo sasa la utaratibu wa kutangaza na kuwataka waliopo wengine washukuru na kadhalika. Ndio utaratibu hatuwezi kufanya. Ndiyo maana mimi nashawishika kusema badala ya kuharakisha na hali kundi moja halijakamilishwa katika kuhesabu basi yote tuyafanye pamoja baada ya Kipindi cha Maswali na Majibu na baada ya hapo ndiyo tuipokee Hoja ya Kuahirisha Bunge.

**WABUNGE FULANI:** Sawa.

**SPIKA:** Nadhani hili linaafikiwa, ahsante sana. Kama hilo linaafikiwa, basi sasa naahirisha shughuli za Bunge hadi hapo kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 02.10 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa, Tarehe 17 Februari, 2005 saa tatu asubuhi)*